ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 23 Mei, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe swali la mwazo litaloulizwa ni swali la Wizara ya Fedha na baadae tutarudi kwenye utaratibu. Kwa hivyo, Katibu kwa wizara.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 29

Ubadhirifu wa Fedha kwa watendaji wa Wizara ya Fedha

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kugundua wizi au ubadhirifu kwa watendaji wake ambao umepelekea kusimamishwa kwa baadhi ya watendaji hao, lakini ni muda mrefu mno haijajulikana hatima yake, jambo linalopelekea usumbufu kwa watendaji hao kutoelewa kinachotendeka juu yao, hata baada ya Tume kuchunguza.

(a) Je, nini hatma ya wafanyakazi hao ambao hadi sasa hawajielewi.

(b) Ni makosa gani yaliyobainika katika uchunguzi huo.

(c) Ni hasara ya kiasi gani Serikali imepata kutokana na ubadhirifu huo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali Nam. 29 la Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:

Ni kweli kuwa serikali ilibaini udanganyifu mkubwa uliopelekea upotevu wa Fedha za Umma. Ni kweli pia kuwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iliunda Bodi ya Uchunguzi ili kubaini usahihi, wahusika na kiasi cha

fedha kilichopotea. Na ni kweli pia kuwa Bodi hiyo ya Uchunguzi imekamilisha kazi yake na kuwasilisha Ripoti Wizarani ambayo kimsingi imethibitisha ubadhirifu huo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wafanyakazi waliothibitika kuhusika na wizi huo, hatua za Kisheria na kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao kulingana na kosa kila mmoja alilohusika nalo na uzito wake.

(b) Kuna makosa tofauti yaliyobainika katika uchunguzi huo lakini kubwa zaidi ni njama za udanganyifu zilizopelekea wizi wa fedha za umma kwa kughushi katika mtandao.

(c) Hasara iiyopatikana kutokana na ubadhirifu huo ni TZS 1.1 bilioni.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha ni kweli kumetokea matatizo. Lakini wale wafanyakazi waliohukumiwa kwa kifungu cha nidhamu cha Utumishi wa Umma namba 82 ilipaswa kusimamishwa ndani ya miezi sita na baada ya miezi sita warudishwe kazini au wapewe mshahara kamili.

(a) Je, serikali haikufanya hivyo, huoni umekiuka kifungu cha sheria ya Utumishi wa Umma.

(b) Kama makosa yamebainika ni makosa ya jinai kwa nini hawapelekwi Mahakamani wakahukumiwa ili wakashitakiwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu maswali ya nyengeza kama ifuatavyo:-

(a) Sheria imefuatwa, Sheria ya Utumishi wa Umma namuomba Mheshimiwa asome kifungu cha 84(4) ambacho kinatoa fursa ya kusimamishwa kwa miezi sita kwa malipo nusu. Lakini pia kuna *extension* ya miezi sita mingine kwa malipo nusu vile vile.

(b) Hatua za kinidhamu zitachukuliwa ikiwemo hiyo kusimamishwa, lakini tayari wahusika wote wameshapewa barua ya kujieleza na baada ya kurudisha maelezo yao hatua za kuwashitaki zitachukuliwa.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi nilipenda kumuuliza swali dogo moja la nyongeza linye kitoto (a) na (b).

Kwa kuwa kadhia hii *transaction* yake ina *transfer* inayoendeshwa kwenye mtandao yaani *IFEM* na uendeshaji huu wa mtandano lazima uendane na ruhusa ya mwenye dhamana.

(a) Je, ni kiongozi gani mwenye dhamana kwa wakati huo aliehusika na *transfer* ya fedha hizo.

(b) Inasemekana kuwa wapo Maafisa waliotumiwa fedha hizi walikiri na kutakiwa kurejesha. Je, ni kiasi gani cha fedha kilichorejeshwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu swali la Mhe. Hamida Abdalla Issa, suala la nyongeza lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza wafanyakazi hawa lioshiriki wamefanya makosa tafauti na kila mmoja wao ametakiwa ajieleze kwa mujibu wa kosa alilolifanya. Si kosa la uhaulishaji tu kuna wafanyakazi waliohusika na uhaulishaji lakini wapo wafanyakazi waliohusika na kufuta kumbukumbu kwenye ule mtandao wenyewe ni makosa tafauti na wote tumewataka wajieleze, mmoja ndie aliehusika na *transfer* wa hizo fedha. Lakini wengine walihusika kwa namna ya kufuta kumbukumbu lakini wengine walihusishwa na hao viongozi wao kwa maana ya kutumwa kwenda kuvunja *cheque* kwa kila mtu ana kosa lake na uzito wake.

Mhe. Spika, samahani naomba alirejee lile la pili.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Inasemekana kuwa wapo maafisa waliotumiwa fedha hizi walikiri na walitakwa wazirejeshe. Je, ni kiasi gani mpaka sasa kilichorejeshwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kujibu swali lake (b) la nyongeza kama ifuaatavyo.

(b) Ni kweli kwanza wapo waliokiri kwa maandishi kuhusika na njama hiyo, lakini vile vile katika hao waliokiri wapo walionza kurudisha fedha. Lakini kima kilichorudishwa si kikubwa na sina takwimu halisi ya kima

kilichorudishwa hadi leo. Kwa hivyo, kwa kima kilichorudishwa nitaomba kumletea kwa maandishi.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, kwanza nataka kukushuru na mimi nataka kumuuliza swala dogo la nyongeza kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri kutokana na kadhia iliyojitokeza na serikali yetu ina mikakati ya kubana matumizi na kuzuaia ubadhirifu wa serikali. Je, wizara yako ina mpango gani madhubuti kuzuia suala kama hili lisijitokeze tena ili kuitia aibu wizara yako.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, moja ya mikakati ambayo tunachukuwa ni kuzidi kuwaelimisha watendaji wetu kuepukana na tabia ya ubadhirifu wa fedha za umma na kazi hiyo tunaifanya kwa taasisi zote na hasa wakiwemo na wale wanaohusika na masuala ya uhasibu na washika fedha. Lakini pia wale wanaohusika na ukusanyaji wa mapato hilo ni moja.

Lakini la pili tunafuatilia kwa karibu zaidi mtandao wenyewe utafanyiwa marekebisho tuta-*install* mtandao mpya ambao utakuwa na uhakika zaidi maana yake sisemi 100% uhakika zaidi wa kudhibiti ubadhirifu wa nama hii. Lakini na kwa wale watakaokuwa wanahusika na matatizo ya aina hii hatua kali za kisheria zitachukuliwa na mbali ya hawa katika kipindi kijacho kisichozidi wiki mbili tunaweza tukatoa taarifa ziadi za wahusika wengine wa matukio kama haya katika sehemu nyengine za kazi. Kwa hiyo, hatua hizi zinachukuliwa na wote watakaohusika watachukuliwa hatua kali za kinidhamu. Lakini la msingi ni taaluma ili watu wabadilike na waachane na tabia hizi za ubadhirifu.

Nam. 70

Adhabu kwa Gari zinazoegeshwa maeneo yasiyohusika

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**

Hivi karibuni Baraza la Manispaa limeanzisha utaratibu mzuri wa kudhibiti gari zinazoegeshwa maeneo yasiyoruhusiwa hasa maeneo ya Mji Mkongwe. Pamoja na utaratibu huo kuwa mzuri, kumekuwa na mapungufu katika utekelezaji wake kwa baadhi ya watendaji wa Baraza la Manispaa wanaohusika

na shughuli hiyo kufanya vitendo vya kubagua gari gani za kuzichukulia hatua na zipi za kuziacha. Nimeshuhudia baadhi ya watu wanaonekana wana fedha wanachukuliwa hatua haraka wanapoegesha eneo lisilohusika ambalo hapo hapo kuna gari nyengine zimeegeshwa bila kuchukuliwa hatua za kufungwa vyuma kwenye maringi.

(a) Baraza la Manispaa lipo tayari kufanya uchunguzi kubaini na kudhibiti vitendo kama hivyo vya ubaguzi.

(b) Endapo dereva atakuwa na malalamiko dhidi ya hatua zisizostahiki za maafisa wa Manispaa, utaratibu gani atumie ili kuwasilisha malalamika na kuchukuliwa hatua.

(c) Baadhi ya maeneo yasiyoruhusiwa kuegesha yanakuwa hayana alama badala yake madereva wanapata usumbufu wa kufungwa gari zao, Baraza halioni umuhimu wa kuweka alama za maegesho na kama hazitawekwa wasichukuwe hatua kwa dereva kama ataegesha eneo lisilokuwa na alama.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Baraza la Manispaa kama taasisi nyengine za serikali linao wajibu wa kusimamia utendaji wa watumishi wake ili waweze kutoa huduma bora na kwa wakati kwa wananchi bila ya upendeleo au namna yoyote ile ya ubaguzi. Baraza linafanya hivyo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma zinazoelekeza watumishi kufanyakazi kwa ufanisi, uweledi na uadilifu. Hivyo basi, Baraza lipo tayari siku zote kushirikiana na raia wema kufichua vitendo vyo vyote kwa mfanyakazi yeyote anayekwenda kinyume na Sheria na Kanuni za Utumishi na hatimae kuchukulia hatua zinazostahiki.

(b) Dereva au mwananchi yeyote yule atakapokuwa na malalamiko dhidi ya mfanyakazi au matendo ya mfanyakazi kwa niaba ya Baraza, anaweza kuwasilisha malalamiko yake kimaandishi au kufika ofisini ili kuweza kuchukuliwa hatua. Baraza la Manispaa linalo Dawati maalumu la kuhudumia wateja ikiwa ni pamoja na kusikiliza malalamiko ya wananchi ili kuyapatia ufumbuzi au kutoa muongozo.

(c) Ni dhahiri kuwa suala kuweka alama barabarani za kuwaongoza watumiaji wa barabara lina umuhimu mkubwa. Baraza linakiri kuwa pasina kuwepo kwa alama za barabarani zikiwemo zile zinazoelekeza maeneo ya kuegesha gari kunawaletea usumbufu mkubwa madereva na watumiaji wengine wa barabara. Aidha, Baraza linakiri pia kuwa baadhi ya maeneo ambayo yanastahiki kuwepo kwa alama, alama hizo hivi sasa hazipo kwa sababu mbali mbali. Hivyo basi, kwa kutambua umuhimu wa alama hizo, Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Usalama Barabarani na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara litayapitia maeneo yote ya Mji ili kulifanyia kazi suala hili inavyostahiki. Aidha, kwa upande wa Mji Mkongwe, Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe ipo katika hatua za kuyatambua na kuainisha rasmi maeneo ya maegesho ya gari katika eneo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri. Mhe. Spika, suala hili lilikuwa linapigiwa kelele sana wacha kwa Wawakilishi kadhia hii inawakuta lakini hata wananchi. Mimi kwa kushuhudia kwa macho yangu na Mwenyezi Mungu shahidi kuna gari ya mtu inafungwa na nyengine kuachwa. Juzi tu katika vifungu hapa nakushukuru ulijibu kuwa wenye mamlaka ya ni Manispaa, lakini inaonekana kwamba Manispaa haya majukumu yameshawashanda au wanauza kwa watu wengine.

(a) Je, unatoa wito gani kwa watendaji wako.

(b) Hebu nieleze Katiba yetu ya Zanzibar hii inasema binaadamu wote wote ni sawa, kuna sababu gani gari ya SMZ kutokufungwa na gari ya Mhe. Waziri kutokufungwa ikawa ya Mwakilishi inafungwa tunafanya nini na jamii inatuelewa nini na haya mambo yanageuka Mhe. Waziri leo uko mbele kesho utakuwa nyuma mimi nitakuja mbele. Lakini Mweneyezi Mungu asije kunijaali kuja mbele...

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala lake la nyongeza lenye a na b kama ifuatavyo:-

(a) Kama nilivyoeleza kwenye jibu mama kama yuko mtumishi yoyote ambaye anakwenda kinyume na taratibu za kikazi au za sheria za kiutumishi

basi huyo mtumishi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na mamlaka ya nidhamu inayohusika na mtumishi huyo.

(b) Lakini kwa nini gari nyengine zinafungwa nyengine hazifungwi. Kama hilo linatokea basi ni dhahiri kwamba watumishi wanaofanya kazi hizo hawako katika uadilifu na kama lipo basi Ofisi yangu itawasiliana na taasisi husika ili kuwabaini hao watumishi na tuweze kuwachakulia hatua.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunijaalia niweze kuuliza swali ya nyongeza. Naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa eneo la maegesho mara nyingi sana ni lile ambalo limetayarishwa na taasisi husika. Lakini leo naona hata barabarani mtu anaegesha gari anatozwa ushuru. Ni sababu zipi za msingi kutozwa ushuru ambapo ni eneo la barabarani na sio la Manispaa waliolitayarisha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Napenda Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waelewe kwamba utaratibu wa maegesho ni vyema ungekuwa katika maeneo maalum ambayo yamepangwa. Lakini kwa sababu tuna upungufu hasa katika eneo la Mji Mkongwe ndio maana nimesema kwenye jibu langu mama kwamba hivi sasa tunashirikiana na Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji mkongwe ili kuyabainisha maeneo halisi ya maegesho ya magari katika eneo la Mji Mkongwe na maeneo mengine ya jirani.

Lakini kwa sababu Baraza la Manispaa kazi yake ni kutoa huduma na kazi yake kutoza ada za *service charge* katika mji wake magari yanaegeshwa katika barabara isingekuwa vyema kama sisi tungeacha magari hayo yakiendelea kuegeshwa na bila ya kuyatoza ada inayostahiki. Kwa sababu maeneo maalum ya kuegesha hayapo. Kwa hivyo, tungeamua kuacha maana yake magari yangeegeshwa mengi zaidi kuliko yale yanayoegeshwa. Lakini kwa sababu tuna *control* ndio maana tunatoza ada lakini mpaka hapo tutakapoweze kuyabainisha maeneo maalum ya maegesho basi gari hazitaegeshwa barabarani. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa naomba kuuliza swala la nyongeza.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Waziri kwamba mji wowote una taratibu zake na kwenye *parking* zozote huweko na alama. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri kwa kuwa Baraza la Mji linafanya kazi zake pindi mtu akiteleza kidogo akiweka gari bila ya muelekeo inafungwa pingu ambayo akalipe ndio apate gari yake suala langu liko hapa.

Kwa kuwa katika barabara yoyote kuna alama usipite eneo hili, usipitishe gari, usiweke gari kwa muda huu kuondoa adha hiyo hata katika maeneo yasiyostahiki huoni ni vyema pakawekwa alama kwamba hapa usiegeshe gari ili watu wakaondokana na adha hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kijitoupele suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu suala langu mama kwamba baadhi ya maeneo hazimo hizo alama na hazimo si kwamba serikali haikuwa kuziweka. Serikali imeziweka lakini baadhi ya wananchi wasio kuwa wema wamezitoa na kuziiba alama hizo.

Hata hivyo, serikali ina mpango wa kuyapitia maeneo yote yanastahiki kuwekwa alama ili ziweze kuwekwa alama za barabarani, lakini wazo lake ni zuri na nadhani katika majibu yangu mama nilisema kwamba nia ya serikali ni nini.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi avute subira ili hiyo kazi inayofanywa kwa pamoja kati ya Jeshi la Polisi, Usalama Barabarani, Idara ya Utunzaji Barabara pamoja na Baraza la Manispaa na Mji Mkongwe ikamilike ili tuweze kuyabainisha hayo maeneo na tuyarejeshee alama ambazo zilikuwepo hapo mwanzo. Ahsante sana.

Nam. 97

Malipo Yanayokusanywa na Wakala wa Ukaguzi wa Zbs Nchini Dubai

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Taasisi ya Viwango Zanzibar inawakilishwa na kitengo cha ukaguzi kule Dubai, kitengo hicho kimekuwa kinafanyakazi za ukaguzi na kukusanya mapato ya kazi hiyo.

(a) Je, tangu kitengo hicho kupewa mamlaka hayo ya kukusanya, kimekusanya kiasi gani cha mapato.

(b) Je, ni utaratibu upi unafanyika Serikali kupatiwa mapato hayo.

(c) Kwa nini Kitengo hicho kinashikilia wafanyabiashara kulipia gharama za ukaguzi wakiwa Dubai badala ya Zanzibar kama wanapenda kufanya hivyo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji (Kny: Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 97 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu utaratibu wa ukaguzi wa ubora wa bidhaa unaotekelezwa nje ya nchi.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa Zanzibar itakuwa salama na bidhaa zisizo na viwango kuzuiliwa, Taasisi ya Viwango vya Zanzibar yaani *Zanzibar Bureau Standard* (*ZBS*) imeanza utekelzaji wa mfumo wa ukaguzi wa ubora wa bidhaa kabla ya kuingizwa nchini kutoka nje ya nchi yaani "*Pre Export Verification of Conformity (PVoC)*".

PVoC ni mfumo wa ukaguzi, uhakiki na uthibiti ubora wa bidhaa zinzotokana nje ya nchi kwamba zinakidhi matakwa ya viwango vya Kitaifa au Kimataifa kabla ya kusafirishwa na kuingizwa nchini.

Mfumo huu unatumika katika nchi nyingi duniani kwa kukuza biashara pamoja na kuharakisha uondoaji wa matatizo ya bidhaa ambazo sio salama na kuhakikisha kwamba hizi bidhaa zinakuwa zenye ubora pale zinapowasili bandarini na hatimae kuwalinda walaji au niseme walaji na watumiaji, yaani *consumers.*

Mhe. Spika, baada ya kukamilika kwa taratibu za zabuni, *ZBS* iliwateua pamoja na kusaini mkataba na mawakala wafuatao kwa ajili ya kufanya ukaguzi kupitia mfumo huu wa *PVoC*.

Kwa bidhaa zisizokuwa vyombo vya moto (*general goods*), mawakala wa Ukaguzi ni:-

(a) *SGS*

(b) *Bereau Veritas*,
(c) *China Certification and Inspection Group Company Limited (CCIC*).

Na kwa upande wa bidhaa za vyombo vya moto vilivyotumika ni:-

(a) Jabal Kilimanjaro Auto Mech – Kwa magari yanayotoka Umoja wa Falme za Kiarabu (*UAE*).
(b) *East Africa Auto Service Co. LTD (EAA)* hii kwa upande wa East Africa, na ni kwa ajili ya magari yanayotoka Japan, Singapore, Hong Kong na UK.

Utekelezwaji wa mfumo huu ulianza rasmi tarehe 01/08/2016 kwa upande wa vyombo vya moto vilivyotumika (magari) na tarehe 01/11/2016 kwa bidhaa zisizokuwa vyombo vya moto vilivyotumika (*general goods*).

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mpaka kufikia mwezi Machi 2017, tangu mfumo huu wa ukaguzi kupitia kwa Wakala wetu wa Dubai ambae ni *Kampuni ya Jabal Kilimanjaro Auto Mech*, ambao wanahusika na kufanya shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto vilivyotumika, jumla ya magari 648 yamekaguliwa na kupewa cheti cha Uthibiti Ubora. Ukaguzi huo umepelekea kukusanya kiasi cha Dola za Kimarekani 81,000 kama tozo ya ukaguzi kwa vyombo hivyo.

(b) Kwa mujibu wa Mkataba baina ya *ZBS* na Wakala husika wa ukaguzi, inampasa kila mwisho wa mwezi awasilishe "*Administrative fee*" ambayo ni asilimia 30 ya mapato anayokusanya kama ni tozo ya ukaguzi kwa vyombo vya moto vilivyotumika vinavyongizwa Zanzibar.

(c) *ZBS* inawataka wafanyabiashara kufanya ukaguzi wa bidhaa zao nje ya nchi kabla ya kusafirisha na kuziingiza nchini kwa sababu zifuatazo:-

- Kukabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo upungufu wa vifaa vya maabara pamoja na kukosekana kwa baadhi ya maabara hizo, kutokuwa na wataalamu wa kutosha pamoja na taaluma ya kutosha ya ukaguzi pamoja na upimaji kwa baadhi ya bidhaa hizo. Yaani hizo ni changamoto tunazo hapa nchini, ukosefu huo na udhaifu huo tunao hapa nchini.

- Kukosekana imani kwa watumiaji wa bidhaa nchini juu ya ubora wa bidhaa ambazo zilizopo katika soko la Zanzibar.

- Kufuata taratibu na matakwa ya utekelezaji wa mfumo huu kama yalivyoainishwa katika mkataba baina ya *ZBS* na Wakala husika na Ukaguzi.

- Kuepusha usumbufu na vikwazo visivyo vya lazima ambavyo vinaweza kukwamisha biashara.

- Kurahisisha biashara.

- Kuenda smbamba na maamuzi ya Kikanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba nchi wanachama watumie mfumo wa *PVoC* katika kurahisisha biashara pamoja na kuwalinda watumiaji.

Mhe. Spika, ikiwa msafirishaji hakukaguliwa kwa mfumo huu na bidhaa yake imo katika orodha inayohusika na mfumo huu, itampasa kulipa faini ya 15% ya gharama ya shehena ya mzigo *cost insurance of freight* (*CIF*) pamoja na gharama zote za ukaguzi. Iwapo baada ya ukaguzi huu na baada ya bidhaa kufika bandarini itabainika kuwa iko hafifu, yaani iko chini ya kiwango husika, muingizaji wa bidhaa hiyo atalazimika kuirejesha katika nchi aliyoitoa au kulipia gharama za uangamizaji wa hizo bidhaa.

Mhe. Spika, nafikiri nimejibu swali kwa ukamilifu.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri majibu yalikuwa marefu mno, lakini pamoja na hivyo naomba sasa nimpe swali la nyongeza Mhe. Jaku Hashim.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na kanuni ulizotupa Mhe. Spika, ya 37. Mhe. Waziri, mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa kwa maswali aliyoulizwa Mhe. Waziri linaweza kujibiwa na mtu mwengine. Muda wa maswali ambayo kwa ufupi, ingawa

Mhe. Spika: Mhe. Jaku hujaomba utaratibu nimekunyanyua uulize swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante. Nimpongeze kwanza Mhe. Waziri, mimi kwanza nimeuliza hapa nikaambiwa mara tatu ukishakujibu hoja, na

inaonekana hapo tarehe 30 ataanza kujibu hoja vizuri, nimpongeze sana Mhe. Waziri. Lakini pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza maswali madogo tu ya nyongeza yenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Spika, mkataba huu Mhe. Waziri wa miaka mingapi hiyo kampuni mliowapa na je, wizara iko tayari kumuweka mwekezaji wa hapa Zanzibar badala ya kuweka huko nje mtu akafungua kitengo chake hiki, na kama ninavyosemwa sadaka inaanza nyumbani na taa unawasha ndani ya nyumba kabla ya kuwasha nje. Mko tayari kumtafuta mwekezaji mzalendo akawekeza hapa mradi huo badala ya kuweko nje, ili serikali ikapata kuona ukweli na uhakika hali ilivyo.

(b) Hebu tuambie Mhe. Waziri serikali inapata asilimia ngapi na kampuni hizo mlizoajiri huko zinapata asilimia ngapi, iliyokuwepo huko Dubai.

Vile vile katika kitengo hicho huko Dubai unalipa na ukifika hapa kuna kitengo cha *food drugs* nako unalipa. Hamuoni ng'ombe mmoja anatoa lita tatu za maziwa baadae unamlazimisha lita sita.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji (Kny: Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwanza kabisa nataka Baraza lako tukufu lielewe kwamba mimi sio Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Mimi nimesimama hapa kujibu kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, nikiwa kaimu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Napenda kukuhakikishia Mhe. Spika, kwamba maswali haya yaliyoulizwa mengine ni ya kitaalamu na nitayajibu yale ambayo naweza nikayajibu. Nitaanza na swali lile alilouliza Mhe. Mjumbe kwamba ni kiasi gani serikali inapata katika pato lile. Nilikwisha eleza hapa kwamba serikali inapokea asilimia 30 kwa 100 ya makusanyo, yaani yule bwana akikusanya dola 100 sisi tunapewa dola 30. Natumai hakutokua na swali la nyongeza kwenye hilo.

Swali la pili la nyongeza linaulizia kuhusu uwezekano wa kuwa na kitengo kama hicho cha kuangalia ubora wa bidhaa hapa Zanzibar. Mhe. Spika, naamini wazi kwamba Mhe. Mjumbe nilipokuwa namjibu swali nilieleza hapa kwa nini ikawa tunatia mikataba na makampuni ya nje, kwa sababu hapa kwetu Zanzibar uwezo huo hatuna.

Swali la nyongeza ni kwamba je, inawezekana tukapata kampuni za kizalendo zikafanya kazi hiyo. Hilo linawezekana lakini nataka kukumbusha tena Mhe.

Spika, kwamba katika kutoa majibu nilitoa majibu hapa kwamba ni vyema vitu hivyo vinavyokuja Zanzibar viangaliwe huko huko, kwa sababu vikionekana kwamba havifai kuja hapa haviletwi. Kulikoni kuwa na kampuni hapa Zanzibar ya kizalendo ije hapa vitu vimeshafika hapa halafu wakisema vime- *fail* itabidi virejeshwe huko vinakotoka au viteketezwe kwa gharama ya ziada. Mimi nashauri kwamba bora tuendelee hivi na masuala ya mikataba na makampuni za nje, yaani tunaangalia ubora wa viwango huko huko mali inapotoka, yaani *from the source*.

Mkataba huu ulitiwa sahihi sijui ni miaka mingapi, lakini jibu lake nitakuletea kwa maandishi. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, swali hili limechukua muda mwingi mno, Katibu tuendelee na swali linalofuata. Katibu. *(Makofi)*

Nam. 38

Unyang'anyaji wa Viwanja vya Mpira kwa Vijana

Mhe. Shaibu Said Ali - Aliuliza:-

Moja kati ya njia nzuri ya kuwaepusha vijana na mambo ya uvunjifu wa amani kama ulevi, wizi na uasharati ni kuwakusanya kupitia michezo. Moja kati ya michezo hiyo ni mchezo wa mpira wa miguu. Lakini hivi sasa kumezuka wimbi kubwa la watu kuwanyang'anya vijana viwanja wanavyotumia wakidai ni ardhi zao walizozimiliki kwa njia yoyote ile.

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu suala hili.

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kisheria unaowawezesha vijana hao kumiliki viwanja hivyo ili waweze kujiepusha na vitendo hivyo viovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa, moja kati ya njia nzuri ya kuwepusha vijana na mambo ya uvunjifu wa amani kama vile ulevi, wizi na uasharati ni kuwakusanya kupitia michezo, mpira wa miguu ni moja kati ya michezo hiyo. Pia ni kweli kuwa, sasa kumezuka vimbi kubwa la watu

kuwanyang'anya vijana viwanja wanavyotumia wakidai kuwa ni ardhi zao walizozimiliki kwa njia wanazojua wao.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ardhi yote ni mali ya serikali na suala la umiliki wa ardhi lipo chini ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Hivi sasa hakuna tamko lililotolewa na serikali, lakini tayari suala la serikali kutenga maeneo ya wazi ya michezo kwa kila wilaya linafanyiwa kazi, ambalo litakwenda sambamba na mipngo miji na vijiji na tayari limesahaingizwa ndani ya rasimu ya Sera ya Michezo na itakapokamilika tamko litatolewa rasmi.

(b) Mhe. Spika, tayari utaratibu wa kisheria wa kuvulinda viwanja visivamiwe na kuvimiliki umeshaandaliwa ili vijana waweze kuvitumia kwa shughuli za michezo.

Mhe. Shaibu Said Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, hivi sasa tayari vijana hao wameshanyang'anywa viwanja vyao au ardhi hiyo. Je, ni utaratibu gani watumie vijana hao ili kurudishiwa viwanja hivyo haraka sana iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, napenda kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Shaibu Said Ali kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, utaratibu ambao upo kwa sasa ili kurejeshewa viwanja vyao wale ambao wamenyang'anywa viwanja hivi ni kwamba, sasa hivi tayari tumeshashirikiana na watu wa ardhi na pale ambapo madai yao wale ambao wamenyang'anywa viwanja vile wanapoleta madai basi tunashirikiana kwa pamoja na tunasimamia.

Kwa mfano, Kaskazini lilijitokeza suala kama hili, kuna mwananchi alijitokeza kujenga katika kiwanja cha skuli karibu na goli, kiwanja hiki walirejeshewa wenyewe na sasa hivi wanatumia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali mama na la nyongeza. Mhe. Spika,

kwa kuwa viwanja vingi na hususan vilivyomo mawilayani na mikoani havina hati miliki na Mhe. Waziri tayari amesema kwamba wamo katika mipango ya sheria kuhusiana na suala hili, lakini uvamizi au kunyang'anywa bado kunaendelea.

Je, ni tahadhari gani ambazo watazichukua ili kuwatanabahisha hao wenye viwanja kuweza kufuatilia hati miliki za viwanja vyao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, napenda kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, tahadhari ambayo wizara inachukua kwa sasa. Kwanza napenda Mhe. Mjumbe atambuwe kwamba umiliki wa ardhi ni watu wenyewe au ni Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba utaratibu ambao tunao sasa hivi, sisi Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ni watumiaji tu wa viwanja. Juhudi iliopo na tahadhari sasa hivi tutazungumza na wamiliki wa viwanja na sheria tayari ipo wafuatilie ili wapate hati miliki za viwanja vyao na kuondosha migogoro ambayo inatokea siku hadi siku. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa nchi nyingi sana huweka katika kila miji kama vile mikoa yetu viwanja mfano Uwanja wa Amani. Ni lini sasa wizara imejipanga kujenga kila mkoa kiwanja ambacho kitafanana na Uwanja wa Amani, ili katika kila mkoa kuwe na kiwanja chake.

(b) Kwa kuwa suala la michezo ni muhimu na hasa kwa upande wa wenzetu nyumbani shamba, wanahitaji pia kucheza mpira usiku na wanawaona wenzao wanacheza mpira usiku mjini na sehemu nyenginezo. Mfano Uzini, mimi kwa upande wa Jimbo la Chaani nimewatilia taa za usiku viwanja vitatu vya mpira.

Lakini Je, Mhe. Waziri ni lini sasa utasaidia kwa upande wa michezo kuja kuvuta umeme wa 3 *phase* ili zile taa ziwake kwa nguvu kuliko sasa hivi hazina nguvu za kucheza mpira usiku.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu a na b kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, ametaka kujua ni lini wizara itachukua hatua za kujenga viwanja katika Wilaya nimjibu Mhe. Nadir kwamba sasa hivi Serikali tayari imo katika mpango huu na sasa hivi tuna viwanja vya Fukuchani, lakini hata kwa kule Pemba tayari ujenzi huu upo Wilaya ya Wete kipo kiwanja cha Wilaya lakini vile vile kuna endelevu ambazo sasa hivi tunaendelea kuvijenga viwanja hivi na kwa upande wa Wilaya ya Micheweni pia kitajengwa maeneo ya Finya, naomba nimfahamishe mjumbe kwamba utaratibu huu unaendelea.

b) Mhe. Spika, naomba suala (b) arejee.

Mhe. Waziri wa Utalii, Utamaduni na Micheo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa umahiri wake wea kujibu maswali, naendelea kumpongeza na kumpa moyo kwamba aendelee na msimamo wa kujibu masuala ambayo tayari ameshayafuatilia kama anavyofanya Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri.

Lakini baada ya hayo Mhe. Spika, naomba nijibu masuala mawili ya nyongeza kama kanuni zetu zinavyoelekeza.

Suala la kwanza napenda kuliweka sawa tu kidogo kwa mujibu wa alivyolijibu Mhe. Naibu Waziri kwamba alitaka kujua ni lini tutajenga viwanja kwenye Mikoa yetu yote tutakuwa na viwanja hivyo vya kuchezea mpira kama kilivyo kiwanja cha Amani. Nataka kukuthibitishia Mhe. Naibu Spika, na kumhakikishia Mhe. Nadir kwamba Serikali inapanga mipango kwa mujibu wa bajeti ambazo tunazipitisha hapa mwaka hadi mwaka, Serikali inafuata ilani ya uchaguzi wa Chama chetu cha Mapinduzi ya mwaka 2015 mpaka 2020, kwa hivyo ndani ya ilani ya mwaka 2015/2020 Serikali ina mpango wa kujenga viwanja vitatu ndani ya Wilaya zote hapa viwanja ambavyo vitakuwa na hadhi si sawa sawa na Amani, lakini vitakuwa na ubora kwa uchezaji wa mpira. Kwa hivyo kwa mpango huo tutasubiri mpaka labda itakapoingizwa katika ilani tunaweza tukafanya hilo suala la viwanja vya Mikoa vyenye hadhi kama Amani.

Lakini nataka kumwambia Mhe. Nadir endapo kuna wafadhili kuna watu ambao wapo tayari kuja kutujengea viwanja kama hivi kama tulivyopata ufadhili wa Gombani, na ufadhili kutoka kwa Jamhuri ya watu wa China kwa

viwanja vya Amani, Wizara inakaribisha na Serikali haitasita kuchukua ufadhili huo kuendeleza kujenga viwanja.

Suala lake la pili aliuliza ni lini tunaweza kuwa na hadhi ya kucheza mipira usiku, kwanza nimshukuru sana Muwakilishi wa Jimbo la Uzini ambae ameonyesha mifano hiyo na yeye ameweza kuweka baadhi viwanja kuweka taa, taa za Amani zinarekebishwa siku hadi siku ili kuongeza muangaza, suala la *3 phase* moto unaofika pale ni *3 phase* na una uwezo mkubwa kabisa kuonesha mataa yale.

Nam. 20

Ununuzi wa Meli ya Uvuvi

Mhe. Said Omar Said – Aliuliza:

Ili kuendeleza sekta ya uvuvi, ni muhimu kuwa na meli itakayoweza kufika na kuvua bahari kuu.

Lini Serikali itanunua meli ya uvuvi hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ili kuendeleza sekta ya Uvuvi, imeanzisha Kampuni mpya ya Uvuvi inayojulikana kwa jina la *ZAFICO* ambayo itakuwa na malengo yafuatayo:-

1. Ununuzi wa meli 2 za uvuvi pamoja na kuingia ubia na makampuni ya ndani na nje ambayo tayari yameonesha nia ya kuekeza katika sekta hii nchini kwetu.

2. Kuongeza ajira has kwa vijana na kukuza kipato cha wananchi.

3. Kuongeza upatikanaji wa samaki sambamba na uwepo uhakika wa chakula, lishe na afya ya jamii na uanzishaji wa viwanda vya kusarifia samaki.

4. Kuwawezesha wavuvi wetu wadogo wadogo kuvua katika bahari ya kina kirefu cha maji.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Spika. pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifutavyo:

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri anayonipatia tokea jana na leo hii.

a) Lakini nilitaka nijue tu ni maandalizi gani ambayo Serikali imefanya kabla ya kununua na kufika kwa meli hiyo.

b) Kwa kuwa mazungumzo haya yapo kwa muda mrefu hapa sasa leo Wazanzibari wanataka wajue lini hasa hii meli yao itafika hapa na waanze kuitumia.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nataka nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein utaratibu wake wa kufanya kazi inapotolewa ahadi yoyote huwa anatoa *time table*, mara hii alituambia tarehe 30 Machi, ahakikishe kampuni imeundwa na tarehe 30 Machi, tulimkabidhi rasmi uundwani wa kampuni hiyo.

Hatua ya pili ni kuundwa kwa bodi ya wadhamini kazi ambayo sasa tunasubiri tu uteuzi wa Mwenyekiti na bodi iweze kuundwa.
Hatua ya tatu ni upatikanaji wa fedha ambapo nataka niyashukuru sana mashirika yetu ya ZSSF, Bandari, PBZ, Mamlaka ya Usafiri wa Anga kwa kuweza kuchangia kuwa kama *Share holders* na kutoa bilioni saba katika kuanzisha kampuni hiyo. Baada ya hatua hiyo bodi itakutana na hatimae wataanza kupanga utaratibu wa kufanya kazi ikiwa ni pamoja na namna bora ya kuweza kununua meli zitakazostahiki kufanya hiyo iliyokusudiwa. Kwa bahati nzuri Mhe. Rais kwa ushauri wake yeye mwenyewe alituteulia mtaalam na mtaalam huyo ametusaidia sana katika kutushauri namna gani ya kupata meli ambazo zinaweza kufanya kazi mbili za muhimu.

Kwanza kufundisha vijana wetu lakini ya pili kufanya utafiti wa kujua kiwango cha samaki ambao wapo na aina ya samaki ambao tunaweza kuwavua, kwa hivyo nasema maandalizi yapo na yanaendelea vizuri wala msiwe na wasiwasi

katika kipindi kifupi kijacho mtapata program kamili ya lini mambo haya yatafanyika, baada ya bodi yenyewe ya wadhamini kukutana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri wa Kilimo na masuala yote ya uvuvi. Mheshimiwa kama tunakumbuka Zanzibar hapo zamani tulikuwa tuna shirika letu la uvuvi na tulikuwa tunapata samaki wa kupimiwa kwa ratili, shirika lile sasa halipo na ilikuwa kila usubuhi tuna uhakika wa kula samaki kununua katika vibanda kwa ratili.

Je, Mheshimiwa kama tulivyokuwa hapo zamani lini utaturudishia lile Shirika letu la uvuvi ili tukavue samaki na tuweze kuwatumia kama tulivyokuwa nao zamani.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kama Mheshimiwa amenisikiliza vizuri nilitamka wazi kwamba kampuni iliyoundwa inaitwa *ZAFICO* sawa na jina la kampuni liliyokuwepo hapo zamani ilikuwa ikiitwa hivyo hivyo *ZAFICO* hilo la kwanza. Lakini la pili kama umefuatilia hutuba yangu ya mwaka jana tulizungumzia suala la ujenzi soko la Malindi ambalo litakuwa la kisasa la kuweza kuhifadhi samaki, vile vile meli hizo zitakazovua na kuleta samaki kuwakuwa na uwezo wa kuhifadhi samaki, kupima samaki na kuingia katika utaratibu bora wa kuuza samaki kuliko tunaoutumia hivi sasa.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika kipindi cha miezi sita ijayo nahakikisha kabisa mambo yote yatakuwa yametulia na wananchi wataona matunda ya kuundwa kwa meli hizi, kwa sababu kila kitu kipo tunangoja tu bodi ianze kazi yake.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza suala la nyongeza, lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake, pamoja na majibu hayo naomba kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametueleza kwamba mwezi Machi mwaka huu wameunda kampuni ya *ZAFICO* lakini suala langu liko hapa.

a) Je, hivi sasa wazee anatwambia ndio kwanza wanaunda bodi na Rais atangaze Mwenyekiti, bodi haijakutana lakini anatwambia mpango wa kununua meli je, haoni kama mpango huu ni hewa na unaweza kuchukua hata miaka mitatu au minne haujatekelezwa.

b) Kwa muda mrefu kama alivyotuahidi mwaka jana kwamba kutakuwa na soko la samaki na wananchi watapata samaki vizuri kama zilivyo nchi za visiwa au zenye bahari ambazo ukienda wana masoko mazuri tu ya samaki na mwananchi wanaweza kupata faida nzuri. Ni lini mradi huu utaanza kwa sababu tunaona kama unasuasua hii kauli ya miezi sita si kwa ajili ya kupitisha bajeti yake tu ambayo inasomwa wiki hii.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kama ifutavyo:

Kwanza Mhe. Spika, nilisema kwamba utaratibu aliouanzisha Mhe. Rais kwa ufanyaji kazi ni tofauti sana na huko nyuma sasa hivi anahakikisha kabisa kila ahadi iliyotolewa iwe ndani ya Baraza la Mapinduzi, iwe ndani ya Baraza la Wawakilishi iwe yeye mwenyewe kataka ilani anazifuatilia kwa utaratibu ambao amejiwekea kila mwezi angalau mara moja tunakutana kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa jambo linalohusika. Kwa maana hiyo nina hakika kabisa utekelezaji utakuwa mzuri.

Lakini nataka niwapongeze vile vile Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mmetimiza wajibu wenu wa kikatiba wa kuibana Serikali katika kufuatilia maagizo ya ahadi za Serikali, na kila wakati mnatutaka tutoe ahadi tunazotoa tutoe majibu hapa. Sasa mimi naomba hebu mtupe muda mtizame katika kipindi hicho cha miezi sita ninayokwambieni kwamba kweli hamtoziona meli.

Ujenzi wa Soko Malindi dola milioni 3.5 zimechangwa Serikali yenyewe ya Mapinduzi ya Zanzibar dola 12.5 zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi imetoa dola milioni 1, vifaa mkandarasi ameshachaguliwa tumeshawasiliana na watu wa *UNESCO* ili kupata idhini ya kujenga pale pahala tumeshapa idhini zote hizo michoro ipo tayari na mkandarasi wakati wowote ataanza kazi na unasimamiwa na *JAICA* pamoja *FAO* hiyo ni miradi inafanyika. Sambamba na hiyo ili kuhakikisha kabisa tunapata samaki wa kutosha, tumeanzisha kitoa cha kuzalisha vifaranga vya samaki ili ndugu zetu wanaofuga samaki katika ponzi 152 ambazo zipo wapate mbegu za samaki za kutosha na waweze ku-*suply* katika nchi yetu.

Kwa hivyo nasema mipango iliyopo nahakikisha kabisa wananchi wataweza kufaidika katika sekta ya samaki, ombi langu kwa wananchi na hasa nyie waheshimiwa, wananchi wanaharibu sana mazingira yaliyoko baharini. Matokeo yake ni kwamba samaki wengi ambao tungeweza kuwavua katika maji madogo hawapatikani sasa, kwa hivyo hata wavuvi wetu wadogo wadogo

wanaokwenda kuvua sasa hivi hawapati samaki wa kutosha kutokana na uharibifu wa mazingira, naomba hili tusimamie kwa pamoja Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa kwa swali hili natoa nafasi ya upendeleo kwa Mhe. Mwakilishi wa Kojani Mhe. Makame aulize swali la nyongeza.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Spika, na mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nina suali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri.

Mimi swali langu lipo hapa jana tu nilimsikia akieleza kama kile Chuo cha Uvuvi kimefungwa na leo hii anatwambia kama tayari Serikali italeta meli mbili za uvuvi, sasa sijui hawa wavuvi watalaalam watapatikana wapi wa kuja kuendesha meli hizo na kufanya kazi hizo za uvuvi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Jana lilikuwa ni swali la Chuo cha Lumumba mwaka 1977 kilitakiwa kiwe kinatoa mafunzo ya kilimo na nikaeleza kabisa kwamba katika kipindi cha miaka minne walikuwa wakitoa mafunzo hayo ya kilimo lakini bahati mbaya ule utaratibu wa kwamba waingie mpaka vyuo vikuu haukutekelezwa. Anauliza suala la kufundishwa wavuvi, wavuvi wanafundishwa ndani ya vyombo vyenyewe na ndio maana katika meli mbili wanazozinunua hawa ndugu zetu kazi yao moja ni kutoa *training* ya kwenda kuvua, mbali masomo ya darasani lakini na kazi ya kwenda kuvua kwenyewe ni taaluma maalum ambayo sio rahisi kuifanya kienyeji hata kidogo.

Kwa maana taaluma ya uvuvi ya kuvua itapatikana ndani ya meli zitakazonunuliwa kufanya kazi hiyo na ndio kazi kubwa hasa itakayofanywa na Shirika letu katika kuwabadilisha wavuvi wetu kutoka uvuvi wanaovua sasa hivi, kuingia katika uvuvi wa kisasa.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Utaratibu Mhe. Spika.

Mhe. Spika. Hapana Mheshimiwa tuendelee hatuna muda.

Nam. 63

Ujenzi wa Barabara ya Konde – Wete

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali imetumia fedha nyingi kwa ujenzi wa barabara ya kutoka Konde/Wete ambayo hata hivyo muda mfupi tu baada ya kukabidhiwa Serikalini imeshaanza kupasuka katika baadhi ya sehemu kunakosababishwa na kutumiwa na gari zenye uzito mkubwa kama inavyozungumzwa na wengi.

(a) Je, mjenzi wa barabara ana muda gani wa uangalizi wa barabara hii ulio chini ya
dhamana yake na kufanya matengenezo pale inapotokea maharibiko kama hayo kwenye barabara zetu.

(b) Je, barabara zilizojengwa za Konde/Wete na Wete/Gando zinamudu kutumiwa kwa gari zenye uwezo wa kubeba tani ngapi za mizigo bila ya kuleta athari katika barabara hizo.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti gari makubwa zenye uzito zaidi ili kukinga maharibiko katika barabara hizo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mjenzi wa barabara ya Wete - Konde ambae alikua ni kampuni ya *MECCO* alikuwa na muda wa mwaka mmoja wa matengenezo inapotokea maharibiko ulio chini ya dhamana yake ambapo kwa sasa hivi tayari muda huo umemalizika.
Mhe. Spika, ningependa kutoa jibu la ziada kusema kwamba kwa utaratibu tuliokuwa nao sasa hivi Mkandarasi akijenga njia ana dhamana ya kuhakikisha kwamba njia ile inakuwa ina viwango vile vinavyotegemewa na kwamba katika chini ya mwaka mmoja ikitokea matengenezo huwa tunamuwajibisha ende akatengeneze, kwa sababu malipo tunakuwa hatumlipi fedha zote tunaweka asilimia tano kwa mia kwa ajili ya hilo kwamba likitokezea kwa ile njia haikujengwa kwa viwango tulivyovitegemea anawajibika kutengeneza.

Lakini kwa ruhusa Mhe. Spika, nataka niseme tu kwamba, baada ya kuhamia Wizara hii nimewatafuta wataalam nikawauliza kwani hii *warrant* inayotoka mwaka mmoja lazima iwe mwaka mmoja haiwezekani tukapewa *warrant* ya miaka 10, wakasema hilo wanakwenda kulifanyia kazi. Kwa hivyo uko uwezekano mkubwa kwamba mikataba mengine ambayo tutaitoa kwa miaka ijayo

tutawataka hawa wakandarasi watoe *warrant*, yaani wawe na dhamana ya kuhakikisha kwamba njia ile haitoharibika kwa kiwango kikubwa katika kipindi cha miaka 10, hilo tunalifanyia kazi.

(b) Barabara hizo za Wete – Konde na Wete – Gando zinamudu kutumiwa na gari zenye uwezo wa kubeba tani kumi (10) bila kuleta athari katika barabara hizo. Yaani magari yasiyopindukia tani 10, kwa hivyo ukweli wake kwamba likija gari zaidi ya tani 10 linakuwa linasababisha uchakavu huo mkubwa kwa njia. Na likiwa chini ya tani 10 huwa halileti athari yoyote katika barabara hizo.

(c) Kuna mpango wa Serikali kudhibiti gari kubwa hasa hizo zilizopindukia tani 10 kutumia njia hili ili kukinga maharibiko katika barabara ni kwamba serikali inakwenda sambamba na teknolojia ya kisasa ambayo inaangalia magari ambayo yanatumia *axle* zaidi ya moja ambazo hupunguza uzito wa magari yale kitaalamu. Maana yake hapo ufafanuzi ni kwamba magari makubwa ambayo yana *axle* moja yakiwa uzito wake ni sawa sawa na gari la *axle* mbili, huwa lila gari la *axle* mbili linapotumia ile njia linakuwa uzito wake unapungua wanavyotwambia wataalam.

Kwa hivyo tunatafanya kila mpango kwa magari yaliyokuwa mazito, yale ambayo yameshakuwa *registered* yataendelea kutumika. Lakini yale ambayo hayajawa *registered* wakileta magari yanayopindukia tani 10 au yakiwa tani10 na *axle* moja tutakuwa hatujaya-*registered* hatutaki watumie hizo njia kwa sababu watakuwa wanaleta uchakavu. Kwa hali hiyo wizara imejipanga vizuri na kuhakikisha kwamba magari makubwa yanayotumika katika barabara zetu ni yale yanayotumia *axle* zaidi ya moja, ambazo tayari hapa Zanzibar gari kama hizo zinatumika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana, Mhe. Spika kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali la nyongeza lakini pia nachukua fursa hii kumpongeza Waziri, kwa jibu lake zuri ambalo sikutegemea kama angenipa hilo jibu.

(a) Lakini pamoja na majibu haya nataka nijue kwa kuwa barabara ya Konde – Wete eneo la kuanzia Mbuyuni, Kinyasini, Bungala, Mgogoni meli sita na Konde vilima vitatu barabara hizo zimeanza kupasuka na kuonyesha nyufa kubwa, jambo lililopelekea kwamba Wizara ya Mawasiliano kitengo cha barabara kuanza kuziziba nyufa hizo zilizoanza kujitokeza na kuwa barabara hizo sasa zimeshabonyea,

nilitaka nijue ni sababu gani zilizopelekea kupasuka kwa barabara na kubonyea.

(b) Kwa kuwa umechukua hatua za kudhibiti haya magari yanayotumia *double axle*, kwa yale magari ambayo kwa sasa yanabeba uzito ambayo hayana zile *double axle* mnachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hayabebi mzigo mzito ambayo yanasababisha kuziharibu barabara zetu.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, la kwanza nikusema kwamba sababu zinazosababisha njia iharibike iwe haipitiki ni chakavu, kwa hiyo njia aliyoizungumzia Mhe. Mwakilishi ni njia ambayo ilijengwa zamani. Na ilijengwa kwa viwango vya zamani, kwa hivyo inaonesha wazi kwamba kutumika kwa njia hiyo kwa magari yaliyokuwa makubwa kumesababisha uchakavu huo, na hivi karibuni kwa sababu za mvua za masika kumetokea pia uharibifu wa njia nyengine, nyengine mpya tumejenga juzi, lakini imetokea bahati mbaya kutokana na mvua kunyesha kwa wingi tumepata matatizo hayo.

Nimekwenda Pemba kukagua na Mhe. Rais, mwenyewe amekwenda Pemba kukagua, hadi njia zilivyo ninachoweza kumhakikishia Mhe. Mwakilishi ni kwamba baada ya muda si mrefu, tutakwenda tena na wataalamu wetu kwenda kuangalia njia zote zilizopata athari kutokana na mvua hizi, halafu tutatngeza mpango kabambe wa kwenda kuzitengeneza hizi njia, kwanza tukazitengeneza kwa muda mfupi na baadae tutakuja na mpango wa kuzitengeneza kwa muda mrefu. Nafikiri Mhe. Spika, nitakuwa nimekidhi swali lililoulizwa na Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja lina kitoto (a) na (b) kama ifuatavyo:

Pamoja na majibu ya Mhe. Waziri lakini nataka nimuulize kwamba:

(a) Serikali imetenga kiasi gani cha fedha *retention money* ili kulinda kifungu cha *guarantee* kwenye mkataba husika kwa ajili ya kukidhi, matengenezo yatakayotokea.

(b) Kama pesa hizo zipo zinatumikaje kwa kurekebisha uharibifu huo wa barabara zetu za Wete – Gando.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwanza kulikuwa na swali aliuliza Mhe. Mwakilishi wa Konde nimesahau kumjibu kwa hivyo, nitakujibu suala lako ulilouliza kuhusu magari yaliyokuwa tani kumi, yenye *axle* moja na *axle* mbili, ninafikiri nilijieza wazi kwamba yale magari ambayo tayari yameshakuwa *registered* itabidi yatumie hizo njia, lakini tutajitahidi kwamba yakija magari mengine yaliyokuwa na *axle* moja na mazito, hatutowapa *registration*. Pili suala lako tulitaka kuchukua hatua gani kuhakisha kwamba haya magari hayachukui uzito mkubwa, hatuna hatua yoyote tunayochukua, lakini nakushukuru kunikubusha kwamba hilo linawezekana, nitakwenda kuzungumza na wataalamu wangu, tuangalie namna ya kuweza scale zile za kupimia uzito wa magari na kusimamia ili kupunguza uchakavu wa hizi njia. *(Makofi)*

Swali lililoulizwa na Mhe. Mwakilishi, kuhusu kiasi tunatenga katika kusimamia hizi njia kwa kweli katika Mikataba yote, tuliyokuwa tunatiliana saini na hawa Wakandarasi tulikuwa tunakubaliana kwamba kutakuwa na asilimia tano, za fedha ambazo zinatumika kujenga zile njia, zinawekwa katika akaunti kwa muda wa mwaka mmoja, katika kipindi kile kama inatokezea tatizo lolote, basi tunatumia hizo fedha kwenda kufanya matengenezo ambayo yanategemea kufanywa. Naamini Mhe. Spika, litakuwa nimekidhi maswali.

Mhe. Spika: Naomba tuendelee maana muda unaenda vibaya sana. Mhe. Omar Seif Abeid kwa suala linalofuata la wizara hii hii.

Nam. 7

Ujenzi wa Barabara ya Wete – Chake Chake

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa kwenye programu ya matumizi ya ujenzi wa barabara 2015/2016 kwa matumizi ya fedha za ndani, serikali ilikadiria na kujipangia kutumia jumla ya Tshs. 1,000,000,000/- kwa ujenzi wa barabara kongwe inayotoka Wete – Chake Chake yenye urefu wa kilomita 22.1. Na kwa kuwa barabara hiyo ni ya muda mrefu toka ilipojengwa na imekuwa mbovu kiasi ambacho ni usumbufu mkubwa kwa wakaazi wa Bahanasa, Piki, Ziwani, Mchanga wa Kwale na Mavungwa kwa sababu madereva wengi wa gari za abiria hawataki kupitisha gari zao kwa sababu ya ubovu wa barabara hiyo.

(a) Je, ni kwa sababu gani hadi sasa Serikali imeshindwa kuanza matengenezo ya ujenzi wa barabara hiyo.

(b) Je, kwa sasa gharama za ujenzi wa barabara hiyo zitalingana na zile zilizotengwa katika Bajeti ya mwaka 2015/2016.

(c) Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa fidia wananchi ili kupisha ujenzi na kutoa muda kwa wananchi walio kandokando ya barabara kuhama kabla ya ujenzi kuanza.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, swali alilouliza Mhe. Mwakilishi kwa sababu gani hadi sasa Serikali imeshindwa kuanza matengenezo ya ujenzi wa barabara, nataka nimuhakikishie Mwakilishi kwamba Serikali haikushindwa, Serikali imo katika matayarisho ya kuweza kufanya hiyo kazi na.

(a) Mradi wa ujenzi wa barabara hii ambao unafadhiliwa kwa pamoja kati ya *BADEA, SAUDI FUND* na Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ). Katika ufadhili huo BADEA tayari imeshatiliana saini mkataba na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu mwaka 2012. Na hatua zinazochukuliwa hivi sasa ni kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka SAUDI FUND na mazungumzo ya kupatikana fedha hizo yanaendelea. Nnachokusudia kusema hapa Mhe. Spika, ni kwamba hatukushindwa kuifanya hiyo kazi lakini tunasumbiri nyenzo, na tunasubiri fedha hizo, za *Co Finance* fedha za ziada kutoka SAUDI FUND na nimeambia hivi karibuni hizi fedha ziko njiani. Kwa hivyo hiyo kazi itafanyika.

(b) Mhe. Spika, kuhusu kulingana kwa gharama za sasa na zile zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2015/16 ni kwamba Wizara inazifanyia tathmini gharama hizo ili zilingane na uhalisia wa ujenzi wa barabara hiyo, Mhe. Spika, sote tunaelewa hapa kwamba shilingi yetu, huwa inachuka thamani ukilinganisha na fedha za nje. Kwa hivyo, kuna uwezekano kabisa, kwamba njia ambayo ilikuwa ijengwe miaka mitatu iliyopita ikibidi ijengwe leo gharama zitaongezeka, lakini hilo limo katika makubaliano ya hawa wafadhili kwamba watatupa fedha za kutosha kwa kuifanya kazi hiyo kwa hivyo nakuhakikishia Mhe. kwamba hiyo kazi itafanyika.

(c) Kwa upande wa tatu kwa swali la Mhe. kwa upande wa fidia, Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wale wote wanaotegemewa kuathirika katika ujenzi huo. Aidha, Wizara imo katika matayarisho ya kuwaorodhesha watu wote watakaoathirika wakati wa ujenzi wa barabara hiyo.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya kutia moyo ya Mhe. Waziri lakini nina swali kidogo nataka kumuuliza.

Kwa kuwa barabara hiyo imeshachukua na mazungumzo haya yameshachukua muda mrefu tokea 2012, na bado kazi haijaanza, mimi nilitaka nijue je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuikarabati ili barabara wakati tunasubiri, yale mazungumzo na zile fedha zikamilike, na inautaratibu gani wa kuikarabati ili wale wananchi, wa maeneo yale tuliyoyataja ya kuanzia Mavungwa, Bahanasa, Mchanga wa Kwale, Ziwani, Kisiwani kwa Binti Abeid na mengineyo, wapate huduma hii ya barabara. Kwa sababu kama swali langu la msingi nilivyozungumza kwamba wenye gari za abiria hawataki kupita kutokana na lile kwamba barabara ni mbovu.

Lakini (b) kwa kuwa Serikali mmeshatenga fedha, na imani yangu mimi na imani ya Wazanzibari wote kwa Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar, kwamba tutajenga ile barabara na ndio ilivyo je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka sasa wa kuwalipa fidia wale wananchi na kuondoa pale ili ukifika ule ujenzi wa barabara ile wawe wameshaondoka kupisha lile eneo je, huu sio muda muafaka, Serikali inalichukuliaje na inalionaje.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, nafikiri masuala ya nyongeza yote nimekwisha yajibu.

Na nitaanza la hilo la mwisho la kuhusu fidia Serikali imekwisha tenga fedha za kulipa fidia na nakubaliana na ushauri wako, kwamba madamu kazi itafanyika basi tuendelee tu kuwalipa watu fidia kabla kazi haijaanza hilo ni jambo ambalo tunaweza kwenda kulifikiria.

La pili la kusema kwamba kuna maeneo ya hizo njia, twende tukatengeneze hilo ni suala la uamuzi, Waziri huyu kaamua kwamba afadhali tusubiri tujenge njia upya, kuliko kwenda tukatumia fedha nyingi sana kwenda kufanya, wenyewe wanaita *patchwork* tukazibe mitundu pale halafu baadae uje uifumbue tena njia yote uje tuijenge tena, kwa ushauri wangu mimi ulikuwa bora tuijenge hiyo njia upya.

Hilo suala la kwamba kuna watu wenye magari wanaoshughulikia usafirishaji hawataki kuendesha magari hayo katika maeneo hayo, hilo litakwenda kuliangalia kwa sababu sisi tunatoa leseni kuwapa watu leseni waendeshe magari hayo, kutoa huduma za usafirishaji, na ikiwa hawataki kufanya hivyo na tumehakikisha kwamba kweli hizo njia hazipitiki hapa tutakaa tutafute suluhu, lakini tukija tukiona kwamba hizo njia zinapitika na leseni tumewapa watoe huduma za usafirishaji na hawataki kutoa huduma hizo basi watakapokuja kuja ku-*renew* leseni zao tutawambia na hizo leseni hatukupeni. *(Makofi)*

Maana hamfanyi huduma iliyotakiwa mfanye, lakini hilo nitakwenda kuzungumza na watu wangu wanaohusika wakazifuatilie hizo njia zilivyo, kama kweli kuna maeneo yaliyokuwa hayana masafa marefu, ambayo hali yake ni mbaya sana, haya tunaweza tukayatengeneza kwa haraka ili magari yanayotoa huduma ya usafirishaji yaweze kutumia hizo njia.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana, Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya naomba kumuuliza suala dogo la nyongeza. Mhe. Waziri katika wizara yako kuna mkataba ambao kwamba umeandikwa kwa lugha ya Kiarabu unaohusika na kutengeneza barabara hii, lakini hadi leo nadhani umekosekana mkalimani wa kutafsiri mkataba ule je, mkalimalini huyo ameshapatika, na kama ameshapatikana ni sababu gani iliyosababisha kwamba barabara hiyo kuchelewa kutengenezwa.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ningependa kujibu swali hili kwa kueleza kwamba katika muda uliopita ni kweli, kulikuwa wakati tulipata matatizo ya kutafsiri ule mkataba kwa sababu uliandikwa kiarabu, lakini tumeweza kufuzu kumpata mtu wa kuweza kutafsiri kwa hivyo hivi sasa hivi, kutafsiri kwa ule mkataba sio tatizo tena. Tunasubiri sasa hivi makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na SAUDI FUND ili tupate hizo fedha tuanze kazi kwa hivyo, suala la Makataba kuandikwa kiarabu kweli kuna wakati ilikuwa ni tatizo lakini sasa hivi sio tatizo tena. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana, Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimpongeza kwa dhati Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri kwa utulivu kabisa naamini sote tumemfahamu jinsi anavyotuelimisha. (*Makofi)*

Suala langu lipo hapa, kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, azma yake kuu katika nchi hii kuiweka katika muelekeo mzuri wa usafirishaji kwa njia ya baharini na nchi kavu, na piganio lake kubwa ujenzi mkuu wa barabara katika barabara zetu zote moja wapo ikawa ya Mwanakwerekwe – Fuoni, nampongeza sasa Mhe. Rais lakini tatizo la pili Mhe. nataka kuuliza kama ifuatavyo:-

Mhe. ujenzi wa barabara unategemea viwango vya ubora, na kwa kuwa katika Serikali yetu kupitia UUB katika Wizara yako Mhe. ina wataalamu wazuri sana kwa sababu ishajenga barabara nyingi nzuri na zimedumu hadi leo. Je, kwa kuwa fedha nyingi zinatumika na barabara kwa muda mfupi baadhi yao huo zinapasuka, kama hizo za MECCO huko Pemba, hivyo UUB huoni ni vyema wakatumiwa kupitia baada ya ujenzi ule wakaonesha ule ubora hasa tukizingatia kwamba Mhe. Rais Magufuli, alipokuwa Waziri wa Miundo mbinu anazikataa kata kata barabara hii siitaki, kuwa haina vigezo, na wewe utachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba inapojengwa barabara kuhakikisha viwango, kupitia wataalamu wako ili kunusuru fedha zetu.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika suala la viwango ni suala muhimu sana kwetu hasa pale tunapotaka kujenga njia, ambayo tunataka tuhakikishe kwamba ile njia inajengwa kwa viwango vile ambavyo tumevipanga. Lakini Mhe. Mwakilishi alitaka kujua jambo moja kwamba katika kujenga njia tunatumia fedha nyingi sana. Katika tarehe 31 mwezi huu, nitakapokuja na Bajeti ya Wizara yetu mtaona kiwango cha fedha ambacho tunakiomba, kwamba ni fedha nyingi sana, na hizo fedha zinategemea sasa unapotaka kujenga ile njia yako unataka ujenge njia ya aina gani. Maana unaweza ukajenga njia kama zile za NewYork Marekani, lakini utatoa bilioni tatu kwa kilo mita moja, na ukajenga njia hizi za *third world*, tukubaliane kwamba sisi na wenzetu viwango vyetu tofauti, ingawaje tunapenda tu tuwe na njia hizo nzuri kama wenzetu maana tunaendelea na sisi.

Lakini nitakuja kukwambia kwamba bili yako badala ya billioni moja na milioni mia mbili utoe bilioni tatu na milioni mia moja kwa kilo mita moja utaamua mwenyewe, au ukiniachia mimi niamue basi nitakuja kukwambia kwamba wataalamu wanasema tupunguze vile viwango vinavyohitajika. Hapo naweza kukuhakikishia kwamba tulifanya makosa huko tunakotoka, kwamba tulikuwa katika kupunguza matumizi, tulikuwa tunataka tuone hiyo njia imejengwa watu walikuwa wanasahau, kwamba zikinyesha mvua maji yatakuja hapa, kuna uwezekano wa mafuriko kuna uwezekano wa madaraja kuharibika. Wengine walikuwa wanapiga hesabu zile wanaona bilioni moja na laki mbili

kwenda kuongeza mitaro, bahati mbaya wengine walisema kwamba aa hiyo tusubiri hizo mvua zenyewe kwani siku ngapi kwa mwaka si siku nane tu.

Unajua kuna watu wengine nao katika kufanya maamuzi yao huwa wanafanya maamuzi ya kuangalia uwezo, kwa hivyo kwenye hilo Mheshimiwa tatizo kubwa ni fedha. Hivi sasa tunapozungumza hapa kuna tenda tumeshatoa, tumepata wakandarasi kumi na nne, katika hawa wakandarasi mmoja anasema ataifanya hiyo kazi kwa bilioni sitini na tisa mwengine anasema kwa bilioni moja mia moja na kumi, mmoja anasema ataifanya kazi hiyo kwa shilingi sitini tisa bilioni mwengine mia moja na kumi. Mimi nikawaita wale nikawambia wewe kwa nini unataka kutozwa pesa zote hizi akasema Waziri, ni hiyari yako katika viwango na nakuhakikishia huyo anaekwambia ataijenga njia ile kwa sitini na tisa bilioni hawezi, mwite hapa nije nimsute. Kwa hivyo suala hili nimeona nitoe maelezo ya ziada kwa sababu kuna kazi ngumu ya kusimamia mambo ya viwango.

La mwisho kwamba tunapompa Mkandarasi kujenga njia huwa pia tunampa mkataba *consultant* yaani kampuni nyengine kabisa ilikuwa haina uhusiano na mkandarasi. Hawa ni wataalamu tunampa mkataba yule aende kule iwe kila siku wakati njia inajengwa anakwenda kuangalia kwamba vile viwango vinakamilishwa.

Lakini dunia imechafuka na hii ni lazima nikwambieni, mkandarasi anakwenda kuripua ripua anavuruga kazi akija huyo mtaalamu (*consulter*) akisema looh! Wewe huwezi kulipwa kwa kazi mbovu kama hii, anamwambia njoo nyumbani usiku tutayamaliza. Hayo pia tunayafuatilia kwa ukaribu sana na la kufanya ni kuhakikisha huyo *consultant* tunayempata awe kweli ni kampuni ambayo ina uwezo huo na kuhakikisha kwamba si watu ambao wanaoweza kupenyezewa bahasha pembeni huko wakatuchafulia kazi yetu.

Nimeona nilijibu hili kwa urefu sana ili uridhike kwamba hiyo kazi ya kusimamia viwango tunaifanya tena kwa mtizamo wa kwamba hatutaki njia zetu ziwe njia mbovu mbovu. Ndiyo maana pale nilipokuwa najibu swali la kwanza nikasema hivi sasa mikataba yote ni kwamba mkandarasi ana dhamana ya njia mwaka huu mmoja lakini wataalamu wangu nimewambia wakafanye utaratibu wa uwezekano kamba tukijenga njia tuwe tunampa mkandarasi dhamana ya kuhakikisha kwamba njia ile ipo katika hali nzuri na viwango vizuri kwa muda wa miaka kumi. Wamenambia hilo linawezekana na linafanyiwa kazi. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante maswali yamekwisha. Nina matangazo kidogo, tangazo lilopo ni tangazo la wageni ambao ni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi kutoka Skuli ya Sekondari Kombeni, jumla yao ni wanafunzi 32 wanaongozwa na walimu wao 2, wakwanza ni mwalimu Shaib Shaib, Suleiman Waziri na mwalimu Mafunda Khamis Hamad, wate kwa pamoja walimu na wanafunzi naomba mnyanyuke. *(Makofi)*

Ahsanteni sana karibuni sana Baraza la Wawakilishi, karibuni mjifunze kwa sababu baadaye baadhi yenu mtakuwemo humu kwa ajili ya kuendesha shughuli hizi. Ahsanteni sana kaeni. Kuna mmoja sikumtaja ni Ndugu Kheri Shaaban Makwaya, kiongozi wa serikali ya skuli hiyo. Ahsante.

HOZA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana Wanawake na Watoto. Kwanza kabisa niwapongeze Wizara na utendaji wake wote katika Wizara hii kwa kazi ngumu ambayo wanaifanya pia niwape pole.

Mhe. Spika, nije moja kwa moja katika hotuba ya Mhe. Waziri katika programu ya uwezeshaji Kiuchumi. Programu hii mimi sina tatizo nayo. Mhe. Waziri ameomba Baraza liidhinishe jumla ya shilingi milioni 232,486,000/- kwa vile programu hii ina lengo la kuinua hali ya wananchi kiuchumi wakiwemo wanawake. Mimi sina tatizo na hili ikiwa mipango yake itakamilika na itafanyika vizuri.

Mhe. Spika, nije katika programu ndogo ya mapambano dhidi ya udhalilishaji Wanawake na Watoto katika ukurasa wa 17. Mhe. Waziri ametwambia kuwa katika utekelezaji wake anaomba Baraza liidhinishe shilingi milioni hamsini na tano na laki moja. Hizi ni kidogo sana. Kwa nini nasema kidogo, kwa sababu kuna mambo mengi katika programu hii yanatakiwa yafanyiwe kazi.

Kwanza kabisa nianze katika programu ambayo wameisema ina mabaraza haya ya Watoto. Wamesema katika *bullet* ya 1,2,3

- Imetoa mafunzo kwa watoto wa Mabaraza ya watoto Wilaya ya Kusini Unguja na skuli 17.
- Wametengeneza miongozo ya Baraza ya watoto hao,
- Imeratibu mikutano miwili ya Kamati ya Mawaziri,
- Imetoa mafunzo ya Viongozi wa Dini kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, wasiwasi wangu upo hapa, hii programu tunayoiyandaa ya Bajeti ina lengo la kuleta matokeo. Wasiwasi wangu katika haya mafunzo Waziri aje anambie waliyoyatoa *impact* yake ikoje. Tulianzisha Mabaraza ya Watoto, wenyeviti na wanaoshughulikia yale masuala ni watoto ambao hawana ajira, wala hawana kile kitu ambacho kinaweza kikawaongezea fedha pale ili kukamilisha ile mipango ambayo wanaiandaa. Mhe. Waziri ndiyo maana nikasema kifungu hichi ni kidogo lazima kama kimeandaa watoto na wana lengo zuri tu katika kuwasilisha yale mambo ya udhalilishaji au kutoa taarifa kwao basi wawezeshe watoto hawa katika kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhe. Spika, watoto wamejipanga na juzi tu tumezindua mpango kazi wa watoto hawa. Ukiangalia watoto hawa wameandaa mpango kazi lakini hawana kile kitendea kazi. Namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie hili na watendaji wake kuhusiana na masuala mazima ya hawa watoto ambao wamewaandaa katika mabaraza haya katika Shehia tofauti tofauti kama walivyoziainisha katika hotuba hii.

Mhe. Spika, jengine nilitaka kujua tayari wametoa mafunzo kwa watoto hawa na shehia tofauti tofauti lakini bado suala la udhalilishaji lipo. Nataka Waziri aje atwambie labda katika hizi shehia ambazo wametoa mafunzo na kuna haya mabaraza ni shehia ngapi zimenufaika na manufaa pengine kwa asilimia ngapi ule udhalilishaji umepungua ndio faida tunayoitaka kwa sababu tunazingatia bajeti hii na matokeo. Kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja ni idadi gani iliyofikiwa kumepunguwa au ule udhalilishaji umezidi katika hizi shehia ambazo zilizotajwa kuundwa kwa haya mabaraza ya watoto.

Mhe. Spika, Mabaraza ya Vijana Mhe. Abdalla Diwani jana alilisemea sana na mimi sitaki niende huko kwa sababu tayari limeshasemewa kuwa bado hayajaanza kufanya kazi vizuri na hili pia walibebe. Nije katika programu hiyo hiyo Mhe. Waziri wamesema kuwa haya mapambano ya udhalilishaji kiambatanisho namba 6 wametoa ile takwimu ambayo inaonesha yale waliyoyafanya kwa kipindi hicho. Bado namuomba Mhe. Waziri waangalie tena kwa kina ijapokuwa labda hizi ndizo zilizoripotiwa katika Wizara yao. Hii ni Wizara ya Wanawake wamo humo, Vijana wamo, Wazee wote wamo, lakini namuomba sana sisi wanawake tunajidai sana katika wizara hii, awaangalie na

watendaji wake waende *field* hasa waone kuna nini hii takwimu iliyotolewa hapa ni kidogo. Hata kama ndio waliyoletewa lakini ni kidogo.

Mhe. Spika, kuna kiambanisho cha Nam. 9 ametoa nauli ya watu wawili kuhusiana na zile kesi ambazo wanapelekewa wao. Mheshimiwa ndio maana nikasema kifungu hichi ni kidogo waangalie. Mhe. Waziri namuomba aangalie kuna kesi ziko Mahakamani za udhalilishaji na wahusika wakubwa wa kesi hizi ni wanawake kwa sababu haya masuala ya udhalilishaji yanakuja kutokana ile aliyoizungumza katika hotuba yake kuna ule utelekezaji na mara nyingi wanaotelekezwa ni akina mama au wanawake, ndiyo zinatokezea kesi hizi tofauti tofauti.

Mhe. Spika, pia kuna kesi hizi ambazo zipo Mahakamani wanashindwa kutoa ushahidi kutokana na sababu mbali mbali. Nilikuwa namuomba tu Mhe. Waziri na watendaji wake wazifatilie wale walioshindwa na hasa wanawake ni sababu gani zilizowafanya kushindwa. Mimi nahisi sababu moja wapo ni kuhusiana na suala zima na ile la kucheleweshwa kwa kesi au kupangiwa siku hadi siku. Mama wale wengine wanakaa vijijini kila siku kuja mjini, kurudi leo anauza kuku, kesho atauza kitumbua nauli inamwishia matokeo yake anashindwa kufika kule na kesi inafutwa kwa sababu tu ya kukosa ushahidi. Namuomba kama hii wizara hashughulike na hili waone tunawasaidiaje akina mama wanaopatwa na kadhia hii.

Mhe. Spika, nije kwenye suala zima la programu hii hii kuhusiana na Sheria ya Mtoto namba. 6 ambayo Wizara hii iliunda sheria hii. Lakini wasiwasi wangu upo hapa namuomba Mhe. Waziri sheria hii ya mtoto na ...

Mhe. Spika: Waheshimiwa kuna mtu ana simu humu ndani ipo karibu na *microphone* zinazofanya kazi zinatupa usumbufu kidogo.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Sheria hii namba 6 Mhe. Spika, inamlinda yule mtoto ambaye amefanya kosa ndiyo inayomlinda. Nimeona katika maelezo kuna karibu watoto 56 wamerekebishwa tabia za watoto wanaopinzana na sheria katika kituo cha kurekebisha tabia kilichopo Madema kuwarejesha katika jamii siyo baya. Lakini hapa katika sheria hii naona ina mapungufu kwa kiasi fulani. Mtoto hapa anahesabika kuanzia siku moja anayozaliwa mpaka miaka 17, kuingia miaka 18 tayari ameshakuwa mkubwa. Lakini mtoto huyu katika umri wa miaka 17 anaweza kafanya kitendo cha udhalilishaji kwa mtoto mwenye umri wa miaka 6. Mtoto huyu wa miaka 6 sheria hii inampa mtoto aliyetenda kosa alipe faini kwa yule mtoto aliyetendewa kosa. Lakini haijaonesha sheria hii, kama yule mtoto

aliyetendewa kosa anafanywa nini? Kwa sababu tayari na yeye ameshapata matatizo na ameshaharibika kisaikolojia. Lakini huyu aliyefanya kosa anawekewa mazingira ya kurekebishwa tabia atafanya vitu vizuri, lakini je, huyu akishakulipwa fidia tu imetosha.

Mhe. Waziri haijatosha na huyu pia kama kuna sheria itengenezwe na yeye huyu mtoto ambaye ameathirika na lile jambo wawekewe sehemu maalum na wao ili (a) waone lile jambo ni baya kulifanya, lakini pia yale mawazo yake yaondoke kule kuliko kulipwa fidia na kurudi nyumbani au kwa kutoa ushahidi mwengine. Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri na hili aliangalie.

Mhe. Spika, lakini pia katika kitabu chao cha bajeti wameandika kuna changamoto zilizokuwepo kwa sheria zinazotoa mianya ya kuwepo kwa vitendo vya udhalilisha na utatuzi wake katika buku lao wamesema kufanyiwa marekebisho ya sheria ambazo zinatoa mianya. Mhe. Waziri tunakuomba sana utakapokuja hapa utueleze ni hatua gani ambazo mmezichukua kama Wizara ambazo mnaona kuna changamoto ya sheria hizi ili zibadilishwe ziwe zinafanya kazi kwa vizuri na zile zilizopitwa na wakati ziondoke. Pia uje utwambie labda mikakati gani mmepanga, au taratibu gani ambazo mmezifanya ili sheria hizi ziondoke na changamoto mlizokuwa nazo. Kwa sababu kwenye changamoto na mmesema kutakuwa na utatuzi wake, lakini huo utatuzi ukoje ndiyo nataka uje utwambie hapa ili tuone kadhia hii inaondoka.

Mhe. Spika, sina mengi ya kuchangia nilikuwa nina hayo, kwaniaba ya wananchi wa jimbo la Chukwani naunga mkono hoja hii kwa asilimia 99 mpaka atakapokuja Mhe. Waziri kunipa majibu ya yale ambayo nimeyauliza hapa. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa. Sasa namwita Mhe. Wanu Hafidh Ameir, atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi kusema machache katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya kukutana hapa. Pia nimshukuru kwa kunipa pumzi ya kusimama kwa mara ya kwanza katika kipindi hichi cha bajeti na kuchangia katika hotuba hizi ambazo zimekuwa zinawasilishwa.

Mhe. Spika, kwanza kabla sijaanza naomba nitangaze nia yangu kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (7)(c) na (d) inayotaka kwamba Mjumbe ambaye ana nia ya

kuzuia fungu basi atangaze kabisa wakati anajadili hotuba ile ya Baraza, naomba niseme kinywa wazi nina nia ya kuzuia fungu ili kuona kwamba hii hoja ambayo ninaijenga basi inapatiwa utatuzi.

Mhe. Spika, kwanza niseme niko *very much disappointed* na wizara hii na sio kwa utendaji wao. Nafahamu kwamba wanafanya vizuri katika mambo mengine lakini kuna hili suala la udhalilishaji ambalo linawatia doa sana. Nasema kwamba nipo *disappointed* kwa sababu Waziri ni Mwanamke, Naibu Waziri ni Mwanamke, Katibu ni mwanamke, wakurugenzi wengi wa wizara hii ni wanawake. Mhe. Rais akaona haijatosha akaongeza mshauri wa mambo ya wanawake ambaye pia ni mwanamke na ni Waziri mzoefu kabisa katika Wizara hii. Kwa hivyo ni lazima niseme kwamba nipo *disappointed* .

Mhe. Mwenyekiti, sababu yangu ni kwamba kwanza niunge mkono hoja ya Kamati ya Wizara hii ambayo imesema kwamba programu ndogo ya mapambano dhidi ya udhalilishaji wa Wanawake na Watoto imetengewa jumla ya shilingi hamsini na tano milioni na laki moja katika mwaka wa fedha 2017/18. Hata hivyo Kamati haijaridhika na utengwaji wa fedha hizi. *Argument* yangu katika hoja hii ina *base* sana na *supporter* ambayo Kamati wameitoa katika hotuba yao.

Mhe. Spika, hapa nina buku la mwaka jana, lakini pia nina buku la mwaka huu nina kitabu cha mwaka jana na nina kitabu cha mwaka huu. Ukiangalia katika takwimu zao mwaka 2016/2017 kifungu hichi kilitengewa milioni mia tatu na kumi na moja wakati ukiangalia viashiria vya kesi vilikuwa kwenye idadi ya 40 kwa makadirio yao, lakini *I am very sure* idadi hii imepindukia mara tatu hata mara kumi zaidi.

Mhe. Spika, kwa kuthibitisha hilo, mimi nadhani wameona hata aibu kuleta takwimu kamili ya hizi kesi. Ukiangalia kitabu chao cha mwaka huu takwimu za mkono kwa mkono hazijaingizwa ambazo hizo ndio zile za mwanzo kabla hazijafika polisi kabla hazijafika Mahakamani zile takwimu za mwanzo hawakuziingiza. Nathubutu kusema kwamba wenyewe wameona aibu kuleta hizi takwimu. Ukiangalia buku la mwaka huu viashiria vya kesi ambavyo wameweka ni 50 yaani mwaka 2017/18, fedha zilizotengewa milioni 55 wakati mwaka jana viashiria vilikuwa 40 fedha milioni 13, sasa hivi 50 na nina uhakika na zaidi lakini fedha zilizotengewa ni milioni 55.

Mhe. Spika, kuna mambo yanaweza kusubiri, lakini kesi za udhalilishaji wa watoto hatuwezi kusubiri *(Makofi)*

Nimeangalia katika kiambatanisho namba 12 kuna fungu la Utawaala na Uendeshaji bilioni moja mia sita na thamanini na tano (1,685,000,000) katika fungu hili kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa wanapandisha ghorofa nadhani jengo lao lile.

Mhe. Spika, jengo litasubiri lakini tupeleke fedha katika fungu la udhalilishaji ili hizi kesi sasa ziwe mwisho. Mimi nashangaa Serikali inakuja hapa inasema Rais anachukizwa sisi tunachukizwa halafu fungu la kwenda kutatua haya matatizo unaweka milioni hamsini na tano (55,000,000) *seriously*, milioni hamsini tano (55,000,000) hata paa la nyumba humalizi tena kwa mwaka hii bajeti ambayo imewekwa kwa mwaka. Sasa nimeangalia hiyo milioni hamsini na tano (55,000,000) wanaenda kufanya nini? Nimeona kwamba kuna Kamati ya Kitaifa ambayo imeundwa ndiyo wanaenda kutekeleza ule mpango wa ile Kamati ya Kitaifa. Mimi namumba Mhe. Waziri aniletee hiyo *breakdown* ya huo mpango uliopangwa lakini na pesa milioni hamsini na tano (55,000,000) watakavyozitumia ili nione hiyo miujiza watakayoifanya mpaka hizi kesi zikamalizika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi naomba na Mwenyekiti wa Kamati nikianza na yeye aniunge mkono kwa sababu kwenye kamati yake ameeleza fedha ni kidogo. Naomba tumege fedha kwenye fungu la Uendeshaji sijui na Utawala zitoke ziingie kwenye fungu la Vitendo vya Udhalilishaji na wala Mhe. Waziri asije hapa akanijibu oh, kuna fedha za wafadhili zitakuja. Ndio maana kumbe hili tatizo halishi kwa kutegemea fedha za wafadhili kwa sababu niliwauliza wajumbe wa kamati wakanambia hivyo ndivyo walivyojibiwa kwamba kuna fedha nyengine kutoka *source* za nje zitakuja.

Sasa wewe una njaa toka nje kalime usisubiri uletewe chakula katika meza ule. Naiomba sana na wajumbe wenzangu waniunge mkono tutoe fungu katika fungu la Utawala na Uendeshaji liende katika vifungu vya udhalilishaji na nimkumbushe tu Mhe. Waziri kwamba Sheria namba 6 ya Mtoto Kesi za Udhalilishaji, Maafisa Ustawi wa Jamii ndio wanaofatilia. Sasa tumekuwa tukipokea malalamiko sana kwamba Maafisa hawa wa Ustawi wa Jamii wanashindwa kwenda kufuata ushahidi kwa sababu wanafika mahala wanambiwa pesa za mafuta kwenda kufatilia ushahidi Nungwi, Makunduchi, Kidoti sijui na wapi hawana. Afisa Ustawi wa Jamii anaenda mara moja, mara ya pili anaambiwa hamna fedha kwa hiyo analala tena vespa haina mafuta analala ushahidi haufatiliwi kesi inachelewa kila siku wazee wanapigwa danadana. Tumechoka, tumechoka na ninataka kuona wajumbe wenzangu wanasema kiukweli kwamba wamechoka, tunaomba fungu la Uendeshaji likatwe liende katika fungu la Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto.

Lakini kitu chengine hapa mnasema mko *serious* Serikali toka mwaka jana tunaimba sheria ziletwe, toka mwaka jana leteni sheria zenye mapungufu, leteni sheria hamjaleta. Sheria ya adhabu mpaka leo haijaletwa tangu mwaka jana tunaimba sheria zenye mapungufu Sheria ya Mtoto yenyewe ina mapungufu leteni marekebisho hamjaleta. Sasa kama wizara hai-*initiate* hizi *changing* za sheria hawa wengine Wizara ya Katiba na Sheria na wao watakaa kitako kwa sababu nadhani na wao wanahisi kwamba *you don't see* ile *important* ya hizi sheria kubadilika ili kuona haya mambo.

Kesi za udhalilishaji kama Serikali na Wizara zote zinazohusika kama hamtokuwa na *good will* ya kumaliza hizi kesi hazitoisha na *good will* haionekani kwa sababu hata hili fungu la kushughulikia hizi kesi eti unatenga milioni hamsini na tano.....

Mhe. Spika: Mhe. Wanu una dakika kumi bado zimebaki za kuongea naomba sasa nichukuwe nafasi hii kumpisha Mwenyekiti Mwanaasha halafu baadae utaendelea Mhe. Wanu na baada ya Mhe. Wanu atafatia Mhe. Hassan Diaspora.

Mhe. Mwenyekiti karibu sana.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha *alikalia kiti)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili kuendelea kama nilivyokuwa nasema kwamba Serikali lazima ioneshe *some seriousness* kwenye hili tatizo kwa sababu limeshakuwa kubwa watu hawana imani tena na Serikali wameanza kupigwa, juzi tu kipindi cha nyuma tumeanza kutumiwa *clips* watu wanaobaka wanapigwa, Pemba kapigwa, mwengine Unguja sijui pale *garden* kapigwa, kwa sababu watu wamekuwa wanakosa imani na ushughulikiaji wa haya mambo na wanawake sasa wamechoka kuona haya mambo yanaendelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na mengi ya kusema lakini najua Mhe. Waziri atakuja kujibu na naomba ni *reserve comment* zangu wakati napitisha mafungu. Tangu mwaka jana wakati nachangia wizara hii nilisema kwamba mimi wizara hii kila ikileta jambo lake nakumbuka kwenye ripoti za Machi nilisema sitochangia chochote nitachangia udhalilishaji na bajeti hii sichangii chochote kwa sababu sioni umuhimu wa kuzungumzia uwezeshaji wa wanawake mnawawezesha nini wakati hawana amani na watoto wao. *(Makofi)*

Unamuwezesha pesa akafanye nini akamtibie mtoto? Shughulikieni suala la Udhalilishaji la Wanawake na Watoto halafu muweze kuwawezesha ili waweze kujiendeleza katika mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kama nilivyosema na *reserve comment* zangu wakati wa kupitisha mafungu na naomba Waziri akija hapa aje vizuri kwanza naomba *breakdown* ya Mpango na hiyo milioni hamsini na tano (55,000,000) watakwenda kuifanya vipi. Lakini pia naomba *breakdown* ya matumizi ya fungu la Utawala na Uendeshaji kwa sababu pia humo humo nimeona mwaka jana kuna malipo wamefanya kwa wafanyakazi mia moja sabini (170) malipo ya malimbikizo ya posho.

Wafanyakazi mia moja sabini (170) wamelipwa wafanyakazi mia (100) wakabaki wafanyakazi sabini (70) mwaka jana bajeti ya mwaka jana, mwaka huu tena wamekuja na malimbikizo ya posho kwa wafanyakazi mia sitini (160) kwa Unguja na hamsini (5) Pemba mnadaiwa na wafanyakazi wangapi, wafanyakazi wangapi wanadai hizi malimbikizo ya posho.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema siungi mkono hoja ya hotuba hii mpaka pale waziri atakapokuja na maelezo yatakayoniwezesha mimi kupitisha hii bajeti ya milioni hamsini na tano (55,000,000) ili wakawezeshe hilo fungu la udhalilishaji. Baada ya kusema hayo Mwenyekiti siungi mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Wanu Hafidh Ameir sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidh akifuatiwa na Mhe. Asha Abdulla Mussa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh : Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika Wizara hii muhimu inashughulikia mambo Wanawake, Watoto, Wazee, Vijana na mambo yote.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi ni mjumbe wa Kamati inayoshughulikia Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Welezo na kuwapa pole wananchi wote wa Zanzibar waliokumbwa na maafa mbali mbali ya mvua iliyosababishwa na Mwenyezi Mungu, lakini kadhalika iliyosababishwa na watu waliojenga katika njia za maji kwa uzembe.

Mhe. Mwenyekiti, pili nampongeza sana Mhe. Waziri anosimamia wizara hii mama Maudline Castico kwa kuisimamia vizuri wizara hii. Lakini tatu nawapongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanya kazi nzuri zinazowawezesha Wanawake, Watoto, Vijana na mambo yote katika kufanya kazi zao za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kuchangia wizara hii kwa kuanzia Ustawi wa Jamii ukurasa wa 20. Mhe. Mwenyekiti ukurasa wa 20 inazungumzia masuala la Ustawi wa jamii katika suala zima la Ustawi wa Jamii, katika suala zima la Ustawi wa Jamii Mhe. Mwenyekiti, kuna Nyumba ya Watoto iliyokuwepo hapo Mombasa, Nyumba ya Wazee ilioko Limbani Pemba, Nyumba ya Wazee iliyoko Sebleni na nyumba ya Wazee ilokuweko katika Jimbo langu la Welezo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu kubwa inakuja katika kuwatizama nichungulia sera inasema ni kuwatunza na kuwahifadhi wazee ili waweze kuishi vizuri wakiwa hapa nchini, Serikali imechukuwa jukumu la kuwatunza na kuwahifadhi wazee wale.

Mhe. Mwenyekiti, kama mjumbe wa kamati nilikuwa nikitembea tulipokuwa tukiwatembelea wazee tuliyakuta mengi, mazuri lakini mengi sana tuliyakuta mabaya ambayo yanatafautiana na Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, yakiwemo wazee wale tulipotembelea wakati ule walikuwa hawapewi chakula kinachorisha kama jinsi Serikali inavyolipa.

Mhe. Mwenyekiti, kama sikosei kwa wakati ule Limbani Pemba kulikuwa na wazee kumi na moja Serikali ilikuwa ikilipa karibu milioni moja na laki nne (1,400,000) Welezo wazee thelathini na nne, Serikali ilikuwa ikilipa karibu milioni tano laki tano (5,500,000) na Sebleni kulikuwa thelathini na moja kwa wakati ule Serikali ilikuwa ikilipa karibu milioni saba na laki tano (7,500,000). Mhe. Mwenyekiti, kwa vile mimi ninakaa karibu sana na nyumba ya Sebleni ya Wazee na Jimbo langu la Welezo huwa natembelea mara kwa mara wiki iliyopita Mhe. Mwenyekiti, nilitembelea tena pale Sebleni na Welezo. Lakini niliyoyapata pale Sebleni yalipendeza sana Mhe. Mwenyekiti, walimpongeza sana sana Mhe. Waziri na Wizara nzima kwa jumla kwa mabadiliko, nitanukuu baadhi ya maneno yalosemwa na wazee huku wakipukutikwa na machozi.

Mzee mmoja alinambia mwanangu si muda mrefu uliopita hapa kama miezi mnne, mitano *wallahi* hatujawahi kula kuku hapa tulikuwa tunakula dagaa, tulikuwa hatutizamwi, tulikuwa mpaka kusema tunaogopa, maana chengine kilichokuwa kinawauma wazee wakiletewa sadaka zinatiwa kunako vipolo

kunako mifuko vyote vinachukuliwa wao wanapewa kipande kimoja cha dagaa msumari wa bati. Lakini wazee wanashukuru sana leo hii kuna Mtendaji mpya pale kaletwa jina lake nimemsahau wanasema wanashukuru anawalea kama wazee wake waliomzaa. *(Makofi)*

Wanasema walikuwa hawajui chipsi kuku lakini leo wanapewa chipsi kuku pale sebleni huyu mtu mpya alokuja, walikuwa hawajui kukaaa nae wakazungumza wanaogopa watendaji lakini huyo ni kama mtoto wao waliomzaa. Wamenipa salamu wamesema ahaa ndiyo Serikali tu lakini Wizara kama itatuhamishia mtu huyu basi siye tutakwenda mpaka kwa Rais, maana yake anatutizama vizuri tunampenda wenyewe kama hatujamuona hapa tushashituka roho.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukiacha hilo Mhe. Mwenyekiti wanalishwa vizuri lakini nina hoja kwa nini Welezo walipwe milioni tano laki tano (5,500,000) na wapewe wenyewe hapana huyu mzabuni, Limbani milioni moja laki nne (1,400,000) wanapewa wenyewe hakuna mzabuni, kwanini Sebleni kuwe na mzabuni mtu wa kati analipwa mzabuni anapelekwa chakula.

Mhe. Mwenyekiti, miye sikubaliani na hilo huyu mzabuni aondoke mzabuni huyu aondoke kwasababu hafanyi vizuri na namuomba Mhe. Waziri na mimi bajeti hii nawekwa mkwala asilimia hamsini (50%) sitoipitisha, kwa sababu mpaka niletewe kopi ya mzabuni huyu, mkataba wa mzabuni huyu niliomba tangu ndani ya kamati nikawa sikupewa nauomba tena kupitia spika yangu sitini na tatu kwa mujibu wa katiba ya nchi hii. *(Makofi)*

Kadhalika naomba kopi ya malipo ya miezi mitatu aliyolipwa mzabuni huyo kwa sababu ukiangalia mahesabu ya maombi ya pesa na mahesabu ya malipo ya mzabuni hayaendi sawa nayaomba kopi ya miezi mitatu aliyolipwa mzabuni huyu ndipo nitapitisha sheria hii. Kwa sababu najua mzabuni huyu alikuwa anadhulumu wazee anapewa pesa nyingi na Serikali lakini chakula anachokipeleka pale sebleni kilikuwa si chakula kizuri anawapelekea anavyotaka yeye pesa nyengine anakula yeye.

Mhe. Waziri, nakuomba sana nitakamata mshahara wako mpaka nihakikishe nimepewa mambo mawili makuu kwanza nipewe mkataba, mbili nipewe kopi tatu za malipo ya mzabuni huyu kwa sababu hafanyi vizuri hali ya kuwa Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar inalipa pesa nzuri katika kuwatizama wazee wale, lakini yeye anajifanya mjanja katika kuwadhulumu na kutowafanyia mambo mazuri wazee wale nitakamata shilingi na mshahara wako.

Mhe. Mwenyekiti namuomba sana Mhe. Waziri atanisamehe kwa hili ni jukumu langu ni kuwatetea wazee wale kwa sababu ndio waliotufikisha hapa, ndio waliofanya mapinduzi ya nchi hii na sisi watoto wao tukawa tunaishi kwa salama na amani katika visiwa hivi vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia namuomba sana Mhe. Waziri pana holi linakodishwa pale namuomba sana Mhe. Waziri lile holi zile pesa zinazopatikana awape pale wawe na *petty cash* ikitokezea tatizo.

Lakini chengine Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri pawe pana gari kuna mzee mmoja jina lake sitaki kumtaja aliumwa usiku pale Sebleni kwasababu hakuna gari, kwa sababu ya kupigiwa Mkurugenzi hapatikani wakati huo aliyekuwa kwa sababu mbali mbali mzee yule aliumwa mpaka kufika asubuhi hali yake ilikuwa mbaya na inasemekana alipopelekwa hospitali kwa sababu ya muda mkubwa alifariki dunia.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana pale panahitajika gari iwepo pale *twenty four hours* kama wazee wale wanapopata *pressure* au mambo mengine aweze kuwahishwa hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hiyo nitaingia katika Baraza la Vijana, Mhe. Mwenyekiti Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama sikosei ilileta sheria ya kuunda Baraza la Vijana naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuunda Baraza la Vijana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nafurahi sana na Wizara Baraza la Vijana baada ya kuwapa *vote* yao ni matumaini yangu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atasimamia vijana wale kwa mujibu wa sheria inavyotaka kwamba wawe vijana wazuri wenye kuleta tija na maendeleo ya Zanzibar. Tulipokuwa tumewatembelea vijana katika sehemu tofauti Mhe. Mwenyekiti, wana malalamiko mengi ambayo hayaleti tija kwa Serikali yetu.

Naomba sana Mhe. Mwenyekiti ahakikishe Mhe. Waziri vijana wale ndiyo mpango mzima, vijana wale ndiyo wajenzi wa Taifa letu lazima kama Serikali kama sheria inavyotaka tuweze kuwalea katika msingi mizuri wawe vijana wanaoleta tija katika maendeleo ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, nitarudi katika Ustawi wa Jamii napenda sana kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuanzisha mfuko wa *pension* wa wazee kwa kuwagaiya shs. 20,000 kila mwezi.

Mhe. Mwenyekiti, nimefanya utafiti wa hali ya juu nimegundua nchi tatu tuu za kiafrika ndizo zinofanya hiyo ikiwemo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hiyo tumpongeze sana Rais wetu wa Zanzibar. Moja Libya, ya pili Botswana inawapa pesa wazee wake na Libya inawapa pesa wazee wake na Zanzibar nchi ya tatu. *(Makofi)*

Kwa hivyo hapa Rais anahitaji kupewa pongezi zote za kuowana na kuweza kuwatunza wazee wetu, lakini Mhe Mwenyekiti, kama mjumbe wa kamati nimefanya utafiti kila uchao tumeyagundua mengi katika mfuko huu wa 20,000 wamo wajanja wasio na kificho wale wazee wote waliotangulia ya haki pesa zao wanazitafuna, kitu ambacho kimelekea mpaka leo Mhe. Rais ana watu wengine kutafuta tunaomba Mhe. CAG aingie kufanya kutafuta mahesabu halisia ya mfuko huu kinacholipwa na kinachobakia.

Na ninajua kulikuwa na ripoti inaandikwa naomba kujua ile Ripoti ya CAG imefikia wapi na ile Ripoti ya CAG inasemaje kwa sababu tuliomba ifanyike Ripoti ya CAG baada ya kujua hapa kuna ubadhirifu fulani unafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, namuombe sana Mhe. Waziri asikae juu ya kiti atembelee dhidi ya mfuko huu, mfuko huu mzuri unalengo la kuwaenzi na kuwalea wazee wetu lakini wapo wajanja wanoutafuna taratibu kwa maslahi yao binafsi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia awe na utaratibu wa kuwabadilisha watu wale wajanja wanaolipa pesa hizi elfu 20,000 za wazee kwani bado wanaposehelea kukaa pale wanaendelea kutafuna na kuunda mipango mbali mbali ya kuendelea kutafuna baadhi ya pesa elfu 20,000 za wazee wetu ambao Serikali yetu ya Mapinduzi inawapa.

Mhe. Mwenyekiti, ukitoka hapo nakwenda kwenye programu ya Mfuko wa Wawezeshaji. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuanzisha mfuko huu wa Programu ya Uwezeshaji najua katika lile lengo la kuondosha na kupambana na umasikini Zanzibar.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, najua Serikali inatumia pesa nyingi sana katika Mfuko wa Uwezeshaji nilikuwa namuomba Mhe. Waziri aje kuniambia kwanza mfuko huu marejesho yake yakoje, na faida yake ikoje, jee watu wangapi wameweze kuondoshewa umasikini na sasa wamekuwa *sustainable* katika kujiendesha wenyewe waliopitia na mfuko huo kwa mwaka wa fedha uliopita 2016/2017.

Wana malengo gani ya kuwakopesha kiasi gani kwa mwaka huu na wana *target* gani ya kuwaondoshea umasikini watu wangapi kwa mwaka wa fedha huu. Au wanawapa tu hizi pesa hakuna *any program*, hakuna *research* ya kuona je, tunafanikiwa au tunafeli; lengo la serikali linafikiwa au tunakwendaje. Naomba kuja kujibiwa suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika ukurasa wa 17 unazungumzia Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Sio siri magazeti ya nje yameandika, redio za ndani ukifungua mawio unasikia mtoto kadhalilishwa. Usiku mmoja nimeshalala nikapigiwa simu na mtu jimboni kwangu haya njoo baba yangu, ana mjukuu wake analea mdogo, mtoto yule mdogo mama namkuta analia namuuliza kitu gani? Mwanangu nimemtuma mafuta ya meli hapo nje tizama alivyofanyiwa, kumtizama yule mtoto basi tulikuwa watu wanne kila mtu aliangua kilio akalia. Mheshimiwa jinsi gani watu wa Zanzibar walivyokuwa wanyama wanawadhalilisha watoto wa miaka minne huu ni unyama.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alipendekeza kitu kwa maoni yake na mtazamo wake na mimi nasema mtu huyu basi sijui tumnyonge Darajani, mana kama kumnyonga tumnyonge Darajani. Niliona Iran Mhe. Mwenyekiti.

Iran niliona watu wananyongwa katika *public place* wanaofanya vitendo vya kishenzi kama hivyo, hata kwenye Uisilamu Mheshimiwa hukumu ya kuuwa imo. Sifikirii mimi Hassan kuna vitendo vya binadamu kama utakwenda kinyume na ubinadamu kama bado utakuwa unahitajika kuishi duniani. Haiwezekani mtu mzima mwenye akili yake akamuingilie mtoto mdogo mwenye miaka minne ni kuvuka kutoka katika ubinadamu kuingia katika unyama.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana wanyama hawa waliokuwa wameshavuka katika vitendo vya kibinadamu hawa si watu wanyama na sisi tusiwaonee huruma, tusiwaonee huruma tuwafanyie vitendo kama tumfunge na gari tumburuze nchi nzima au vipi, lakini lazima tumfanyie vitendo ambavyo na yeye akumbuke ili iwe fundisho kwa mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Muingereza mmoja alisema, "*the only way* kumaliza matatizo ni hukumu kali", *the only way* kumaliza matatizo ni kutoa hukumu kali kwa wale wenye kufanya matatizo. Mheshimiwa tumekuwa tunatoa hukumu kwa kujuana lazima hukumu ya watu hawa iwe kali. Nilikuwa na-*chart* na Mhe. Waziri katika mazungumzo ya kawaida alisema ah, *I wish, I don't want to go further*. Mhe. Mwenyekiti, lazima tutoe hukumu kali.

Sasa kinachonishinda tangu nilipokuwa katika kamati kuona shilingi 55,100,000 nikasema hee, na niliuliza suali hili kweli tumekusudia kupambana na vitendo vya udhalilishaji? Nikaambiwa kuna pesa zinakuja kwa wafadhili, uratibu, mambo mengi nikaambiwa nikahoji sana, lakini nikasema basi kikomo cha kuhoji kwangu kunaishia hapa katika kamati nitakwenda kutumia spika nambari 63 katika kuhoji zaidi ili nipate ufumbuzi wa suala hili. Kwa sababu hili suala lazima tulipatie ufumbuzi, ukimsikia Mhe. Rais analalamika, anasikitika dhidi ya vitendo hivi tutavikomesha lini mpaka kuliundwa timu ya watu kutoka Bara askari kuja kutusaidia dhidi ya udhalilishaji wa vitendo hivi.

Mhe. Mwenyekiti, shilingi 55,100,000 haitoshi hata kidogo wala haifanyi chochote. Mimi Hassan Khamis Hafidh, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Welezo mtetezi wa wakwezi na wakulima waliopindua nchi hii naomba sana kutumia kifungu nambari 98(4)(1) cha kuzuia fungu na mshahara wa waziri mpaka tupate ufumbuzi halisi wa kitu hiki. Na mimi nasema tena nisiambiwe kwamba tutagaiwa na wafadhili Waswahili wamesema "Mtegemea cha ndugu hufa masikini", lazima tuwe na vyanzo vyetu vya mapato, tuwe na pesa zetu wenyewe katika kupambana na wanyama hawa katika kuwakomesha waache kabisa kutudhalilishia watoto wetu na wajukuu wetu ambao ni taifa letu la baadae.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hapa nitazuwia fungu na ninaomba tutoe pesa katika zile huduma tuweke hapa tusitegemee za wafadhili, kama za wafadhili zitakuja baadae tutenge leo tujue tunapambana nao vipi lazima tatizo hili liishe.

Mhe. Mwenyekiti, na kumalia tatizo hili ni kuwa na *pressure* zinazokidhi katika kupambana na suala hili. Mheshimiwa pesa hizi hazifui dafu wala hazifanyi chochote na tusitegemee cha mfadhili, mtegemea cha ndugu hufa masikini. Tunahitaji kutenga pesa zetu si chini ya shilingi milioni mia saba katika kupambana na wanyama hawa mpaka tuwakomeshe na tuwakomeshe hakika.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika Programu ya Kusimamia Sheria...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis Hafidh malizia una dakika tatu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, haya nashukuru. Katika programu ya kusimamia sheria za kazi, ukaguzi wa kazi na kazi zote. Tumeshuhudia idara inafanya kazi nzuri za kuwatafutia ndugu zetu, jamaa na marafiki ajira ndani na nje ya nchi, lakini nitaomba kusema mawili.

Hawa watu wanaokwenda nje ya nchi kufanya kazi naiomba sana wizara iwapangie programu maalum, mpango mzuri kwa mwenye kwenda nje ajulikane anakwenda kufanya kazi wapi. Tumeshuhudia unyanyasaji wa hali ya juu kwa wale watu wanaowachukua huko nje ya nchi mwisho kufikia kuwauwa. Naomba sana wizara iwe na mpango na mkakati maalumu wa kuwajua na kuja kufanya *registration* hapo wanapokwenda.

Jengine katika programu hii kuna inayosimamia kazi za mahoteli, usuluhishaji na mambo mengine. Sitaki kusema sana hapa Mheshimiwa, lakini nasema waziwazi hao wanaosimamia kuhusu kazi za mahoteli na kwengine baadhi yao wanafanya ubadhirifu wanamkandamiza mzalendo na kumtetea mgeni, Mzungu mwenye kusimamia hoteli. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena baadhi yao wanafanya ubadhirifu wa kumtetea mgeni Mzungu na kumtia matatizoni mzalendo kwa sababu anagaiwa dola mia sita au mia tano. Mhe. Mwenyekiti, natumia spika yangu nambari 63 tuanwajua na tunayajua. Leo tunatoa indhari tu Mheshimiwa, naomba sana waziri na wanaofanya kazi hii waisimamie vizuri.

La mwisho katika dakika zangu tatu dakika yangu moja iliyobakia Idara inayosimamia Usalama na Afya Kazini, *Health and Safety*. Mhe. Mwenyekiti, Kampuni ya Bakhresa, Kampuni ya Estim iliyoajiriwa na Bakhresha inafanya kazi pale Mtoni iliuwa, ilipouwa mtu huyu kwa mujibu wa sheria ya serikali ililipwa fidia na serikali, lakini kampuni mpaka leo imekataa kutoa fidia mtu huyo ana kizuka kamuacha, ana watoto watatu, angekuwa mtu huyu kafa nchi ya wenzetu ya nje wale watoto wake na mke wake wangekuwa matajiri na kampuni hii inajua sheria hizi lakini kwa sababu imekuja kwetu hapa umasikini ime-*take advantage* ya umasikini wetu kutudhalilisha kutuulia mtu wetu na kukataa kumlipa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupendekeza tulipokwenda kutembelea katika Mfuko kama huu Bara tuliyakuta mambo mazuri matatu. La kwanza, tulikuta ule Mfuko wa kule unajitegemea ni *authority*, kwa hivyo na mimi ningependa sheria hii tuibadilishe na wetu uwe *authority*. Lakini la pili nilikuta wana Mfuko kwa ajili ya watakaoathirika wanaanzisha Mfuko maalumu kila mfanyakazi anachangia asilimia 1 na anapopata athari yoyote akiwa kaziai ule Mfuko unamtizama yeye na familia yake mpaka mwisho wa uhai wake.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni mambo mazuri ya kuyaiga naomba na sisi tuyaige ili tufanye kazi kwa vizuri na usalama tunapokutwa na maafa tuwe na wa

kututetea isiwe maafa yametukuta na maafa mengine ya umasikini yatukute unakufa siku zako zikiwa bado.

Mhe. Mwenyekiti, naona taa yako umewasha naomba nikushukuru sana, niwashukuru wananchi wa Welezo, niwashukuru wakwezi na wakulima, niwashukuru wana Mapinduzi wa nchi hii niwashukuru na watu wote, lakini naunga mkono hoja wizara hii asilimia 50 mpaka nipewe *copy* ya mkataba, nipewe *copy* ya malipo ya miezi mitatu na nipewe maelezo ya kina pesa hizi ziko wapi, zitapatikana wapi za kupambana na udhalilishaji wa wanawake na watoto wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis kwa mchango wako, sasa namwita Mhe. Asha Abdalla Mussa wa jimbo la Kiwengwa akifuatiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa wa Kiwani na Mhe. Panya Ali Abdalla ajitayarishe.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia machache katika wizara hii ya wanawake na watoto. Kwanza kabisa niwapongeze sana wizara hii kwa kazi ambazo wanazifanya, lakini pia niwapongeze sana tena sana manaibu makatibu wakuu wa wizara hii kwa kazi ambayo wanaifanya kwa kuhakikisha kwamba wizara hii inatekeleza wajibu wao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba niungane na wenzangu waliotangulia kwamba wizara hii inatugusa sana sisi wanawake, lakini mimi niende moja kwa moja kwenye michango. Katika wizara hii ya wanawake na watoto kuna idara ambayo uwezeshaji wananchi kiuchumi. Programu hii ambako kuna Mfuko wa uwezeshaji, katika kitabu chake Mhe. Waziri aliposoma ametwambia kwamba, kwa mwaka 2016/2017 kuna pesa ambazo shilingi 600 milioni zilitengwa kwa ajili ya mikopo kwa wananchi na wametoa mikopo kwa ajili ya wananchi wa Unguja na Pemba. Lakini ukiangalia kwa kina utakuta kwamba katika mwaka 2016/2017 katika programu hii nzima zilitengwa shilingi 527,540,000; cha kushangaza huku kwenye hotuba yao wametwambia wametoa mikopo yenye thamani ya shilingi 600 milioni, waje watueleze toka mwaka 2016/17 tulipopitisha bajeti idadi halisi ya fedha zilizoombwa ambazo zilitolewa shilingi ngapi zilitolewa lakini pia zimetumika vipi.

Vile vile nilitaka kujua kwamba kuna bodi ambayo imeanzishwa, Mhe Rais ameanzisha bodi ya kuhusiana a Mfuko huu wa Uwezeshaji Wananchi. Mhe. Waziri atakapokuja hapa nataka kujua atueleze kwamba toka imeanzishwa bodi

hii wamekaa vikao vingapi na ni sababu gani ambazo zimesababisha kwamba vikao hivi visiwekwe.

Mhe. Mwenyekiti, pia nije kwenye Programu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendeshaji Wanawake, ambapo kuna programu ya mapambano dhidi ya huu udhalilishaji wanawake na watoto. Mhe. Wanu Hafidh amesema tupunguze vifungu kwenye utawala na uendeshaji ili kuhakikisha kwamba fungu hili lililotengewa shilingi 55,100,000 ni ndogo na mimi naungana mkono na Mhe. Wanu Hafidh. Kwa sababu gani, sababu zangu za msingi kwamba matukio yaliyoripotiwa wao wametwambia ni matukio 173, lakini mimi nikiwa mmoja wapo nilioleta hoja hapa Barazani ya jinsi ya mfumo wa uendeshaji wa kesi za udhalilishaji bado hoja ninayo lakini takwimu zilionesha kwamba kuna kesi 2,346. Lakini cha kushangaza kwamba tunakuta wizara wanatuletea 173, sijui niseme kwamba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze wamefanya utafiti gani ambao wakaweza kupata idadi hii ambayo wametuletea hapa.

Niseme kwamba kesi hizi ni nyingi na ukiangalia kiambatanisho Nam. 9 wamesema kwamba kati ya kesi hizo 173 kuna kesi za ubakaji 9 tu kwa Zanzibar nzima na ukitizama vizuri kwa upande wa Pemba hakuna kesi hata moja ya mtu aliyebakwa. Hivi kweli Mhe. Mwenyekiti hii ni sawa? Na tunasikia kila siku kukicha watu wamebakwa, watoto wamebakwa wa kike na wakiume, tunaomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe idadi halisi ya kesi zilizoripotiwa mkono kwa mkono katika vituo vyote vya Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kiambatanisho hicho hicho cha Nam. 9 kuna kesi ya kuachishwa masomo ni kesi moja tu, lakini nasema kwamba katika suala hili si kweli. Kwa sababu mimi nikiwa ni shahidi na kama ni mwanamke na nipo Zanzibar katika jimbo langu la Kiwengwa naamini kuna watoto ambao wameachishwa masomo kwa kupewa ujauzito ni wanafunzi, lakini niseme kwamba hizi takwimu zao walizoturipotia hapa zinatokewa wapi. Kama hawafahamu vizuri basi naungana mkono na Mhe. Wanu Hafidh kwamba mimi naliona fungu litoke la uratibu na utawala Pemba shilingi hizo bilioni mbili, laki tisa na thamanini na nne elfu zipunguzwe zipelekwe kwenye idara hii ambayo ya mapambano dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia ili kwamba Mhe. Waziri atakapozipata hizi fedha likiongezwa hili fungu la shilingi 55,100,000 watapata fedha za kwenda kututafutia idadi halisi ya takwimu ili tufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili tukilitizama kwa juu tunaliona ni dogo lakini suala la udhalilishaji hapa Zanzibar limekuwa kubwa sana na linazidi kuongezeka. Mheshimiwa tuache yote wizara pamoja na wizara nyengine zinazohusika na

haya tunaona vipindi mbali mbali kwenye televisheni vinavyohusiana na masuala ya udhalilishaji wanawake na watoto.

Kuna kipindi kimoja ambacho kinaonesha kwamba kinamama wawili wamebeba watoto wao wanatoka kuhangaika kusikila kesi au kufuatilia kesi ambazo wamepeleka Kituo cha Mkono kwa Mkono kupitia Wizara ya Afya, walipokwenda pale wanasema kwamba ameambiwa vile vipimo majibu hayajarudishwa, kutokana na mashine ile iko Muhimbili. Kwa hiyo, tunaomba sana serikali kwamba kuhakikisha kuwa suala hili tunalipatia ufumbuzi japokuwa wanasema kwamba mashine ya *DNA* sio suluhisho lakini sisi wanawake tunasema *DNA* ni suluhisho, likisimamiwa ipasavyo naamini kwamba kesi zitakwenda kama kawaida na hawa watuhumiwa basi watafikishwa pahala panapohusika na kesi hizi zinaweza kupungua.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala zima la Wazee, Ustawi wa Jamii. Mheshimiwa hapo mwanzo nilikuwa Mjumbe wa Kamati hiyo ya Wanawake na Watoto, niligombana sana kupitia suala zima la wazee. Humu wametuletea bajeti yao makadirio ya mwaka jana kupitia Ustawi wa Jamii walikuwa na shilingi 5,000,410,440; lakini kwa mwaka 2017/2018 wameomba shilingi 8,000,942,360.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwanza atupe idadi halisi ya wazee wote ambao wanapokea pencheni hapa Zanzibar. Kwa sababu ya kusema hivyo, Mheshimiwa katika kitabu chake ukurasa wa 20 amesema kwamba wazee wote walioanzia mwanzo kupokea pencheni hiyo walikuwa 24,000 lakini wameongezeka mpaka kufikia 27,000; lakini cha kushangaza kwamba katika ripoti yao wametuorodheshea kwamba kuna wazee 144 wamefariki. Katika kitabu kikubwa cha bajeti wametuandikia kwamba idadi ya wazee waliosajiliwa na kulipwa pencheni ya jamii ni 28,500, lakini katika kitabu hiki hiki hawakueleza ni kiasi gani cha fedha walichokitoa kwa ajili ya kuwapa pencheni wazee hawa.

Pia ukienda kwenye wazee wanaohudumiwa wanaolelewa Sebleni na Welezo na Limbani, pia idadi bado inachanganya. Kwenye kitabu cha hotuba wamesema wapo wazee 73 lakini kwenye kitabu chao cha bajeti kuna wazee 87, tushike wapi Mwenyekiti? Tunataka kujua Mhe. Waziri atakapofika hapa atupe idadi halisi ya wazee wanaohudumiwa waliopo katika nyumba za kulelea wazee.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba wizara hii tunaiheshimu kwa sababu ni ya wanawake, vijana, wazee na watoto. Wanawake wanapokwenda kwenye

mikopo wananyanyasika sana mikopo ile wanayoomba wanapewa mikopo tofauti na walichokiomba. Pia wizara hii wanatwambia kwamba wao wamechukua wajasiria mali kuwapeleka nje kupeleka bidhaa zao, lakini cha kushangaza kwamba huduma ile wanajihudumia wenyewe hawahudumiwi na wizara na wenyewe wanatufata wanasema, mana wanaishi ndani ya majimbo yetu.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze katika mwaka 2016/2017 ni wanawake wangapi waliopelekwa nje kupeleka bidhaa zao, lakini pia ni jumla ya shilingi ngapi ambayo wamewahudumia wao kama wizara kwenda kupeleka bidhaa zao hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache mengine nitapeleka kwa maandishi ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Jimbo la Kiwengwa kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Mussa Foum Mussa akifuatiwa na Mhe. Bi Panya Ali Abdalla na Mhe. Suleiman Makame ajitayarishe.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kupata fursa hii ya kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka nianze kwa shukurani za kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri, Makatibu Wakuu wa wizara hii na watendaji wake wote, kwa mashirikiano yetu kama sisi ni Wajumbe wa kamati na tumeshirikiana kwa hali na mali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo na mimi nianze kidogo kwa sababu sitakuwa na mchango mkubwa mchango wangu sana nimeutumia kwenye kamati. Sasa hapa nitakuwa na maelezo kidogo tu na mimi kutoa maelezo kidogo ambayo yananikereketa kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na Pencheni ya wazee, kwanza na mimi nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Rais amefanya jambo kubwa katika nchi yetu ya kuwajali wazee waliotimia umri wa miaka 70 na hili jambo halichagui halina chama hili kila mzee aliefikia umri wa miaka 70 basi anaayo haki ya kupata pesa hii ya shilingi ishirini elfu kila mwezi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba bado naiomba wizara, bado kuna wazee na mimi hili nalizungumza hasa katika jimbo langu la Kiwani. Bado tunao wazee wamefikia umri wa miaka 70 na zaidi lakini hii pesa bado hawajapata. Kiukweli wakati mwengine unaona huruma ingawaje unaenda unaambiwa hakuna cheti cha kuzaliwa wala hana kitambulisho cha Uzanzibari, unajua mambo ya wazee wetu wa zamani mtu atakamwambia kazaliwa mwaka wa "Batileti" mwaka wa "Kilo" lakini cheti hana. Kwa hivyo, inakuwa ugumu hasa kwa watendaji wetu.

Sasa naiomba wizara namuomba Mhe. Waziri afanye utafiti apite yeye na watendaji wake awaamrishe wapite kwenye Shehia ili kuwajua wazee ambao kuwa wanayo haki ya kupata pencheni hii na mpaka leo bado hawajaipata na wao waendelee kupata haki hii kwa vile na wao wameshafika umri wa kupata haki.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo vile vile nichangie kidogo katika vijana wetu wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi kama Oman, Qatar na nchi nyengine za falme za Kiarabu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze wizara kwa jitihada yake hii wanaowachukuwa vijana wetu wakawapekea huko nje kwa ajili ya kufanya kazi na kupata pato la kuwasaidia katika maisha yao.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba kuna matatizo hata jana kwenye kipindi cha Mawio asubuhi kulikuwa na kijana anaelezea matatizo yaliyowakutia huko na yeye alikuwa ni mwanamke. Sasa sijui kwamba kuna njia mbili kuna njia ya wizara wanayowapeleka kihalali au vile vile kuna njia nyengine za panya. Kwa sababu yeye anasema unapofika kule kwanza wale Mawakala wanakataa kuwapeleka wale vijana wanaoenda kule kwenye Ubalozi wa Watanzania, baadae vile vile kile kima wanachokubaliana huku kwa mfano Riale 70 au Dola 70 kwamba walipwe kule hawalipwi wanapewa kama hivyo Riale 50 au 40.

Sasa yale makubaliano wameshafika kule hawawezi cha kufanya. Kwa hivyo, wanaleta malalamiko na tatu kazi kubwa, kazi wanafanya mpaka saa sita za usiku. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri haya mambo yafatiliwe na sisi kama kamati basi tunaomba tupelekwe huko na sisi tukawaangalie hawa vijana hili suala ni kweli. Namuomba Mhe. Waziri hili suala lifuatiliwe ili tuone kwamba vijana wetu bado wanaendelea kupata maslahi kama vile ambavyo serikali imekusudia kwa vijana hawa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo vile vile niende katika Baraza la Vijana. Kwanza niipongeze serikali kwa nia yake thabiti ya kuanzisha Baraza

la Vijana. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba vijana wetu wa Zanzibar walipolipata suala hili kiukweli walilichangamkia na walilifurahia na kwa kipindi kilichopita lilikuwa ni gumu upande mmoja kwa sababu walikuwa hawa fungu la kuendesha Mabaraza haya. Sasa hili jambo ni zito upande mmoja. Kwa hivyo, mimi kwanza nimefurahi kwamba mara hii kuna fungu walilotengewa vijana wetu ili kujiendeleza katika masuala yao ya kimaendeleo.

Lakini nataka niseme kwamba huko chini kuko hali mbaya kwa sababu chini kuna kila Shehia kuna Baraza la Vijana na ki ukweli hali si nzuri kwa sababu wanafanya mambo yao lakini kile kitu cha kujiendeleza hawana. Sasa namuomba Mhe. Waziri haya mabaraza ya Msingi yalioko kila Shehia kwanza yaangaliwe vizuri kwa sababu tukiwa na mabaraza yako katika hali nzuri chini basi na huku juu mabaraza yetu yatakuwa yanaenda vizuri.

Sasa namuomba Mhe. Waziri kwamba ingawaje katika kitabu kuna Mabaraza hapa yaliyozunguzwa kwenye Shehia 52 tu lakini nadhani hili limeshazungumzwa inawezekana mkono umechupa kidogo. Kwa hivyo, nadhani atakapokuja Mhe. Waziri hii hesabu ataiweka vizuri. Lakini kina Shehia kuna Baraza la Vijana na kila Wilaya lipo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri hii hali uisimamie na mara hii tuna matumaini makubwa kwamba yale malalamiko makubwa ya vijana wetu yatapungua.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo vile vile niligusie tu kidogo kwa sababu wenzangu wameshalizungumza suala la udhalilishaji wanawake na watoto. Hili suala tumekuwa tunalizungumza sana lakini bado lipo na pesa kama sisi kamati tumezunguza kwamba pesa iliyotengwa ni ndogo na ni kweli ni ndogo. Lakini mimi nataka niseme kwamba hili jambo linataka mashirikiano inaweza ikatengwa pesa kubwa sana lakini ikiwa hapana ushirikiano wa utendaji wa kazi ikawa kazi bure kwa sababu wazee wanasema "Mjenzi na Mjengewa".

Sasa wizara itakuwa kama ni mjenzi lakini wananchi wa Zanzibar watakuwa ndio wanaojengewa. Sasa lazima tupate mashirikiano baina ya serikali yaani Wizara na wananchi wa Zanzibar. Kwa sababu haya mambo yanafanyika vijijini na wafanyaji ni jumla ya sisi wananchi. Sasa pale yatakapokuwa wanafanyika ni lazima tushirikiane hapa panahitajika mashirikiano makubwa Wizara ya Afya, Jeshi la Polisi, Mahakama hayo lazima kunata ushirikiano na sisi wananchi kwa sababu wakati mwengine yanayokea mambo wewe kama mwananchi unaambiwa kaa ushahidi hutaki.

Sasa mimi naomba tu kwamba Mhe. Waziri sisi tunasema hii pesa ndogo iliyotengwa. Sasa tunakuomba ili hili jambo liende vizuri na yapungue haya manguniko kwa sababu linatuathiri sisi. Naomba kwamba kitafutwe kipengele chochote ili kupunguzwe kizidishwe hapa ili hili jambo lifanyike vizuri. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nadhani kwa ninavyokufahamu utakapokuja hapa nadhani utawafurahisha Wajumbe ili hii Bajeti ipite ili iwe haina mabuti mengi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii, kwa hivyo huo ndio mchango wangu namuomba tu Mhe. Waziri atakapokuja atoe maelezo ili hii bajeti yake na yeye ipite bila ya kupingwa sana.

Baada ya maelezo hayo mimi naiunga mkono mia juu ya mia kwa niaba ya wananchi wa Kiwani. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukaweza kuweko hapa katika Baraza lako tukufu.

Lakini pia nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe kwa kuweza kunipatia nafasi hii na mimi nikazungumza machache katika wizara hii ambayo inatugusa sana sisi wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru Mhe. Waziri na Naibu Waziri wake na watendaji wao wote wa wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika majukumu yao ya kila siku.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango waangu kwa kuwapongeza wale wote walioanza kuchangia na wakaonesha dhamira ya kuzuia fungu katika sehemu ya udhalilishaji. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja, na kwa nini nawaunga mkono waliosema hivyo, kwa sababu suala kubwa ambalo linatuumiza nyoyo zetu kila siku ni suala zito la udhalilishaji. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, suala la udhalilishaji hata Mhe. Rais yeye mwenyewe alisema "Sasa na iwe basi kuhusu suala hili la udhalilishaji" na sisi Wajumbe tunaitikia kweli na iwe basi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hichi ambacho tunaona kumepagwa milioni 55 kwa sababu ya udhalilishaji, tunahisi bado dhamira ya kuwakomboa watoto wanaodhalilishwa bado haijakuwa rasmi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, na mimi niseme naungana na wenzangu katika suala hili lazima tupunguze fungu ili tuweze kuongeza fungu katika suala zima la udhalilishaji na mafungu yapo yanaonekana. Kuna fungu la Utawala na Uendeshaji. Mhe. Mwenyekiti, fungu tupunguze na ikiwezekana tukipata sehemu nyengine tupunguze ili suala la udhalilishaji liweze kufikia kikomo. (*Makofi*)

Kwa kweli nchi yetu imepata athari kubwa kwa kuona suala hili bado linaendelea na tulikuwa tunajiuliza maswali lakini pengine kwa nini suala hili linakuwa kikwazo lakini kumbe hatujawa rasmi katika utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kujua serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watoto tukijua watoto ni watu wenye kupoteza kumbukumbu wakati wanapohojiwa katika kutoa ushahidi, serikali ina mpango gani wa kuweza kuwarekodi watoto wale pale wanapotoa ushahidi wao ili mara nyengine asije akababaika akaweza kusema maneno mengine ile rikodi ile iweze kuendelea kumsikiliza mtoto yule katika ushahidi wake. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kujua serikali imejipanga vipi juu ya jambo hilo.

Lakini pia nilikuwa nailomba serikali kuhusu suala hili tuweze kuleta sheria ambayo tutaweza kuwaonesha *live* wale wahusika wa kesi hizi ili wale wananchi wanaosikiliza au wanaoangalia waweze kuwaona na vipi wanaweza kupewa adhabu ili jamii ielewe na pengine ilete tahayuri kuhusu jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kujua katika Mkoa wa Kaskazini tumefungua pale Mhe. Rais amefungua Mahakama ya watoto. Kwanza nimpongeze Dr Ali Mohd Shein kwa kutufungulia Mahkama ile lakini nilitaka nimuulize Mhe. Waziri atakapokuja hapa aweze kuniambia tangu kufunguliwa kwa Mahkama ile ni kesi ngapi zilizoripotiwa katika wizara yake kutoka katika Mahkama ile ya pale Mahonda. Lakini kwa kuwa pia wizara inasaidia watoto wale wanaopatwa na kadhia ya udhalilishaji huwa wizara inawasaidia, nilitaka kujua katika Mkoa wangu wa Kaskazini ni watoto wangapi wamesaidiwa ambao walipatikana na kadhia hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika suala zima la Mabaraza ya Vijana. Mhe. Mwenyekiti, Mabaraza ya Vijana tumeyaunda katika Shehia, katika Wilaya hadi Taifa. Lakini katika bajeti hatuoni wapi Mabaraza haya yanapata *support* ya kuweza kuendelea na programu zao ambazo wamejipangia.

Mhe. Mwenyekiti, Mabaraza haya tumeyaunda na yapo kisheria basi nilitaka kujua serikali ina mkakati gani kupitia bajeti hii kuona wanawasaidia vijana wale na sio kuonekana fedha zile kidogo ambazo hazioneshi kama zinaweza kuwasaidia vijana wetu. Serikali imejipanga vipi juu ya hili nilitaka kujua. Lakini ni lini pia serikali itawaingizia vijana fedha za kutosha ili waweze kutimiza malengo ya kuwepo mabaraza yale.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika hili fungu la udhalilishaji ambalo nililizungumza mwanzo pia kuna msongamano wa hizi takwimu. Mwaka jana tunaambiwa kuwa wizara iliomba milioni mia sita, lakini kuna fedha zilizoingizwa ikawa ni milioni mia tatu na kumi na moja lakini ukija katika kitabu hichi cha bajeti kinaonesha fedha zilizokadiriwa ni milioni 461, lakini fedha zilizopatikana ni 451,007 tushike ipi iliyokuwa sahihi. Kitabu hiki kinasema vyengine kitabu kikubwa kinasema vyengine, ipi iliyokuwa sahihi utakapokuja Mhe. Waziri naomba ufafanuzi wa kina.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nataka kujua kuhusu vikundi vya ushirika. Vikundi vya Ushirika kusema kweli pamoja na changamoto walizonazo, lakini vinakabiliwa na tatizo kubwa la masoko. Wazalishaji wanajitahidi katika kuzalisha lakini masoko kwao ni tatizo.

Mimi nataka kujua mheshimiwa wewe ni mwezeshaji unawawezesha lakini nataka kujua unashirikiana vipi na waziri mwenye wizara hii ya masoko ili kuweza kuwatafutia vijana wetu hawa masoko na kuendelea kujikwamua katika suala zima la umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilitaka kujua je, mitaji tunayowapatia inakidhi haja, kwa sababu inaonekana hakuna ufanisi mzuri katika hivi vikundi vyetu. Vikundi vipo vingi lakini ufanisi wake ukifuatilia utakuta sio mzuri, nilitaka kujua vikundi hivi mikopo hii ambayo tunawapatia vipi inakidhi mahitaji au la.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilitaka kujua kuhusu ufuatiliaji wa urejeshwaji wa mikopo hii. Katika vikundi hivi inaonekana vikundi 96 ndio vimepewa vile vikundi, lakini mikopo ile binafsi wameweza kupatiwa watu 243. Mimi nataka kujua hapa ni vigezo gani labda wanavyovitumia hawa watu binafsi wakaweza kupata hii mikopo, na ni kwa nini vikundi ambavyo vimejikusanya kwa pamoja vimeweza kupatiwa mikopo wao wamepata kidogo na wale watu binafsi wameweza kupata wengi. Lakini pia nilitaka kujua urejeshwaji, ni wepi kati ya mtu mmoja mmoja wanaoweza kurejesha mikopo hii kwa haraka na au ni vikundi ndio wanaweza kurejesha mikopo hii kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama ungenisaidia Mhe. Waziri utakapokuja ukaweza kunieleza vijana waliopatiwa mikopo mtu mmoja mmoja katika mkoa wangu kama utakuwa unawaelewa ni vyema ungenitajia ili na mimi nikapata kufuatilia kwa undani suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende katika programu ya kusimamia viwango vya kazi vya kimataifa na majadiliano ya pamoja kazini. Mhe. Waziri, umeeleza katika majukumu yako kwamba umefanya ukaguzi kwa taasisi 240 Unguja 156 na Pemba 84 na taasisi 20 zilipewa *notice* ya muda maalum wa kurekebisha kasoro zilizobainika. Mimi nilitaka kujua huo muda maalum labda ni muda gani kwa sababu tuna tatizo zima la kuona hizi kasoro, kama hazipati kushughulikiwa kwa muda maalum basi tunapoteza ile sifa ya kuwa na utawala bora.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kujua huu muda ambao umepangwa, lakini pia nilitaka kujua hizo taasisi zilizopata kasoro hizo, za serikali ni ngapi na kama za watu binafsi ngapi. Mhe. Mwenyekiti, niseme katika kasoro hizi pia kuna tatizo zima la mikataba ambayo inasababisha kuingia katika matatizo ya migogoro. Sasa nataka kujua katika suala zima la mikataba ndio suala ambalo linaonekana katika hasa taasisi binafsi ni watu wetu wengi wanafanyakazi bila ya kupewa mikataba. Mhe. Waziri hebu utakapokuja tueleze ni kwa kiasi gani wewe umeweza kubaini kasoro hiyo katika wafanyakazi wetu wanaofanyakazi bila ya kupatiwa mikataba hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwa leo hii nilikuwa sina mengi sana lakini nataka kujua pia Mhe Waziri utakapokuja, kitabu chako hiki hakioneshi malengo na utekelezaji wa kazi zako. Nataka pia utujulishe umepanga vipi kutekeleza. Nini malengo yako lakini na nini utekelezaji wake.

Vile vile jana Mhe. Suleiman naomba nimuunge mkono kwa mchango alioutoa kuhusu wanawake na wanavyokumbana na kadhia za kupewa talaka kiholela na kubaki na watoto wengi sasa wa mitaani. Kwa sababu mtoto anapokosa malezi ya baba na mama inakuwa kuna watoto wengi wa mitaani. Nilitaka kujua na leo asubuhi nilisikia Zanzibar inaongoza kwa wimbi kubwa la talaka. Je, ni mikakati gani ambayo mnaipanga kuweza kuwasaidia wale kinamama wenzetu wanaopewa talaka hizi kiholela ili kuweza kuwasaidia ulezi ule wa kuwalea watoto vizuri na wasiwe wanatanga tanga nao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi nasema naunga mkono kwa asilimia 50, lakini asilimia 50 nataka kujua ni vipi tunaweza kukwamuka na suala zima la udhalilishaji. Mhe. Mwenyekiti, nikipata majibu hayo mazuri kwa Mhe. Waziri

basi sina matatizo naunga mkono kwa sababu hii ni bajeti yetu na lengo letu wanawake tuweze kuishi kwa amani na kuwakomboa watoto na wanawake katika suala zima la udhalilishaji. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Bi Panya Ali Abdalla. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali, akifuatiwa na Mhe. Tatu Mohamed Ussi, lakini kuna waheshimiwa wameomba dakika tano baada ya Mhe. Bi Tatu nitampa Mhe. Zulfa Mmaka Omar dakika tano. Ahsante tuendelee.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niende kwenye ukurasa wa 8, hapa wamesema kuhusu masuala ya uwezeshaji wa mikopo. Wamesema kwamba kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wizara kwa kupitia programu ya mfuko wa uwezeshaji, imepanga kutoa mikopo 600 na bajeti hii hii ya mwaka jana 2016/2017 walitoa mikopo hiyo hiyo 600, yenye thamani ya shilingi milioni 600, hakuna kilichoongezeka wala hakuna kilichopungua.

Mhe. Mwenyekiti, pia walitaka tuwaidhinishie kwenye bajeti iliyopita, walisema tuwape jumla ya shilingi milioni 41,230,000 kwa ajili ya kushughulikia programu hii hapa ya masuala ya mikopo. Lakini mara hii wametuambia hapa kwenye kitabu hiki katika ukurasa 8, wametuambia tuwape shilingi milioni 232,486,000. Sasa mimi nataka niulize mikopo hii 600, mara ile mlitaka shilingi milioni 41,230,000, mara hii mnataka shilingi milioni 200 zifanye nini. Kwa sababu utekelezaji ni ule ule na mikopo ni ile ile 600 hakuna kilichoongezeka. Kwa hivyo, hapa mimi ningeomba kidogo waje wanipe jibu vizuri ili niweze kuwaunga mkono kwenye hili, kwa sababu kuna fungu moja kule la udhalilishaji wa kinamama, pesa zilizopo ni kidogo na tukiangalia watoto, kinamama na dada zetu wanadhalilishwa kwa kila leo, kwa sababu mikopo ni hii hii 600 na ukifanya hesabu ya mikopo 600 ni kila mtu mkopo mmoja shilingi milioni moja, kwa watu 600 hivyo hivyo.

Kwa hivyo, mimi naomba hapa shilingi milioni hizi 232, 486,000 za mwaka jana shilingi milioni 41, mimi naona zinatosha zile zile za mwaka jana tulizowaidhinishia kwa sababu mikopo ni ile ile 600.

Mhe. Mwenyekiti, labda wakati mwengine tuseme wizara wanaona kama tunasahau kwenye hivi vitabu wanaona kama tunaviweka chini ya mivungu.

Hatuviweki mivunguni tunavyo na tunavifanyia kazi, kwa sababu tunataka tutizame ule utekelezaji umefikia hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 20. Hapa unasema kuendelea kuwahudumia wazee 64 kwa Unguja na Pemba, Welezo na Sebleni pamoja na Limbani. Mhe. Mwenyekiti, suala hili la wazee ni muhimu sana katika nchi yetu kwa sababu wazee kuenziwa ni jambo la busara sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nithubutu kusema kwamba wazee kule Pemba wamepata nyumba nzuri ya Limbani, tunashukuru na wao wenyewe wanashukuru kwa hilo. Lakini nyumba ile ina uzio wa waya hapana mlinzi pale, sasa na wale wazee waliopo Limbani wapatiwe mlinzi kama wanavyopatiwa mlinzi wazee waliopo Welezo na pale Amani.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 31 ambao unasema kwamba kufanya matengenezo makazi ya wazee Dimbani. Hapa nakubaliana nalo silikatai hilo.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la pencheni za wazee. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa mjumbe kwenye kamati ya wizara hii, lakini kwa bahati nzuri nimetoka kule nimekwenda kwenye kamati nyengine. Lengo ni kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Mussa alisema hapa kwamba kuna wazee ambao wameshafikia umri lakini zile pesa hawapati. Mimi namuunga mkono Mhe. Mussa kwa hilo. Lakini kuna jambo wakati ule wa usajili wa vitambulisho lilifanyika. Wale waliokuwa wakisajili vitambulisho waliwakisia tu umri wale wazee na ndio maana ukaona kuna msongomano mkubwa wa wazee ambao hawapati kuingia kwenye orodha hii ya kupatiwa posho hili, kwa sababu unamkuta mzee anaendea mkongojo lakini anaambiwa ana miaka 20. Mama yangu mimi mzazi eti ana miaka 20 mpaka leo hii, mimi nina miaka 27 yeye ana miaka 20, hata nimekosa *passport* kule *Immigration* kwa sababu ya hilo. Kwa hivyo, niliwaambia watu wa vitambulisho walifanya kosa hilo, kwa sababu wazee hawajui tarehe waliyozaliwa kwa miaka hiyo iliyopita, sio vyema kuwaripulia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala hili hili la mikopo. Kuna sehemu hapa walisema kwamba wanatoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wafanyabiashara wanaouza chakula kwa jumla. Sasa mimi nashangaa unampa mfanyabiashara anayeuza chakula kwa jumla, huyo kusema kweli sio masikini tena, kwa sababu anayeuza chakula kwa jumla mkopo wa shilingi milioni moja utamsaidia nini, huyo apate mkopo wa mamilioni. Mpe yule mjasiriamali mdogo ambaye hatimizi hata shilingi laki 500,000. Lakini leo unampa mkopo anayeuza chakula kwa jumla, sio masikini tena huyo wa kuwezeshwa aende

benki akakope aweze kupata mkopo wa kuendeleza biashara zake. Lakini leo milioni 600 hii apewe yule anayeuza biashara kwa jumla, yule anayeuza biashara ndogo ndogo akoseshwe aah! hiyo itakuwa hatuwatendei haki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la ajira. Walisema hapa kwenye kitabu hiki kuhusu wajasiriamali wadogo waliwapeleka Uganda. Ni kweli hata mimi nilishuhudia, kuna siku moja niliwakuta pale kinamama kutoka Pemba, kina bi Mafunda Mmaka yule mama yake Mhe. Zulfa Mmaka Omar na mama wengine kutoka Kiwani kule walikwenda Uganda kuuza biashara zile. Tena biashara zenyewe Mhe. Mwenyekiti, ni Makombo Alawi yako kule Pemba maandazi hayo yanaitwa Makombo Alawi. Eti mtu anatoka hapa anakwenda Uganda kuuza Kombo Alawi. Hasara kubwa, nauli anayoitoa ni kubwa kuliko ile biashara anayokwenda kuiuza. Walipofika kule Uganda Makombo Alawi yote yameshakatika katika ndani ya polo sijui walimuuzia nani. *(Makofi)*

Sasa kusema kweli Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ipo haja ya kuwaangalia hawa kwamba nyinyi mnakwenda kuuza biashara Uganda, lakini hii biashara yenu mnayokwenda kuuza Uganda je, ina soko huko Uganda, mna soko gani huko Uganda, kwa nini msiuze hapa hapa Zanzibar. Kwa bahati nzuri siku ile ilikuwa pale kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja kulikuwa na maonesho ya biashara, walipokwenda kule wale kinamama wakadhalilika nauli. Wakanipigia saa mbili za usiku nikaenda pale hawana hata nauli ya kuingilia kwenye boti. Sasa leo tunaambiwa kwamba wajasiriamali hapa 26 wamewasafirisha. Mimi nilikwenda nikawashuhudia kwa macho yangu, na Mhe. Mussa huyu hapa shahidi tulikwenda pamoja, wakataka nauli ya kuwasaidia wale kinamama ili kupata ile nauli ya kuingia kwenye boti mpaka kufika Dar es Salaam. Sasa leo unamtoa mtu hapa unampeleka Uganda, iangalie kwanza ile biashara yake anayokwenda kuiuza kule Uganda ina soko gani la kuweza kupata pesa ya kujikimu na kurudi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mjasiriamali, ujasiri ni mtu aliyekuwa haogopi hasara, hilo nalikubali kwa sababu ndio maana ya ujasiri na ndio mjasiriamali. Lakini sasa Uganda sio karibu, unamtoa mtu hapa umpeleke Uganda biashara anayokwendea kule haikidhi haja, hata ile nauli ya kurudia hapati ikabidi sasa wapige tena simu. Mheshimiwa tunakuomba tena utusaidie, nikawaambia aah! mimi nimeshawasaidia, kuwasaidia sasa hivi siwezi tena kuwasaidia kwa sababu tayari nimeshawasaidia mlipokwenda. Kwa hivyo, mimi naitaka hii wizara Mhe. Waziri akija hapa atuambie vizuri kwamba wale watu 26 walisaidiwa vipi, mbona walitulalamikia sisi kutaka misaada. Na ni kweli kwa

sababu walitoka kule Pemba wakafika pale mizigo yao imeshatangulia kwenye meli ya Bakharesa wao wako nje huko wanadhalilika. Nawatafuta watu wa wizara ya uwezeshaji siwaoni pale.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri aje aniambie hapa kwamba hili suala la watu 26 kwenda Uganda kwenda kuuza biashara zao aah! mimi hili kidogo nitakuwa na mashaka nalo, Mhe. Waziri aje anifahamishe vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende pale pale kwenye suala la wazee kuhusu masuala ya chakula…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Makame Ali subiri kidogo. Nimemuona Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naomba watusaidie kuzungumza kidogo kidogo na watamke maneno vizuri, ili tuweze kuyasikia na kuyajibu. Akisema *speed* sana sipati kitu na huku kuna *echo* kidogo nadhani. Tunaomba msaada wao watakapojieleza wajieleze vizuri na kwa utaratibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Mhe. Mjumbe, umeombwa muongozo unatakiwa uzungumze taratibu ili waziri apate asikie aje akupe majawabu yako kwa uhakika na kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nadhani ninalozungumza nina fahamika na wengi humu, labda mama yangu kidogo atakuwa yeye hafahamu, lakini wako wawili pale na kwa bahati nzuri hii wizara ni ya wanawake na watoto na wote ni wanawake, yuko mama Shadya pale na mkwe wangu bi Castico, kwa sababu natarajia pengine awe mkwe wangu nadhani atanifahamu vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la kuwahudumia wazee ukurasa wa 20 kwenye bajeti hii. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokuambia nilikuwa mjumbe wa kamati hii nikisimamia wizara hii. Utaambiwa kwamba wazee kunatoka pesa pale shilingi 800,000 kwa siku. Lakini wazee wale wanapewa mchuzi wa haragwe hata nazi hautiwi nathubutu kusema hivyo. Mkate wa boflo hata siagi hauna, chai wanayopikiwa ni yale maji ya kunguni ile chai nyeusi hata maziwa, yaani chai sisi kule Pemba tunaita chai ya mkandaa ile nyekundu. Mhe. Mwenyekiti, nikisema hivyo labda utaifahamu. Mhe. Mwenyekiti, hata ndizi wazee wale walikuwa hawapewi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niulize hapa kwamba vipi kuhusu wazee katika masuala haya ya chakula pesa inayotengwa ni kubwa na hicho chakula wanachopata kweli ndicho kwa mujibu wa pesa inayotolewa. Kwa sababu sio kama tunatoa pesa hapa wapewe wazee wanakula vijana waliokuwa na nguvu zao. Hili Mhe. Waziri akija anipe jibu kuhusu suala hili la chakula cha wazee, kwa sababu pale mimi naona ni wali mweupe, asubuhi mkate wa boflo maziwa hawayajui wazee wale na kamati ilipokuja siku ile ilisema. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naliomba hili wahakikishe kwamba wazee wanawafanyia vizuri, kama tunavyowafanyia sisi vizuri humu kwenye Baraza ili kupitisha hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niende mbali sana isipokuwa nirudi tena pale pale kwenye ukurasa wa 20 na ukurasa 8 wa mwaka huu. Hapa mimi kidogo anipe ufafanuzi Mhe. Waziri ili kuweza kumuidhinishia shilingi milioni 230,486,000 kwa mujibu wa mikopo atakayoitoa 600. Kwenye mikopo ile ile aliyoitoa mara ile mikopo 600 akatumia milioni 41, mara hii akataka milioni 200, anipe jibu kwa nini akataka hizi, mimi naona hizi hizi zinamtosha 41 milioni na zile nyengine zipelekwe kule.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia 80, asilimia 20 nzima nazibakisha mpaka mama yangu Mhe. Waziri anipe majibu ya kuniridhisha ili kuweza kumuidhinishia pesa hizi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Zulfa Mmaka ambaye ameomba dakika tano zinamtosha, akifuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa pia ameomba dakika tano. Kwanza nitawapa hawa, naomba Mhe. Zulfa uendelee.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa dakika zangu hizo, ikiwezekana zikizidi na dakika mbili hapo nitafurahi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja katika suala la udhalilishaji. Mhe. Waziri suala la udhalilishaji linazidi siku hadi siku, ingawa tunakuja hapa kusema kila siku kulisemea suala la udhalilishaji, lakini bado linazidi na tukiona hapa kwamba kuna pesa nyingi nyingi hapa kidogo zinaingizwa katika suala hili, lakini nikuombe sana Mhe. Waziri wewe mwenyewe uwe tayari zaidi ambavyo uko katika kufuatilia masuala haya.

Mhe. Waziri kinachonisikitisha kimoja suala hili la udhalilishaji mimi hivi juzi nilishawahi kwenda Mahakamani pale kuna mtoto mmoja kabwakwa wa miaka

mitano lakini nikaumia sana kufika pale sikumuona mtendaji wa Wizara yako. Mhe. Waziri abebwae hujikaza wale watu watu wanaendesha kesi zetu hizo za udhalilishaji tulikuwa tunatakiwa na watu wa Wizara hii wawepo pale kwa ajili ya kutoa macho makali, lakini sasa tukisema kwamba watendaji wako wanakaa tu Wizarani na kusubiri kuletewa katika meza zao tutachelewa na hatutofanikiwa. Kwa hivyo nikuombe sana hapo unataka pesa za ufuatiliaji lakini mashaka yangu kwamba watu wako hawafahamu kwamba hizi pesa tunazipitisha kwa nia moja, kwa hivyo nikuombe sana uwaambie pesa hizi tunapitisha lakini na wao waweko tayari kufuatilia mambo haya wasikae tu katika meza zao na kusubiri kupelekewa kesi hizi.

Mheshimiwa nije katika mikopo mimi sitaki niseme sana kwa sababu dakika ni kidogo lakini nilikuwa nakuomba sana uje kuniambia ni vikundi vingapi vya vijana waliowezeshwa katika mikopo hii, pia nataka nijue ni vijana wangapi Unguja na Pemba waliopatiwa mikopo hii nafuu katika Wizara yako.

Nikitoka hapo niende katika Baraza la Vijana tumeona kwamba kuna pesa hapo umeziingiza katika Baraza la Vijana, lakini nikuombe sana pesa hizi ziwafikie walengwa sio pesa hizi zimalizikie pale ofisini, kwa kufanya masuala mengine ambayo hayahusiani na vijana. Tunajua kwamba vijana kuna changamoto nyingi sana katika mabaraza haya na naamini kwamba bajeti hii ni ndogo sana kwa kusaidia mabaraza ya vijana kwa sababu hawana ofisi, wala hawana chochote cha kutendea kazi hawa ndio kwanza wanaanza sasa. Kungekuwa kuna uwezekano ningeomba kwamba bajeti hii izidishwe lakini kwa sasa basi tu naziingizwe hizo hizo, mimi ningekuomba sana hizi pesa wanaingiziwa mabaraza ya vijana ziende katika mabaraza ya vijana na sisi tutakuja hapa kukuhoji pesa hizi zimefika vipi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika suala la wazee, Mheshimiwa Wazee tunawapenda sana na kipindi cha nyuma hapa ulikuja ukasema kwamba wazee wanakula vyakula vizuri, mayai, siagi lakini niseme kwamba wazee wale bado kula yao si nzuri kihivyo. Kwa hivyo nikuombe sana katika bajeti hii uangalie sana sana wazee, wale ni wazee wetu na kila mmoja matarajio yake kufika katika uzee ule. Kwa hivyo nikuombe sana leo unawatengenezea wao huwezi kuamini pengine kesho na keshokutwa kile ambacho umekifanya na wewe unakwenda kufaidika pale. Pia niwaombee wazee hawa Mheshimiwa katika zile nyumba zao hawa wazee hawana TV wale wazee wamekaa kama watoto sasa hivi, wanataka na wao kujiliwaza. Ningekuomba sana katika bajeti hii kila kituo upeleke japo TV moja moja ili na wao waweze kuona mambo yanayofanyika.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo wazee hao hao wana tatizo kwamba wale wazee hawana madaktari kwa hivyo wakati wanapopatwa na matatizo ya homa na kitu chengine wanasumbuka sana, kwa hivivyo nikuombe sana ufanye jitihada zako kwenda katika Wizara ya Afya uwaombee madaktari angalau mmoja mmoja katika nyumba zile ili wazee wale wanapoumwa waweze kutibiwa kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nende katika wajasiriamali, wajasiriamali wana masikitiko juu ya safari ambazo wanazipata zile safari zinatolewa za kwenda kama Uganda na sehemu nyengine lakini Mheshimiwa na sisi tunapata tabu kwa sababu wajasiriamali wale wakisha kupewa safari zile wanakuwa mara nyingi sana wanaomba omba pesa za nauli. Hapa tunawapitishia pesa hizi za nauli na mambo mengine lakini kiukweli pesa hizi hawapewi na safari zile pia wanapokwenda hizo nafasi kuzipata zinatolewa kwa upendeleo Mheshimiwa, Na mara nyingi wanakuwa wanaambiwa tumieni pesa zenu baadae hivi na hivi, wakati wanakuwa wanajua kuwa wengine hawana uwezo wa kutumia pesa zao na wao wanataka kwenda kule kwa ajili ya kwenda kujifunza biashara moja na nyengine. Kwa hivyo ningekuomba sana uwe muwazi katika hao wajasiriamali, jamani tulichonacho ni hichi waende hawa isiambiwe kwamba jitegemeeni halafu wakirudi wengine wananung'unika inakuwa ile jitegemeeni kwa kujificha ili wengine wasiende wengine waende. Pia hizi pesa hapa zimepitishwa kuna watu ambao walikwenda safari wana manung'uniko zile pesa hamkuwapa. Kwa hivyo nikuombe sana Mheshimiwa zile pesa za wajasiriamali tukishazipitisha hapa leo zipo zinapitishwa nikuombe sana wale watu wapewe kwa sababu ni haki yao.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo mbio mbio nataka niende katika masuala hapa ndio kitovu ambacho kimenifanya nisimame Mheshimiwa mashirikiano ni kitu muhimu kwanza nimpongeze Mhe. Rais kwa kuona kwamba hii Wizara ni kubwa wanawake, vijana, wazee na wanaume humo wanahusika, lakini sasa nina masikitiko hii Wizara kiukweli hamna mashirikiano. Leo hapa tunakupitishieni pesa nyingi sana, hizi pesa zinataka mashirikiano kufanya kazi hakuhitaji mtu kuwa na ujuzi zaidi, kuwa na elimu zaidi, ama kuwa na kitu chengine chochote. Kufanya kazi kunataka mashirikiano kwa njia moja au nyengine tushukuru kwamba Wizara hii viongozi wake kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, sijui nani wote ni wanawake, wanawake tunaweza.

Lakini sasa mnatuumiza, mnatuangusha wizara hamna mashirikiano. Mheshimiwa mashirikiano katika Wizara hii kuna kamati zikienda unasikia kwamba aa tumekwenda tumepata Naibu Waziri Waziri hakuwepo, sijui leo tumekwenda kuna Katibu Mkuu nani hakuwepo, Mheshimiwa mnatuangusha

sana wanawake tunaweza na mumeaminiwa. Kwa hivyo nakuombeni sana kutoka Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, watendaji wote mushirikiane hii Wizara ni kubwa, hii Wizara ni nzito, hii Wizara haitaki elimu, hii Wizara haitaki makabrasha, hii Wizara inataka imani za nafsi zenu. Mkiwa na imani na nafsi zenu udhalilishaji utaondoka, ukiwa na imani na hii Wizara naamini kwamba mambo yatakwenda vizuri lakini mkianza kukaa huko pembeni fulani kantendaje, fulani kamfanyaje, hatutoenda na hizi pesa zetu hizi ambazo tunazipitisha naamini kwamba hazitokwenda vizuri.

Kwa hivyo nikuombeni sana sana mashirikiano ni kitu muhimu katika nchi yetu, kwa vile imani mnayo na naamini kwamba mnaipenda nchi yenu nikuombeni sana mulete mashirikiano. Haya mambo sijui yanayopitwa kusemwa sijui hivi na hivi, naamini kwamba mkileta mashirikiano masuala haya yote yataondoka, kama ambavyo leo tunaiona kwamba mashirikiano Wizara hii wanayo, nakuombeeni kwa mungu kwa mashirikiano haya muendelee kuwa nayo.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia, nina suala moja nataka niliulize hii Wizara ya Wanawake na watoto ingawa na wanaume wamo, lakini hii mikopo wanapatiwa wanaume mingi kuliko wanawake, sasa nikuombe tu Mhe. Waziri, ukija kwa sababu pana pesa mimi bila ya kuzipigia buti hapa nataka uje kunieleza ni sababu zipi zinazopelekea kwamba wanaume wakapatiwa mikopo hii kwa wingi kulikoni sisi wanawake ambao tumo katika nembo hii ya Wizara, ukishakunijibu hilo Mheshimiwa hili fungu ambalo nina nia ya kulizuia naamini nitalipitisha kwa moyo mkunjufu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono asilimia thamanini ishirini nimezuia kwa sababu hizi ambazo nimezitaja zimenikasirisha na naomba Wajumbe wenzangu waichangie kwa nguvu ili waweze kufanikiwa ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka mwakilishi wa Vijana kutoka Pemba sasa naomba nimuite Mhe. Miraji nae ameniomba dakika tano akitoka Mhe. Miraji nitampa Mhe. Tatu Mohamed Ussi na kuna Waheshimiwa wawili wameomba dakika tano kama muda utaruhusu nitawaruhusu Mhe. Miraji karibu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache tu kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, mimi nitajitahidi kama alivyosema nizungumze taratibu kwa sababu hii hoja yangu ninayotaka kuizungumza aifahamu vizuri. Lakini moja kwa moja niende katika program hii ambayo

inawagusa vijana, watoto katika suala la udhalilishaji, kwa kweli naomba niungane na wenzangu na mimi niseme kwenye eneo hili Mhe. Waziri na viongozi ambao mnaiongoza Wizara hii hamkuitendea haki. Kuna takwimu ambazo zimo kwenye kitabu kuna Mheshimiwa mmoja alisema 311 lakini si sahihi pia kunako kitabu hichi mmewekwa takwimu za maombi ya fedha za kuidhinisha ni 461, lakini mkatiliwa 451 lakini uratibu wenzangu wameuzungumza mimi sitaki niuzungumze.

Lakini leo fungu hili hili wakati tukiona vitendo vya udhalilishaji vimeongezeka tumekuja na bajeti hii tuwaidhinishieni 55 mnatupeleka mbali kweli kweli na mnatutoa imani kweli kweli ya kuwa mnaweza hasa mkafika pahala mkaturejesha kwenye dhamira ya Serikali, kwenye dhamira ya kiongozi wetu mkuu wa nchi ya kupambana na kuratibu vizuri matendo haya ya udhalilishaji. Kuna mwenzangu mmoja jana alichangia nikawa namsikiliza kwa makini maana alikuwa anasema kwa nini tusiwanyonge hawa, lakini ukisikiliza haki za binaadamu na mambo mengine mimi siendi huko sitaki niende nje ya sheria katika mtazamo huo.

Lakini katika sura ya kawaida eneo hili Mhe. Waziri hatukulitendea haki na mimi siko tayari kupitisha fungu hili likiwa na Shilingi 55 milioni na nitawashangaa sana Waheshimiwa wawakilishi ambao ni wadau wakubwa kwa sababu sisi ndio tunaozaa na sisi ndio walezi, na sisi ndio tunaoongoza jamii tukaipitisha Wizara ina shilingi 55 milioni wakati tulipowapa 451 kwenye kitabu chao takwimu wameon/esha wenyewe haya matatizo yameongezeka, leo tukisema tunawapa 55 si wanakwenda kufuta kabisa kushughulikia matatizo ya udhalilishaji. Maana lazima tuseme ukweli huo ndio muelekeo wao, kwa *percentage wise* haiwezekani kama lazima 55 ndio watatekeleza. Mimi nasema katika kuhaulisha lazima niseme kwenye fungu la uendeshaji na uratibu wa Wizara hapa palitengwa fedha kunako programu moja ya uratibu wa mipango na sera tafiti na Wizara pamoja na kuwa kuna tafiti muhimu na kuna mambo muhimu hapa tuondoe kunako 427 milioni tuwape milioni 227na mia mbili tuzipeleke kwenye fungu hilo la kushughulikia udhalilishaji. Mimi nawaomba sana wenzangu Waziri wa Fedha yupo, mwenyekiti wa kamati ya bajeti hayupo lakini hizi tuhamishe hapa watajua namna gani ya ku-*control* utafiti wao kwa kipindi hichi kigumu lakini fedha hizi mia mbili zielekee hapo.

Lakini eneo la pili la utawala na uendeshaji kuna kifungu cha usimamizi wa rasilimali watu kina bilioni moja milioni mia sita na hapa tuhamishe mia mbili ziwe 455 tutakuwa tumefanya kazi nzuri ya kukiweka kifungu hichi chenye uratibu mzuri katika mambo haya. Nawaomba sana wenzangu kama tunachukia na kukemea vitendo vya udhalilishaji lazima tuvipe nguvu kifedha, lakini

tuvipe nguvu katika kuvisimamia. Mimi naomba wenzangu uratibu huu ni muhimu sana maeneo haya mawili Mhe. Waziri nimeyataja kwa ufasaha na nitayasubiri, tumesema haya tuyahamishe na naomba utukubalie ili bajeti yako iende vizuri vyenginevyo mafungu haya tutamalizana na wewe. Mhe. Waziri eneo hilo la udhalilishaji naomba nielelee kwengine.

Katika eneo la udhalilishaji mimi naomba sana nipate muongozo na mwanasheria Mkuu pia yupo kuna mfungwa mmoja sitaki nimtaje kwa jina, kafungwa miaka mitano mwanamke lakini amejifungua akiwa gerezani gereza letu la Zanzibar yupo na ana mtoto, mtoto hakufungwa kafungwa mama mtu sasa tunataka tujue utaratibu wa kisheria kumpa haki huyu mtoto. Kwa sababu miaka mitano akiwa gerezani maana yake huyu *Nursery* inamkuta akiwa gerezani, sasa tunataka ufafanuzi mzuri kunako kulinda haki za watoto wetu hawa na fursa zao kamili. Maana nasema mama mtu kaenda na mimba hatuna tatizo na makosa yake, lakini mtoto lazima amfuate mama mtu sasa utaratibu gani tunaoutumia kutafuta ile haki ya mtoto katika kunusuru kwenye kadhia hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie maana azma yangu ilikuwa kwenye udhalilishaji, kwenye Mabaraza ya Vijana. Mabaraza ya Vijana kwanza niipongeze azma ya Serikali, nimpongeze Rais wa Zanzibar kwenye eneo hili lakini lazima tukiri mwaka jana hawa vijana hatukuwatengea hata fedha waliyumba sana katika kufanya kazi zao, lakini wamejitahidi sana nimpongeze sana Katibu Mtendaji na timu yake wameyapeleka Mabaraza haya hivyo hivyo katika ugumu wao lakini vijana wamehamasishika wamefanya kazi nzuri ukenda huko ndani ya mawilaya, lakini *support* ya Serikali kupitia Wizara ilikuwa ndogo mno. Leo ukiangalia kitabu hapa wana milioni 427 mwaka jana walikuwa na 0 wanaanzia maana yake kama pilot 427 ni hela ndogo sana. Maana hii tumewabajeti, lakini nina uhakika huko tunakokwenda kwa bajeti hii pia sijui hizi kama tutawapa. Kwa hivyo nawaombeni sana kwa sababu leo tumepunguza mafungu kwenda kule lakini nilikua na azma ya kupunguza fungu angalau tuwapatie milioni 800.

Lakini na tunakokuja Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango naomba unisikilize kwamba mabaraza haya kwa azma yao nzuri na utaratibu wao mzuri na mikwamo wanayoipata tuwatengenezee OC yao na iendeshwe na Katibu Mtendaji mwenyewe, isipitie kwenye mkono mwengine usumbufu mkubwa vijana hawapati kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana tuawasaidie vijana wetu, tusaidie kuratibu azma ya serikali kuanzisha mabaraza haya lakini na mimi nimalizie siungi mkono hoja mpaka nione ile hatua ya Serikali tunakwendaje katika kuhamisha fedha kwa kusaidia fungu lile la eneo la udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa naomba nimuite sasa Mhe. Bitatu Mohammed Ussi akifuatiwa na Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis na kama muda utakuwepo Mhe. Viwe ameniambia anataka dakika tano nitamruhusu. Mhe. Bitatu.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kusimama mchana huu ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake kwa jinsi walivyoandaa hotuba hii hotuba ilikuwa ni nzuri ingawaje ina baadhi ya mapunfugu, lakini muwasilishaji aliwasilisha vizuri kwa ufasaha na sisi tukaifahamu, baada ya shukurani hizo nataka niende kwenye mchango wangu kwenye ukurasa wa 8 programu ya usimamizi na uendeshaji wa vyama vya ushirika.

Mhe. Mwenyekiti tunaishukuru Serikali yetu kwa kutuweka Wizara hii ya Uwezeshaji Vijana Wanawake na Watoto kutuwezesha wananchi wake kwa sehemu mbali mbali ikiwemo kuimarisha vijana na wanawake kuunda vikundi vya ushirika kwa lengo la kujipunguzia umasikini. Mhe. Mwenyekiti wanawake na vijana tunaunda vikundi na vikundi hivi tunaviunda kwa hamu kubwa tunakuwa tunafanya kazi mwanzo wake lakini ikifika wakati vikundi hivi baada ya muda mdogo utakuta vikundi vimeshasambaratika. Mimi nilikuwa naishauri Wizara kabla ya kuunda vikundi au kama kuna kundi ambalo limeshajiweka kutaka kuunda ushirika basi kwanza vikundi vyetu vipewe elimu ya ujasiriamali.

Kwa sababu vikundi vyetu vinakufa kutokana na ukosefu wa elimu ya ujasiriamali ingawaje hapa kwenye kitabu chao hichi Wizara imesema kwamba inatoa mafunzo, lakini mafunzo hayo wanayotoa yanakuwa hayakidhi haja, sasa kama hayakidhi haja vikundi vile inakuwa bado uelewa wao unakuwa ni mdogo. Kwa hivyo naiomba Wizara iwape elimu tena wajasiriamali wetu ili waweze kundeleza vikundi vya ushirika na wajue namna gani ya kujiwekea akiba lakini pia kuweza kurudisha ile fadha ili iweze kuzunguruka kwa wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije ukurasa wa 12 na mimi naungana na wale wenzangu waliozungumzia wale wajasiri amali waliopelekwa Uganda. Mhe.

Mwenyekiti na mimi naungana nao kwa sababu wajasiri amali hawa walipelekwa kule Uganda lakini inaonekana walijitegemea wenyewe kuanzia nauli mpaka walipofika Uganda kwenda na kurudi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hivi leo tumfikirie mjasiri amali mdogo mdogo, tunampeleka Uganda na Wizara bila ya kumsaidia, kweli tuna nia ya kumsaidia mjasiri amali huyu. Mhe. Mwenyekiti wajasiri amali hawa walikwenda Uganda lakini walirudi hawana kitu. Kwa sababu hicho walichokiuza walitumia nauli na kula na bidhaa zao nyengine walirudi nazo, mimi nikiwa shahidi bidhaa hizi nimeziona wamerudi nazo. Lakini pia Mhe. mimi nataka kujua wizara hii baada ya kuwapeleka wajasiri amali hawa Uganda je, tokea waliporudi wamewaita angalau wakawauliza, mlipokwenda Uganda mmefarajika vipi au mlipata hasara gani?

Hili nataka kulijua, kwa sababu ukimpeleka mtoto safari unatakiwa unaporudi umuulize mwanangu umefanikiwa vipi, sasa mimi nataka kujua wizara hii, angalau imewaita wajasiri amali hawa wakawauliza faida na hasara walioyoipata?

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naenda ukurasa wa ishirini saba kifungu cha hichi kinachosema, “kimepokea na kusikiliza kufanyakazi jumla ya malalamiko 173 Unguja na Pemba”. Kutokana na kesi zinazowakabili wananchi zikiwemo tutelekezwa, migogoro ya ndoa na familia kupigwa kudhulumiwa mali zao, kati ya hao 102, ishirini na nane Pemba na sabini na nne Unguja zimeshughulikiwa Lakini Mhe. Mwenyekiti nataka kujua katika hawa vijana wetu wanaotekelezwa, kuna matatizo ya ndoa.

Nataka kujua, kwanza hapa kwa kule upande wa Pemba vijana wetu wanaotelekezwa je, kuna nyumba ambayo inawahifadhi hawa vijana waliotelekezwa, kutokana na familia zao, au hawa vijana hawa tunawaweka sehemu gani hapo nilikuwa nataka kujua kama kuna nyumba au wizara ina mpango gani kuwaekea sehemu ambayo vijana hao waliotelekezwa, ili kuwekwa kwa kujihifadhi na Serikali kuwaangalia. Nataka kujua hilo kwanza, lakini pia katika hapo nende kwenye kesi hizo za udhalilishaji na mimi niungane na wenzangu, kutokana na pesa hizi, pesa hizi zilizowekwa kuhusu mambo ya udhalilishaji.

Hivi Mhe. Mwenyekiti, sisi sote tunapiga kelele hapa Barazani, kesi za udhalilishaji hazendi hazendi, lakini kumbe tunalaumu vyombo wakati pengine vile vitendea kazi havipo, sasa na mimi kutokana na hali hiyo, hizi milioni hamsini na tano zilizowekwa kwa fedha hizi nasema naungana ni ndogo

haitoshi, kwa sababu kesi hizi zinataka kufuatiliwa vijijini nyengine ili zifike Mahakamani. Sasa hapa tutalaumu watendaji kule kumbe chakufuatilia hawana. kwa hiyo mimi naishauri Wizara kutengua fungu lile la Utawala na Uendeshaji fedha hizi ziongezewe kwenye kule kesi za udhalilishaji kwa sababu Mheshimiwa tumechoka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama wazazi tumechoka kuona vitendo hivi kila siku vinaendelea, na tutakuwa tunakaa Barazani tunasema kesi hizi hazendi hazendi, lakini kumbe hazendi kutokana na ukosefu wa fedha. Sasa Mhe. Mwenyekiti na mimi naungana na wenzangu kwamba hizi fedha tutengue fungu ili kesi ziishe na kama kesi haziendi Mahakamani ina maana tunazalisha matatizo mengine, tunalazalisha kesi nyengine. Kwa sababu leo kesi itawekwa pale mfanya makosa anapewa dhamana au anaachiliwa ende kwao, atafanya nini si ataendelea kufanya kitendo kile. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tumechoka tunasema kudhalilishwa kwa sababu ukimdhalilisha mtoto wa kike unamdhalilisha na wazee wake, kwa hivyo watoto wanadhalilika lakini na sisi wazee tunadhalilika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti baada ya hilo nende kwenye pencheni ya wazee ile ya shilingi 20,000 elfu Mhe. Mwenyekiti, wazee wengi wanapiga kelele kutokana hili, lakini tuseme ukweli kuna baadhi ya wazee wetu walikuwa kwa kweli miaka yao hawaijui, na watu wa Ustawi wa Jamii, wenyewe walikuwa wanatumia vigezo kwa sababu kama walivyosema wenzangu, utamuona bibi mtu mzima lakini ukimuuliza amezaliwa mwaka gani haujui anakwambia ana miaka 20. Na kweli wakati tulipoandika vitambulisho vya Uzanzibari watu wengi walikuwa hawajui miaka yao, sasa kutokana na hili Mhe. Mwenyekiti, ndio imesababisha hilo baadhi ya watu hawakujua miaka yao sasa wanalalamika kuwa hawapewi pencheni ya elfu 20,000. Mimi naiomba Wizara labda itafute mbinu na mikakati gani ya kuweza kujua wale ambao wazee wametimia miaka sabiini kamili.

Lakini bila hivyo, Mwenyekiti kelele hizi itakuwa kila siku tunazipiga malalamiko kwa wazee hayeshi, kwa sababu hii ni pesa na penye pesa hapeshi maneno kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimie naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia tisini mpaka Mhe. Waziri anieleze kule Pemba wale watoto wanaotelekezwa, wana mpango gani wa kuwaekea sehemu ya kuwahifadhi.

Mhe. Mwenyekiti baada ya mchango wangu huu naunga mkono asilimia thamanini na ishirini naziweka. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii, na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenye ezi Mungu kwa kunijaalia pumzi, za kuweza kusimama hapa na mie nikaweza kueleza machache katika Hotuba ya Bajeti hii. Mhe. pia nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kuweza kututayarishia Kitabu ambacho leo hii tumekaa hapa kukijadili. Bila ya wao jitihada zao tusingeweza kufanya hichi ambacho tunakifanya wakati huu. Lakini vile vile nimpongeze Mhe. Maryam kwa niaba ya Kamati kwa uwasilishaji wake mwanana na tukaweza kuelewa ili tukapata fursa kubwa ya kuweza kuainisha baada ya Kitabu na maelezo ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu na mimi kama walivyonitangulia wenzangu niliwaunge mkono wale wote, waliochangia juu ya Bajeti ya mwaka 2017/2018, juu ya suala zima la programu ya mapambano juu ya udhalilishaji wa kijinsia, Mhe. Mwenyekiti na mimi naungana na wenzangu, kwa sababu sote tunaelewa kwamba suala la udhalilishaji, linahitaji mikakati maalum ni suala gumu ambalo viongozi sote tunaumiza kichwa juu ya suala hili. Lakini badala ya kuwa twende mbele tunarudi nyuma, lakini Mhe. Mwenyekiti hapo hapo, tulipitisha hoja iliyowasilishwa na Mhe. Asha hoja, ile miongoni mwa maazimio yake ilikuwa ni tuliazimia kwamba Bajeti, programu hii iongezewe kwa mwaka wa fedha huu ambao tunaujadili hapa leo, lakini shakusikitisha maazimio yale inaonesha Wizara tunapotoa maazimio ndani ya Baraza la Wawakilishi hawayatilii maanani, na wanayapuuza. *(Makofi)*

Na laiti kama wangekuwa wanayatilia manani leo hii tusingelizungumza suala hili kwa kiasi ambapo tumelizingumza, nawashauri Wizara, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni chombo ambacho kinatunga Sheria na kutoa maamuzi, na yale maazimio ambayo tunawasilisha humu tunaomba myafanyie kazi vyenginevyo yatatokea haya ambayo yametokea hapa leo. Mhe. Mwenyekiti katika Bajeti ya mwaka 2016-2017 milioni mia tatu kumi na moja zilitengwa kwa programu hii, lakini kama ninavyosema kwa mwaka na wenzangu walivyozungumza wameweka milioni hamsini na tano ukitizama suala la udhalilishaji mikakati yake mikubwa inahitaji, ufuatiliaji wa kutosha.

Lakini vile vile, wakati tukipitia katika Wizara Kamati, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria. Tulikwenda Mahakama ya watoto tukakuta watendaji wa Ustawi wa Jamii, changamoto yao moja wanashindwa kufuatilia

kesi wamekuwa usafiri hawana mafuta watafanyaje kazi. Ili utekeleze majukumu yako vizuri lazima ufuatilie na sikukaa juu ya meza ukasubiri kuletewa taarifa, hatufiki pahala lakini vile vile, kunahitajika ushauri nasaha kwa wale ambao wameathirika kifungu hichi cha fedha tunampa wakati mgumu, tutakapomuekea Bajeti kama hii Mkurugenzi wa Wanawake na Watoto atafanyaje kazi kama hizi, kweli tutafika mbele? Hatufiki. Kwa hiyo kwa vile wenzangu washatangulia na mimi nazuwia au napunguza fungu la Utawala tupeleke katika programu hii ya udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti mengi yamezungumzwa nende katika programu ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji, Mhe. programu hii, ina lengo lake la kutoa mitaji na huduma nyengine za kifedha kwa wananchi wenye kipato kidogo, Mhe. imeelezwa kuwa, watu waliopatiwa mikopo ni mia sita kipindi kilichopita na tulipitisha Bajeti ya milioni ya mia sita, kitabu hichi leo kurasa wa 44 kiambatanisho Nam. 1 inaonesha tofauti ya kile ambacho tulokipitisha na makadirio ambayo yameoneshwa humu, nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa atufafanulie kwa kina na atueleze vizuri ili tumuelewe tofauti hii imetokana na nini, vyenginevyo tutazuia fungu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwawezesha wananchi kiuchumi imeelezwa kwamba kuna mikopo mia tatu na arubaini na moja, imetolewa yenye thamani ya milioni mia sita, lakini vile vile, ikaelezwa asilimia saba ya mikopo hiyo wanufaika ni makundi maalum. Mhe. Mwenyekiti, makundi maalum yanatafsiri pana kuna makundi kuna wazee, makundi maalum vijana, makundi maalum watu wenye ulemavu, makundi maalum wale walioathirika ee sasa mimi nilitaka kwanza aje anifafanulie makundi haya maalum yaliyowekwa hapa ni yepi. *(Makofi)*

Lakini vile vile, akasema haya makundi maalum yaliyoelezwa hapa, kwamba wakiwemo wenye ulemavu. Mhe. Mwenyekiti watu wenye ulemavu wanasikitika kwamba Wizara hii wanapokwenda kutaka huduma wanawambia wana Idara yao, lakini Mhe. Mwenyekiti Idara ya Watu Wenye Ulemavu ipo kwa kuratibu masuala ya watu mwenye ulemavu ambayo iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, huduma za mtu mwenye ulemavu ni sawa sawa na huduma za mtu mwengine. Inakuwaje leo unatoa huduma kwa wanawake, unamwambia mwanamke mwenye ulemavu ende Idara ya Ulemavu huo ni unyanyapaa, inakuwaje unatoa huduma kwa vijana, kijana mwenye ulemavu unamwambia ende Idara ya Ulemavu huo ni unyanyapaa. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha lakini pamoja na hayo Mhe. Waziri atakapokuja hapa ameeleza kuna vikundi viwili, vimepatiwa mikopo na aje anambie ni vikundi gani na viko wapi. *(Makofi)*

Lakini na chengine katika hawa watu arubaini ambao anasema kwamba wamepatiwa mikopo, na watu wenye ulemavu nje wanalalamika hawapati hii mikopo itakuwa ni busara sana, Mhe. Waziri atakapokuja hapa, akatwambia ni wepi hawa watu arubaini wenye ulemavu lakini wapo katika maeneo gani. Mhe. Mwenyekiti, dakika zangu tano, Mhe. Mwenyekiti kwa kweli masuala yanasikitisha, Wizara inajitihada kubwa ya kuhakikisha kwamba inafanya kazi si kama haifanyi kazi Wizara inafanya kazi, inaanzisha vikundi mbali mbali vya vijana, lakini tatizo mnashindwa kuviendeleza mwisho wa siku vikundi hivi vinasambaratika na havijui wapi pa kwenda, pesa nyingi mnatumia gharama kubwa mnatumia, nguvu kubwa mnatumia kwa kuanzisha lakini kwa kuendeleza inakuwa wagumu. Niwaombe Wizara, mchukue jitihada za makusudi kuhakikisha kile tunachokianzisha, zile gharama tunazozitumia mnaziendeleza ili kupata manufaa mazuri kwa vijana wetu na kwa Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima la wajasiri amali, kama walivyotangulia wenzangu wajasiri amali wanalalamika ni kweli kabisa, na Mhe. Mwenyekiti inapotokea maonesho wajasiri amali ndani ya mikoa wanasema kwamba, tumeambiwa na Wanawake na Watoto tukufateni Wabunge na Wawakilishi mtuwezeshe kusafirisha mizigo, nauli pesa ya kujikimu tutoe sisi, leo hii Wizara inasema imewawezesha, itakuwa ni busara sana kupitia kikao hichi Mhe. Waziri akatoa ufafanuzi wa kutosha juu ya hili ili sisi tukaelewa na wale wajasiri amali wakaelewa utaratibu mzima. Kama wizara ina jukumu la kuwalipa basi wataelewa kwamba wizara inatakiwa itulipe, lakini wizara kama haina wajibu wa kuwalipa vile vile, wale wale wataelewa na watajua kwa jinsi gani wajipange na kuondokana na ile omba omba.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naunga mkono hoja kwa asilimia 80 mpaka utakapotolewa ufafanuzi wa kutosha na nikajiridhisha. Ahsante nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana, Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Mwakilishi wa Wanawake Nafasi za Watu Wenye Ulemavu, sasa naomba nimpishe Mhe. Viwe Khamis naye aliomba dakika tano na mwisho kabisa na muda huu atakuwa Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuniona ukaweza kunipatia dakika tano ili niweze kuchangia Hotuba Mhe. Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nimpongeze Afisa Mdhamini wa Wizara hii ambaye kuwa ni kijana mwenzetu, naamini hatutoangusha. Mhe. Mwenyekiti, shukrani za pekee ziende kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua Mama yetu Mhe. Zainab kuwa Mshauri wa Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu na Baraza la Vijana, wenzangu wengi tayari wameshalizungumzia Baraza hili la Vijana, lakini Mhe. nitakuwa mkosefu wa fadhila kama na mimi sikulichangia Baraza hili la Vijana au sikulizungumzia Baraza hili la Vijana. Nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuahidi sisi vijana kuwa tutakuwa na chombo chetu ambacho kuwa kitakuwa ni chombo kinachoweza kuweza kututatulia matatizo yetu sisi vijana. Lakini Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha kabisa Baraza hili la Vijana limeonekana ni Baraza ambalo kuwa halina maana katika Wizara hii, katika ukurasa 27 Mhe. Mwenyekiti, limezungumziwa Baraza hili la Vijana kuwa litaingiziwa milioni 44. Pia linakwenda na ile idara inayoelezea maendeleo ya vijana. Pia Baraza hili litapatiwa ruzuku. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake aje anambie ni kiasi gani hichi watapatiwa ruzuku vijana wetu hawa katika kuliendeleza Baraza hili la Vijana Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa uchaguzi wa Baraza hili la Vijana Taifa kulitokea changamoto kubwa sana katika uchaguzi huu. Chamoto hii ilisababishwa na Kanuni ya uchaguzi ya Baraza hili la Vijana ilikuwa haipo vizuri. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipatie maelezo ya kina ni lini kanuni ile iliyoleta mgogoro wakati wa kipindi cha uchaguzi itarekebishwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa wa 4 kuna ajira za mikataba (ajira za nje) ajira hizi wanakwenda kufanya vijana wetu. Wizara yao ndiyo Wizara inayoshughulikia ajira hizi za vijana wetu. Wengi wameshachangia kuhusiana na ajira hizi za mikataba. Kama nilivyosema mwanzo mimi ni Mwakilishi wa vijana nipo hapa wanawawakilisha vijana. Tunaomba Wizara walishughulikie kwa kina suala hili la ajira za nje kwa vijana wetu, Vijana wetu wanapata matatizo wanapokwenda kufanya kazi katika nchi hizi za Kiarabu, vijana wetu wanabakwa huko huko katika nchi hizi za Kiarabu.

Mhe. Mwenyekiti, wanapofika kule wanakuwa wanachangamoto ya kuchukua paspoti ili vijana wetu ale wasipate kusafiri, wanaona suluhisho kubwa wazuie paspoti za vijana wetu. Wizara walishughulikie suala hili ili zisitokee tena changamoto hizi ambazo zinawakabili vijana wetu hawa.

Nikitoka hapo niende kwenye programu za Mfuko wa Uwezeshaji. Programu hii wenzangu wengi wameshaizungumzia, Programu hii imetoa mikopo 341 Unguja na 232 Pemba na 40 asilimia za watu wenye ulemavu. Niipongeze idara hii ya mikopo inajitahidi kutokana na kuwa vijana wanaohitaji mikopo hii ni wengi pamoja na wanawake lakini hamkututendea haki kama sisi vijana. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake aje atupatie maelezo ni vijana wangapi ambao wamepatiwa pesa hizi za uwezeshaji Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye programu ya mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto. Tumeona malalamiko 173 ambayo ni malalamiko ya vitendo vya udhalilishaji Unguja 128 na Pemba 45. Niseme kuwa tatizo hili la udhalilishaji bado lipo na tatizo hili bado linaendelea na wizara hasa hawajawa tayari katika kulishughulikia tatizo hili. Tunakuwa tukisikia kwenye vipindi vya redio hasa asubuhi wakati wa kipindi cha mawiyo kama unataka ujuwe tatizo hili Zanzibar usikilize kipindi cha habari za Mawiyo. Kipindi hichi kinatoa habari mbali mbali za watoto wetu ambao wanabakwa, wanadhalilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara pamojana Wizara nyengine zinazohusiana na hili suala la udhalilishaji basi washirikiane ili kuhakikisha tatizo hili la udhalilishaji Zanzibar limeondoka. Tatizo hili la udhalilishaji haliwezi likaondoka tu hivi hivi kwa kusema tu kila siku tunakaa kwenye vyombo vya habari tunasema udhalilishaji sasa basi. Ni lazima serikali ichukue hatua kali ili hawa wanaofanya vitendo hivi vya udhalilishaji itakuwa ni fundisho kwao ili wasiweze kurejea vitendo hivi vya udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niseme kama walivyosema wenzangu tupunguze fungu katika Idara ya Utawala na Uendeshaji ili tuweze kuongeza katika sehemu hii ya Ustwi wa Udhalilishaji na Kijinsia kutokana na kuwa pesa hizi milioni 55 pesa hizi hasiwezi zikaweza kutatua matatizo ambayo yapo Zanzibar ya udhalilishaji wa kijinsia watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jiseme naunga mkono asilimia 80 asilimia 20 nitaunga mkono mara baada ya kupatiwa maelezo kuhusiana na udhalilishaji na hizi pesa tukahakikisha kwamba zimehama huku na kuingia hapa. Jengine sitounga mkono mpaka Mhe. Waziri aje anambiye anipe maelezo ni kiasi gani cha ruzuku ambacho kimeandaliwa kwa ajili ya Baraza la Vijana Taifa. Ahsante sana.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima asubuhi hii ya leo. Lakini nikushukuru Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, kwa bahati nzuri kwa bajeti ya mwaka huu leo ndio mara yangu ya kwanza. Kwa hivyo namshukuru Mwenyezi Mungu na kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza naomba nichukue nafasi hii kuwapa pole wananchi wote wa Zanzibar ambao wamepata mafuruko kutokana na mvua kubwa wambazo zinaendelea.

Pili naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za kujenga uchumi wa Zanzibar, lakini pia kuimarisha ustawi wa wananchi kwa kupitia wafanyakazi wa serikali kwa kuongeza mishahara lakini pia kwa kujali makundi maalum yakiwemo ya wazee, wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, muda wenyewe ni mchache kwa hivyo nitazungumza kidogo kidogo kwa sababu nina vifungu kama vinne ambavyo nimekusudia kuvichangia. Nianze na kuhusu na Uwezeshaji wa Wazee au watu wenye umri zaidi ya miaka 70. Hili ni jambo jema sana kama walivyozungumza Waheshimiwa wengine. Hili Rais wetu kaweza kutekeleza ahadi yake kwa asilimia mia. Tunamshukuru na kumpongeza. Ninaloliomba kwa Wizara ni kuhakikisha kwamba wale wote ambao wana haki hii wanaipata, yapo malalamiko kwa baadhi ya maeneo kwamba waliostahiki kuingia katika mfuko huu hawakuingia na waliokuwa hawakustahiki kuingia katika mfumo huu wengine wameingia.

Mimi sitaki kuzuia fungu lolote la Wizara hii na niseme wazi kwamba naiyunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia. Lakini niseme ni wajibu wao kujiridhisha kwamba wale je, waliohusika kwa kupitia Wakuu wa Wilaya na Masheha ndio wanaostahiki kupewa hizo fedha. Maana fedha hizi ni nyingi kwa serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika udhalilishaji wa watoto na akina mama. Kwanza niungane na Waheshimiwa wenzangu wote waliozungumzwa kwamba fungu lililowekwa katika kifungu hiki ni dogo sana kutokana na mazingira ya kazi zake. Mimi niseme kwamba kwa bahati nzuri ukiangalia ratiba ya vikao vyetu bahati mbaya Mwenyekiti wa Kamati ya bajeti simuoni sijui yuko wapi. Tuna siku nne za majumuisho yale yote yaliyozungumzwa katika bajeti kupitia Wizara mbali mbali kabla ya Mhe. Waziri wa Fedha kusema bajeti Kuu ya Serikali. Mimi niombe zile siku nne Kamati yetu ya Bajeti ingelikuwa vyema kama Mwenyekiti wa Kamati hii angekuwa kamuandikia Mwenyekiti wa

Kamati ya Bajeti barua kuhusu fungu hili na mafungu mengine ya Wizara hii kwamba uangaliwe uwezekeno wa kuhaulisha baadhi ya mafungu ya Wizara hii au kuyapunguza. Mfano ukiangalia fungu la Sheria za Kazi na Kazi za Staha kuna karibu bilioni moja nukta hivi hatuwezi tukamega pale kidogo kuziingiza katika fungu hili la wanawake.

Nafikiri mimi niombe Waheshimiwa Wizara hii kwa vyovyote inazihitaji hizi fedha, lakini basi Serikali Kuu ikae iangalie wakati wa kufanya majumuisho na Kamati ya Bajeti hizi fedha wajuwe kuzitengeneza vizuri ili hili fungu liongezeke. Mimi nilitaka maelezo kidogo katika kesi ambazo zimeripotiwa 173 za udhalilishaji mimi naona katika kitabu hichi zimeandikwa zile za matunzo ya watoto na malezi ya watoto siyo zile kesi za kubaka na hizo ndizo tunazozilalamikia sana kwamba ubakaji umekuwa Zanzibar. Sasa sijui Wizara inatwambiaji wana kesi ngapi za kubaka.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Mwantatu, mimi nipo Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, tumekwenda huko tumeona Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya wanalalamika ubakaji umekuwa mkubwa. Wasiseme au wasituletee kwamba kesi za udhalilishaji ni matunzo ya watoto au kesi za malezi. Hii ni sehemu moja ya udhalilishaji lakini kesi za ubakaji je, zinachukuliwa vipi, zinachukuliwa hatua gani na huu ni mkubwa sana Zanzibar. Kuna kipindi walifanya majaribio ya kwenda kuwacheki watoto wa Skuli ya Welezo, ambao wameharibiwa ni wengi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi naomba sana mimi bajeti yako naiyunga mkono lakini uwe na utaratibu wa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Afisi ya Mufti kwa skuli ya vyuo vya Qur-an, kuhakikisha kwamba watoto wetu wanakuwa salama. Yaani sasa hivi unakuwa na watoto wawili akiwa mmoja hayupo humwambie yule mwengine aende chuoni au aende skuli ni lazima wafuatane. Sasa hili ni tatizo Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo mimi namuomba Mhe. Waziri wajipange kwa suala hili kuhakikisha kwamba katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, hilo ndilo nililokusudia kulizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala la kuwawezesha kiuchumi wanawake na Vijana nalo hili Mheshimiwa linakuwa kama ni jambo mtambuka, linazungumzwa kwa upana wake tu lakini uhalisia wenyewe unakuwa kidogo hauko wazi. Sasa mimi naomba tena naomba sana huko mitaani vijana wengi hawana ajira na Mhe. Waziri atakuwa shahidi kwamba vijana wengi hawana ajira, hivi kuwawezesha kwa vikundi na mambo mengine vinasaidia sana kuleta hali ya amani na nchi yetu.

Nimuombe Mhe. Waziri na kwa bahati nzuri tumeona kwamba wanazo fedha au nyengine wamewekeza Benki. Hizi za Benki labda atatueleza kama hizi milioni 800 zimewekwa kule kwa kipindi ambacho anaziweka benki zinazalisha kiasi gani na ile riba inakwenda wapi. Katika baadhi ya taasisi za serikali sasa hivi mtu anaweza kuwa na dhamana ya fedha akaziweka benki baada ya mwaka kama bilioni moja akenda kuchukua ile riba ikawa yake zile fedha za serikali zinabakia pale pale anakuwa kapiga dili kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, tuombe tu kwamba fedha kwa ajili uwekezaji zitumike kwa ajili ya uwekezaji na zisipotee potee tu. Kulikuwa na mfuko hapa tukiuwita JK na AK. Tulikuwa tunauzungumza kupitia Wizara hii, tumeuzungumza mpaka sasa hivi naona hauzungumzwi kabisa labda zile fedha zimerejeshwa zote au msamaha umetoka wa madeni yale. Mimi nilitaka kujua baadaye Waziri anifahamishe kama kuna msamaha wowote kwa wale ambao walikopeshwa. Kwa sababu gani tunazungumza hivyo, zile fedha hazikuwalenga sana wananchi mmoja mmoja, watu waliopewa wale wengi waliokuwa wajanja wajanja na fedha wamezichukua. Wakati mwingi kama walivyozungumza Waheshimiwa wanzangu watu ambao wanapata mikopo ni wale wajanja ambao wanajua baada ya muda hawawezi kurejesha tena mkopo ule. Uzuri wenyewe Wizara hii mnaye mtaalamu nafikiri alikuwa Ruwanda kaja Tanzania Zanzibar anao uwezo wa kutusaidia, sasa hebu tumsaidia vizuri tuweze kufanikiwa katika shughuli zetu za kuwawezesha akina mama na vijana katika shughuli za uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyengine iwe vyema sio kutuandikia tu kwamba Wilaya hii ilipata hiki, tuorodheshewe na majina ya vikundi hasa. Kwa sababu inawezekana Wilaya hiyo hiyo lakini likawa ni Jimbo moja tu waliopata mikopo ya vijana, majimbo mengine inawezekana wakakaa miaka mitano, kumi, ikawa wao hawapati lakini kwa sababu wapo katika Wilaya ile ikaonekana na wao wanapata. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kunizimia taa mimi niseme kwamba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia sina matatizo nayo, lakini naomba tu ajitahidi tu kwa hayo mambo ambayo nimeyachangia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said ambaye ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa sasa. Lakini kabla ya kuakhirisha kuna wachangiaji watakuja kuchangia jioni na wao waliomba wachangie kwa hizo dakika tano, ataanza Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo), Mhe. Shehe Hamad Matari. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuahirisha kuna tangazo kutoka kwa Mnadhimu wa CCM amesema hapa kwamba ameomba Wawakilishi wote wa CCM baada ya kuahirisha wabakie humu ndani.

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nawashukuru sana wachangiaji wote waliochangia na pia nimshukuru Waziri na Wafanyakazi wote katika Wizara hii nina imani Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ataleta jawabu sahihi ili bajeti hii ipitishwe, tukizingatia ni Wizara ya Wanawake na wachangiaji wengi walikuwa wanawake nina imani hutowaangusha Mhe. Waziri. naakhirisha Kikao mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa majadiliano yanaendelea. Mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mhe. Ali Khamis Bakari una dakika tano na baadae atafuata Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi jioni hii nikiwa mtu wa mwanzo kuweza kuchangia Wizara hii ya Uwezeshaji,Wanawake, Vijana na Wazee katika bajeti ya 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza viongozi wa wizara hii, kuanzia Waziri mwenyewe, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa jumla kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya za kuhakikisha kwamba majukumu haya wanayasimamia vyema na kuona kama Wizara yao inaendelea siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, nikianze nianze kwenye ukurasa namba 3 ambao kuna jumla ya pesa hapa ziliidhinishwa shilingi milioni mia nne na sabini na tano, laki nane na tisini na nne elfu, mia sita na sabini (475,894,670) zilitumika kwa kutekeleza programu ya kukuza usawa wa kijinsia na kuwaendeleza wanawake ambao ni sawa na asilimia 97 ya fedha za programu. Mhe. Naibu Spika, mimi hapa sijafahamu ilikuwa Mhe. Waziri tu namuomba kwamba katika ukurasa huu hizi pesa ambazo zimeidhinishwa hapa sijafahamu huu usawa wa kijinsia na kuendeleza wanawake, sijafahamu kakusudia kuendeleza kivipi.

Lakini nikitoka hapo Mhe. Naibu Spika, niendelee kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuvisaidia hivi vikundi vya ushirika pamoja na vya *SACCOs*, kwa kuwasaidia kwa kuweza kuwapa mikopo ili waweze kujiendeleza. Lakini Mhe. Naibu Spika, vile vile mimi nilikuwa niseme hapa, nimtake Mhe. Waziri kwamba pamoja na kuvisaidia hivi vikundi, lakini vile vile ni vyema kuwasaidia katika kuwatafutia masoko. Mhe. Suleiman alisema kwamba

kulikuwa na wajasiriamali ambao waliwezeshwa mpaka wakafika nje ya nchi kwa ajili ya kuuza makombo alawi, lakini hawa kuna wengine hawana bidhaaa hizi, wengine wana bidhaa ambazo zimo ndani ya nchi vile vile lakini vile vile zatakikana zipelekwe nje ya nchi kwa ajili ya kupata soko. Kwa hivyo ni vyema Mhe. Waziri kwa bajeti hii ambayo tunaijadili na hivi vikundi ambavyo utavisaidia basi ni vyema na wewe ukasimamia kwa jili ya kupata haya masoko, kwa sababu itakuwa pesa zinatolewa, bidhaa zinazalishwa lakini wapi pa kuweza kupata soko inakuwa shida.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile Mhe. Waziri kuhusiana na hivi hivi vikundi, mimi nilikuwa nishauri kwamba mbali ya kutoa hizi pesa kwa ajili ya matumizi, lakini vile vile ungevipitia hivi vikundi ukavikagua ni vingapi mpaka sasa viko hai na vingapi ambavyo vishakufa. Kwa sababu tumeona uko nyuma kuna vikundi vingi ambavyo vimepewa fedha kwa ajili ya kuwezeshwa ili viwe hai, lakini mwisho wa siku kwa mfano kuna vikundi vilivyoanzishwa kwa ajili ya masuala ya mbuzi, wengine ng'ombe kwa ajili ya ufugaji, wengine walikuwa masuala la mboga mboga. Lakini vikundi hivi watu hukaa tu kwa kipindi fulani wakabuni kama tufanye vikundi tuwezeshwe lakini wakishapewa zile pesa, hata miezi mitatu haifiki vikundi hivi vinakufa.Kwa hivyo Mhe. Waziri nilikuwa naomba sana pamoja na watendaji wako ni kweli kwamba vikundi tunataka tuvisaidie, lakini mbali ya kwishakuvisaidia, vile vile tuvifuatilie tuone kwamba vile vikundi ambavyo tuliviwezesha, je, viko haii mpaka sasa ama vishakufa.

Nikitoka hapo Mhe. Naibu Spika, nije kwenye suala la Mabaraza ya Vijana. Mhe. Naibu Spika wengi wao waliokwishakuhangia walisema kuhusu haya Mabaraza ya Vijana kwamba yameanzishwa kwa lengo zuri la kuona kwamba vijana wetu wanajiendeleza katika Mabaraza haya ili kujikwamua na matatizo ambayo wanakumbana nayo. Vile vile Mhe. Naibu Spika, nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba wezangu walizitaja hizi pesa kama ni kidogo na mimi vile vile niseme kwamba kwa fungu hili, kuna fungu ambalo litaangaliwa kwa kupunguzwa basi vile vile na mimi naunga mkono kwamba hizi fedha kwa mara hii ingawa ni mara ya mwanzo, huko nyuma tuliona kuwa hakuna fedha zozote ambazo waliingiziwa, ikiwa ni hii hatua ya mwanzo kwa ajili ya kupewa hii mikopo na kusaidiwa katika hivi vikundi pamoja na haya Mabaraza ya Vijana.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile naomba kwamba Mhe. Waziri kama kutakuwa na uwezekano wa pesa hizi basi ziongezwe kwa sababu haya Mabaraza yametajwa hapa ya vijana yako 52 ambayo haya yatakuwa ya Shehia, yameundwa ya Wilaya karibuni 11 na vile vile kuna ya taifa. Kwa

hivyo haya Mabaraza ni mengi kama wenzangu walivyokusema huko chini vijana wapo na wanasubiria pesa hizi hizi. Kwa hivyo ni vyema zikaangaliwa kwa jicho la huruma ili ziongezewe tuone kwamba vijana wanafaidika siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nije kwenye ukurasa namba 22. Hapa kumetajwa kituo cha kulelea watoto ambacho kilifungwa cha Omar bin Khatab. Mhe. Waziri mimi hapa nataka kujua kidogo. Hiki kituo ni sababu zipi zilizopelekea mpaka kikafungwa. Lakini vile vile Mhe. Waziri hebu tuangalie kwamba baadhi ya watu pengine wapo katika mazingira ambayo hawapendi kuona maendeleo yanatokea siku hadi siku. Kwa mfano inawezekana Mhe. Naibu Spika, watu hawa wameandaa au wameweka hivi vyuo kwa ajili ya kulelea watoto, lakini baada ya muda mfupi ukasikia vinafungwa pengine inawezekana watu hapa wameviwekwa kwa maslahi yao wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, sasa nimwambie Mhe. Waziri afuatilie basi hivi vituo wakati mwengine mtu inawezekana pengine aliona aah! mimi nimeweka kituo kwa muda mfupi, lakini nikishapata ile michangio ya watu wanayokuja nayo au kupata ruzuku, kama zimekatishwa na kile kituo kinakuwa kinafungwa. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri apite kwenye hivi vituo avikague kwa sababu vimekuwa kama uyoga, ni vingi sana, watu wanajiandaa huko kuweka vituo lakini wakiona kama maslahi hayapo na vituo hivi vinafungwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Kusini ambaye alikaa na Kamati yake ya kuunda katika Mkoa wake pamoja na Wilaya, akaona kama apunguze masuala ya udhalilishaji juu ya vijana wetu au watoto wetu ambao wanazurura mno, baadhi yao wakiwa wanahamia katika maeneo ya masoko na fukwe kwaajili ya kupara samaki, akaona ni vyema sasa aandae timu maalum ya kuweza kuwafuatilia vijana hawa ili kuona kwamba wanarudi kule kule katika masomo yao. Nimpokeze sana na niwatake baadhi ya watendaji kama vile Mkoa wangu wa Kaskazini, Wakuu wa Wilaya kule basi na wao waige nyayo hizi za kuona kwamba wanahakikisha na hawa vijana wetu hawabakii majumbani na kuhamia katika sehemu ambazo si nzuri na badala yake warudi kwenye masomo.

Mhe. Naibu Spika, mimi ulinipa dakika tano ni kweli. Kwa hivyo nikimalizia tu niseme kwamba naipongeza Wizara hii na naunga mkono asilimia mia moja.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe. Sasa Mhe. Mhe. Shehe Hamad Mattar baadae ajitayarishe Mhe. Said Soud Said

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima muda huu, lakini nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii na pia nikuongeze kwamba leo tokea asubuhi Wizara hii, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto pia inaongozwa katika Baraza hili na UWAWAZA wenyewe tokea asubuhi.

Baada ya hapo katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi naomba nichangie moja kwa moja katika ukurusa namba 8 unaozungumzia programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji, Vyama vya Ushirika.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii katika ukurasa huu imeonesha mambo mbali mbali ambayo kuwa wameifanyia Vyama vya Ushirika na *SACCOs.* Kwa kweli niwapongeze sana kwa sababu vikundi hivi ni muhimu sana katika jamii yetu na mara nyingi sana huwa tunavishajihisha ili viendelee kuwepo na kuona kama ni namna gani Serikali inaweze kuwasaidia kwa pamoja badala ya kuwa mtu mmoja mmoja. Lakini hata hivyo wameweza kuonesha hapa katika kitabu hiki ukurasa namba 9 kwamba wamefanya ukaguzi katika *SACCOs* 230 na pia wamesema *SACCOs* hizi nyengine zimepanda daraja.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ningeomba kwamba alieleze Baraza hili kwamba kufanikiwa kwao wametumia vigezo gani, viashiria gani kuonesha kwamba hizi *SACCOs* zimepanda daraja, naomba viashiria ambavyo vimeonesha *SACCOs* kutoka sehemu hii mpaka hii kuna mabadiliko yoyote naomba sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine niende moja kwa moja katika ukurasa wa 10. Hapa wamesema wamesaidia uandishi wa miradi mitatu ya usarifu wa mazao ya Vyama vya Ushirika pamoja na kuwaombea ruzuku programu ya *MIVARP*.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu hiki, nimeona katika jadweli namba 8 imeonesha kwamba kuna jadweli hapa inaonesha kwamba miradi mitatu lakini mimi naona sijaielewe hii, jadweli inavyoonesha hapa vyama vikuu vilivyosaidiwa na programu ya *MIVARP*. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri naomba atakapokuja afafanue hii miradi hapa hizi shilingi milioni mia moja na ishirini na moja, laki tano (121,500,000) tayari ambapo ndio wamepata msaada hizi *SACCOs* na hizi milioni kumi na tatu na laki tatu (113,300,00) walicholipa sijakuwelewa kabisa hapa. Ninataka nielewe ni kitu gani kilichofanyika hapa katika jadweli hii ili niweze kujua kama kuna maendeleo yoyote yaliopatika. Lakini vile vile kuhusu wajasiamali hao ambao kuwa

wamejitokeza pia ningejua suala zima la kujua kiwanja cha wajasiriamali Kitogani kimefikia wapi hadi sasa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 11. Mhe. Waziri alieleza kwamba anahitaji shilingi milioni mia tatu na thamanini na mbili elfu (382,000,000). Sasa niulize fedha hizi. Je, ni kwa Ofisi au ni kwa hawa walengwa wajasiriamali ambao kuwa wataweza kukopeshwa au kusaidiwa kwa ruzuku. Kwa hivyo ningependa nielewe katika hizi milioni mia tatu thamanini walizoziomba hapa kwamba tumuidhinishie, vipi zitakavyotumika alivyokusudia.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika hotuba ya Mhe. Waziri katika ukurasa namba 24 kwenye maendeleo ya vijana. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua kwamba idadi kubwa katika nchi ni vijana popote pale na vijana wana kero zao. Vijana mara nyingi sana wanalalamika kuhusu ajira na hicho ni kilio sio cha kwetu sisi, kwa kweli ni kilio cha dunia nzima, hata hizo nchi zilizoendelea zina matatizo hayo hayo. Kwa hivyo Waziri ameonesha hapa amechukua hatua mbali mbali, kama vile amechukua hatua mbali mbali, kama vile kuwapa elimu ya stadi za maisha, mafunzo mbali mbali kwa Unguja na Pemba na kutatua baadhi ya changamoto ikiwemo kuchimba visiwa kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji maji katika ukulima.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo nimefarijika kuona kwamba pale waliposhirikiana na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo, katika programu ambayo kuwa inasema kwamba itakapofika mwaka 2030 tutokomeze umaskini kwa uzalishaji endelevu na matumizi yenye tija.

Mhe. Naibu Spika, katika mpango huu unaonekana hapa ni mzuri sana lakini nashauri sasa. Shauri langu katika vikundi hivi na ile tufikie hapo kutokomeza umaskini, uzalishaji endelevu ni kuwajengea vijana hawa kuwaweka pamoja, kuwajengea nyumba za *green house. Green House* au kwa jina jengine nyumba za kijani ambazo zitakuwa na uzalishaji wa uhakika na kwa muda wote, tuwape taaluma ambazo kuwa hawa wakiweza kupata kitu kama hichi, basi wataona mabadiliko ambayo kuwa hawatahitaji hata kazi za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kilimo ni kitu ambacho kuwa ni ajira tosha lakini wengine wanaona kama ni adhabu, lakini kwa walikwishajaribu kilimo basi kinamkomboa mtu katika hali ya unyonge kabisa. Kwa hivyo nashauri sana wajengewe *green house* katika Mikao yetu na katika Wilaya zetu wakabidhiwe, na hii iwe kionesho kwa wale wengine watakapoona mafanikio pale waweze kuiga. Lakini kabla hapajafanywa jambo hili, ninaomba sana Wizara ifanye

juhudi ya kufanya utafiti wa udongo kwa sababu nchi mwetu tuna tabia na hatuna uwezo huo tufanye kwa namna yoyote ile kwa kufanya utafiti wa udongo ili kazi yote hii isije ikawa ni bure, tumekuwa tunapata matatizo hatua maabara ambayo ya kujua kwamba udongo huu unahitaji kilimo gani na udongo huu unahitaji nini. Kwa hivyo ni imani yangu kwamba wazo hili atalichukua na kulifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika ukurasa namba 27 kuhusu Baraza la Vijana. Vijana kama nilivyoeleza kwamba ndio nguvu kazi. Ninashukurusa sana walipoonesha kwamba vijana Mhe. Rais amekubali liundwe Baraza hilo, lakini Baraza limeundwa na sasa vijana wapate haki zao, ili tuendelee vijana hawa lazima wapewe mafunzo zaidi na zaidi ya kuona kwamba Serikali yao inawajali. Kwa sababu vijana hawa wamekuwa wakichukuliwa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wakiwaambia kwamba Serikali ina ajira nyingi lakini haitaki kuwapa, kitu ambacho sio kweli. Kwa hivyo vijana hawa wakitumiwa vizuri, wakielimishwa katika Mabaraza yao haya, naona tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana. Kwanza vijana wanaweza kutumiwa katika kuleta uchafuzi wa nchi lakini pia vile vile hawa wakitulizwa amani inaweza kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, Mabaraza haya lakini nao vile vile yanakabiliwa na changamoto ambazo kuwa nahitaji kuona kwamba zinatatuliwa kwa haraka sana. Hapa katika ukurasa huu inaeleza kwamba ...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa dakika moja umebakiza

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Dakika moja.

Hata hivyo Mabaraza haya naomba sana yapewe kila mbinu ambayo kuwa yataonekana wao wanajaliwa na Serikali ya Mapinduzi. Kwa hivyo isiwe tunatengeneza Mabaraza haya lakini yanaishia kwenye vitabu, naomba sana sana Mhe. Naibu Spika kwa Mhe. Waziri waliangalie suala hili.

Baada ya hayo nauonga mkono hoja asilimia mia juu mia. Baada ya maelezo hayo atakapokuja lakini naomba sana anieleze kama nilivyoomba katika maelezo yangu.

Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante mchangiaji anayefuata sasa hivi ni Mhe. Said Soud Said. Mheshimiwa nakupa dakika kumi.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie wizara hii, wizara mama. Wizara ambayo kwa kweli kwanza nichukue nafasi ya kumpongeza Dkt. Ali Mohamed Shein. Nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwa na imani kabisa ya kunyanyua jinsia katika demokrasia. *(Makofi).*

Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein amemchagua Mama Maudline Castico pamoja na Mama Shadya pamoja na watendaji wao wa kike, wakiwa na maana ya kwamba ananyanyua demokrasia katika Zanzibar na Tanzania kwa jumla.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spka, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hakufanya makosa ya kumchagua Mama Castico, kwa sababu nimemuamini na ninamkubali kwamba mama huyu anafanyakazi ya uhakika kuwatetea wanawake, anawatetea wanawake wa nchi hii pamoja na watoto na nimeshuhudia mimi mwenyewe akitoka machozi pale anapoeleza udhalilishaji unaofanywa juu ya watoto wa nchi hii.(*Makofi*).

Kwa hivyo mimi namuamini na namkubali na naseme amepewa mzigo mzito, kwa sababu wizara yake imechukua mambo sita. Wizara hii imechukua mambo sita mambo ambayo yote ni muhimu. Kwa kweli ni kwamba wizara hii imechukua wazee, vijana, watoto, uwezeshaji, kazi, mambo haya si mepesi ni mambo makubwa Mhe. Naibu Spika. Kimsingi katika hali ambayo sasa hivi inapaswa tumsaidie ni kwamba sasa sote sisi Wawakilishi tuliomo katika Baraza hili, tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba ubakaji na udhalilishaji hautokei katika majimbo yetu. Na sisi kama viongozi tunayo nafasi kubwa ya kuweza kusema kwamba tusisubiri udhalilishaji ukatokea au tusisubiri jambo baya likatendeka wakati wizara hii tuna uhuru wa kufika na kumueleza Mhe. Waziri, tukamueleza Mhe. Naibu Waziri au Katibu Mkuu kwamba kuna moja, mbili, tatu katika jimbo langu, naomba msaada wako. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nina imani kabisa kutokana na serikali yetu ilivyokazana kabisa kupambana na hoja hii, nina imani kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa na udhalilishaji huo hautatokea. Lakini kama sote tutakuwa tuna mawazo ya kuja humu ndani na kujiandaa kwa ajili ya kutoa hoja hizi na zile, mimi nadhani tutakuwa hatuitendei vyema serikali yetu. Lazima tukubali kwamba sisi ndio wenye serikali, sisi ndio Wawakilishi wa wananchi, sisi ndio watumwa na tuliokubali kutumika kwa ajili ya serikali yetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa basi, tukisema kwamba Wizara hii imepewa shilingi 55 milioni hazitoshi, hata tukipeleka shilingi bilioni moja kama hatujakuwa tayari kuzuwia udhalilishaji, shilingi bilioni moja itatafunwa na udhalilishaji utatokea, pesa sio inayozuwia. Mhe. Naibu Spika, nataka niseme pesa sio inayozuwia udhalilishaji. Kitakachozuwia udhalilishaji kwanza ni kujipanga sisi wenyewe kwamba tunakataa udhalilishaji, halafu tukawa tayari sasa kutoa adhabu kali kwa watu wanaodhalilisha watoto. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuna watu wengine wamesema wanyongwe, wengine wamesema hivi, wengine wamesema vyengine. Mimi nasema mdhalilishaji hana haja ya kunyongwa, afungwe miaka 30 atolewe kwenye televisheni wiki mbili, aandikwe kwenye magazeti basi, hakuna mtu yeyote atakayemdhalilisha mtoto. Lakini hata tukitoa shilingi bilioni moja narudia kusema kwamba udhalilishaji kama hatujakubali sisi wenyewe kupiga vita, udhalilishaji utatokea. Kwa hivyo mimi nafikiri nataka niseme tu kwamba serikali ilipomteuwa yule mama pamoja na Katibu Mkuu na Manaibu wake pamoja na wataalamu wao, wakaleta bajeti ya shilingi 55 milioni, *it is reasonable*, walikwishaona kwamba pesa hii inatosha. Hii wizara inaendeshwa na wataalamu, kuna wataalamu hapa, sio wizara kama anaendesha Mama Castico (Mhe. Waziri) pamoja na Mama Shadya (Naibu Waziri). Wizara ina wataalamu na kwa sababu ina wataalamu wameshagundua kwamba shilingi 55 milioni zinatosha, kilichobakia ni juhudi na jitihada za serikali kuhakikisha udhalilishaji unaondoka.

Sasa basi, ningetaka niseme hivi, kwa mantiki hii kilichobakia sisi ni kuongeza nguvu na jitihada katika kuendelea harakati za kumfanya mwanamke, mtoto na mzee anapata haki sawa katika nchi hii. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, si watu wengi ambao wanajua thamani ya vijana, lakini nataka niseme kwamba vijana ni nguvu kazi ya taifa na lazima vijana wapewe *priorities* ya mambo yote yanayokuja katika nchi, ikiwemo ajira na mambo mengine na mama huyu anajitahidi. Kuna watu Mhe. Waziri ameshawapeleka Dubai, Sharjah, Kuwait na kwengineko. Pia sisi sote tumeshuhudia sasa wazee wetu walioko katika Nyumba za Wazee wanakula kuku na nyama za kawaida hata kama ni wiki mara moja, kwa jinsi ya kuwashughulikia na kuwapeleka katika mazingira yale ambayo yanafaa.(*Makofi*).

Mhe. Waziri pia amekuwa na jitihada za makusudi kuwatetea watoto na kuwafuatilia matokeo mbali mbali katika mahospitali, katika majumba yao na katika shughuli zao. Sasa mimi nataka niseme kwamba ni wajibu wetu, sisi kama viongozi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaoiwakilsha serikali

hapa katika Baraza na kutunga sheria, tuwe tayari kumsaidia Mhe. Waziri na wizara yake ili aweze kupiga hatua ile ambayo inatakiwa na taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nasema tena kwa mara nyengine kwamba sisi ndio wenye dhamana ya kuhakikisha serikali inatekeleza sera yake ya Chama cha Mapinduzi na miongoni mwa sera ya Chama cha Mapinduzi ni kuhakikisha kwamba watoto, vijana na wazee wanapata haki zao. Sasa leo tusibakie kulaumu wakati sisi ndio tunaotakiwa tutekeleze hizo sera. Sera za Chama zinatakiwa zitekelezwe na zisimamiwe. Sasa miongoni mwa kuzitekeleza na kuzisimamia ni kuhakikisha kwamba kwanza ile bajeti inayoletwa na Mhe. Waziri inapita, sio kupiga mabuti mnazuwia, mnazuwia nini, mnazuwia kitu gani.

UTARATIBU

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, nainuka na Kanuni ya 68 "Mjumbe anaposema mambo yasiyofaa". "Baada ya kujuulisha Baraza juu ya tabia ya Mjumbe anayeshikilia kusema mambo yasiyofaa kwa mujibu wa Kanuni hizi, Spika anaweza kumuamuru Mjumbe huyo kukatisha hotuba yake na kukaa". *(Makofi)*

Mhe. Nabu Spika, sisi tumetoa mawazo Wajumbe na tumezungumza kwa mujibu wa Kanuni ya Baraza la Wawakilishi tuna haki ya kushauri na kutoa michango kwa mujibu wa nchi tunavyoona. Sasa Mhe. Waziri akitu-*crush* akisema shilingi 55 milioni zinafaa au suala la sheria kwamba mtu asinyongwe haiwezekani yeye anataka mtu asinyongwe, au yeye ndiye anayehusika na mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, naomba muongozo na namuomba sana afute kauli yake aheshimu kauli za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ana haki na yeye ya kuchangia, lazima mlielewe hilo, ana haki isipokuwa tu nitamwambai Mhe. Waziri kwa sababu yeye anachojaribu kufahamisha, anawafahamisha Wajumbe yale mambo ambayo Wajumbe wamesema na yeye ni Waziri. Ni sawa sawa na kwamba anajibu hoja.

Kwa hivyo tumuachie sisi tulipata nafasi huko *back benchers* wakazungumza, sasa tumuachie ana dakika zake tatu anamalizia.

Mheshimiwa malizia, najua hayapendezi maneno yake lakini tumuachie amalizie. *(Makofi)*

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, kwanza nafurahi sana kwa watu kujifunza siasa kupitia kichwa hiki. Nafurahi sana kwa sababu mimi nimefanya siasa. *(Makofi/Kicheko).*

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa endeleana hoja yako. Mhe. Nadir Abdul-latif sijakupa ruhusa ya kusimama. Nimeshasema anaendelea na hoja yake.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, utaratibu. Hujanipa ruhusa, huyu mpinzani Mheshimiwa si mwana CCM.

Mhe. Naibu Spika: Haya sawa, endelea Mheshimiwa na hoja yako.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Kwanza nataka ajue kwamba mimi nimekuja humu kwa tiketi ya Chama cha Upinzani. *(Makofi)*

(Hapa palitokea zogo la Wajumbe kumpigia Mhe. Said Soud Said)

Mhe. Naibu Spika: Nimesema usijibu hoja Mhe. Said Soud Said, kaa kitako. Mheshimiwa tunaendelea Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kuchangia machache kuhusiana na Hotuba ya Bajeti ya Makadirio ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba kuchangia yafuatayo kutokana na michango mingi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wamejaribu kuchangia. Kwanza kabisa nataka kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inafanya kazi kwa mashirikiano makubwa sana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto katika kupambana na masuala mazima ya kesi za udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha hili linafanikiwa vizuri, Wizara zetu mbili hizi zimeunda timu ya pamoja kufanya kazi kwa pamoja katika kuona na kufuatilia namna kesi za udhalilishaji zinavyokwenda mbele. Kesi hizi Mhe. Naibu Spika, ni kwamba zinaporipotiwa basi Ofisi ya Mrajis wa Elimu inazifuatilia na kuzipeleka Polisi na Polisi nao wanafuata hatua zao.

Mhe. Naibu Spika, sio wizara mbili peke yato tu lakini vile vile wizara mbili hizi zinashirikiana na Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa; Mahakama na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa pamoja tunafanya kazi kuhakikisha kwamba kesi za udhalilishaji zinamalizika na tunapambana nazo. Lakini nataka niseme tu kwamba wizara peke yake haziwezi kufanya kitu, bali mashirikiano ya pamoja ndani ya jamii yetu ndio ambayo yanaweza kutokomeza vitendo hivi vya udhalilishaji.

Mhe. Naibu Spika, sisi sote humu ni wazazi na kila mzazi anaumwa na anaumia kuhusiana na kesi hizo za udhalilishaji. Kwa hivyo tukishirikiana kwa pamoja basi tunaamini kwamba kesi hizi zote zinaweza kumalizika. Katika kulihakikisha hilo Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mrajis wa Elimu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka huu imepokea kesi za ubakaji na ulawiti zipatazo 26 kwa mwaka 2016/2017. Hizi ni kesi tu ambazo zimeweza kuripotiwa lakini baada ya kufuatilia zaidi kuna kesi nyingi ambazo hazitolewi wala hazisemwi. Kwa hivyo ni kusema kwamba wizara zetu mbili hizi zinafanya kazi kwa mashirikiano ya karibu zaidi ili kuona kwamba kama kesi ambayo sisi tumeipata, wenzetu hawajaipata tunashirikiana kuona kwamba tunawalinda watoto wetu. Kwa sababu Mhe. Waziri hapa yeye ana watoto na mimi nina wanafunzi na wanafunzi hawa ndio watoto wetu. Kwa hivyo wanapoathirika maana yake linaathirika kundi zima la vijana wetu na viongozi wetu wa baadae.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hili kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tumeanzisha Kitengo cha Ushauri Nasaha. Kitengo hiki kipo katika skuli zote za Unguja na Pemba. Nia na madhumuni ya kitengo hiki ni katika kuwashauri vijana kuhusiana na masuala mazima ya kukabiliana na mahitaji ya jamii na makundi rika. Kwa sababu tunaona kwamba mwanafunzi anapopata ushauri nasaha inakuwa inamsaidia angalau namna ya kuweza kujitambua na kujielewa na vile vile kuweza kujikinga yeye kama yeye.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Wizara ya Kazi ina sheria ya kumlinda mwari na mtoto wa mzazi mmoja ya mwaka 2005. Katika kifungu cha 4, Sheria hii inamlinda mwanafunzi ambaye kwa bahati mbaya labda atabakwa na kupata ujauzito. Mhe. Naibu Spika, Sheria hii inamlinda mwanafunzi kuweza kuendelea na masomo yake baada ya kujifungua. Kwa hivyo hii yote inadhihirisha namna gani wizara zetu hizi zinafanya kazi kwa pamoja.

Vile vile ningependa kuchangia katika suala zima la mambo ambayo yanapelekea kuongezeka kwa masuala ya udhalilishaji wa watoto. Kuna

mambo mengi ambayo yanasababisha, lakini miongoni mwa mambo hayo ni suala zima la ucheleweshwaji wa kesi katika kufikia hatua ya mwisho. Ucheleweshaji wa kesi Mhe. Naibu Spika, kutoka Polisi kwa *DPP* kwenda Mahakamani, ucheleweshaji wake huwakata tamaa baadhi ya watu wengi na wengi huona kwamba hakuna umuhimu wa kuripoti kesi hizi.

Mhe. Naibu Spika, jambo hili linapelekea sana vitendo vya ubakaji na udhalilishaji kuweza kuendelea kwa sana. Kwa hivyo bado tunarudi kwamba jamii tushirikiane tuhakikishe kwamba tunawaripoti wale wote ambao wanaofanya vitendo hivi ili hatua kali ziweze kuchukua mkondo wake na tuwaripoti lakini vile vile tuwe tayari kwenda kutoa ushahidi ili kesi hizi ziweze kwenda mbele.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo linapelekea kuongezeka kwa vitendo hivi ni mmong'onyoko wa maadili. Sote humu ni mashahidi tunaona kwamba sasa hivi kuna vitendo vingi ambavyo viko tofauti na maadili yetu ya kiasili ya Kizanzibari. Jambo hili linapelekea sana masuala mazima ya udhalilishaji. Suala moja wapo ni masuala mazima ya mavazi. Tunaona kwamba mavazi yanayovaliwa sasa hivi sio mazuri, lakini hata hao watu wengine wazee labda hawajielewi kwa sababu kuna watu ambao wanabaka watoto wadogo miezi minne, hapana mavazi lakini kutokujielewa kwao. Kwa hivyo ni suala ambalo linapelekea kwa hizo kesi.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile suala zima la kuvunjika kwa ndoa. Ndoa zinapovunjika watoto hulelewa na mzazi mmoja. Hili nalo vile vile linapelekea kuongezeka kwa kesi hizi kwa sababu miongoni mwa wazee ambao wanalea watoto hawa, basi mmoja wao huwa ni chanzo cha kuharibika ama chanzo cha kuharibiwa kwa mtoto. Kwa mfano, mama ambaye ameachwa na kukaa na baba wa kambo, baba wa kambo kesi nyingi ambazo zinatokea wako baba wa kambo ambao wanawaharibu watoto wa wake zao. Kwa maana hili nalo linachangiwa sana na kuongezeka kwa hizi kesi za udhalilishaji.

Suala jengine vile vile ni masuala mazima ya utandawazi. Dunia sasa imekuwa ni kama kijiji. Kwa hivyo hili nalo lina athari yake na athari yake ni kwamba watoto wetu ama vijana wengi wamejikuta wanaangalia masuala ambayo hayawahusu kinyume na umri wao. Kwa hivyo hii huwapelekea pengine kutaka kujaribu yale masuala ambayo wanayaona. Lakini vile vile utandawazi umeweka mambo mengi kuwa bayana kiasi kwamba hakuna siri kwa mtu ambaye umri haujafikia. Kwa hivyo hili nalo linapelekea suala zima la kuongezeka kwa kesi za udhalilishaji.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kupotea kwa utamaduni wa malezi. Zamani wazee wetu walivyolelewa ni kwamba mtoto alilelewa na jamii nzima, lakini sasa kila mtu analea mwanawe, jirani hathubutu hata kumgombeza mtoto na akimgombeza basi yule mzazi mwenyewe anakuja juu. Kwa hivyo hili nalo pia linapelekea masuala kama haya kuweza kuendelea na kuongezeka siku hadi siku.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, ni mabadiliko ya mfumo wa maisha. Wazazi wengi sasa wamekuwa wako *busy* na maisha. Kila mmoja yuko *busy*, mzazi akitoka nyumbani asubuhi anarudi usiku, hana hata muda wa kukaa na mtoto wake angalau kuweza kumuelimisha masuala mbali mbali ambayo yanamuhusu mtoto kuweza kujielewa. Kwa hivyo hili nalo linapelekea mzazi kutokujua nini kinamkuta mtoto wake, lakini hata kama kapatwa na jambo basi vile vile mzazi anashindwa kuelewa kwamba mtoto wake amebakwa ama amelawitiwa. Mhe. Naibu Spika, haya ni miongoni mwa mambo ambayo yanapelekea kuongezeka kwa kesi za udhalilishaji.

Jengine ni mashirikiano ya pamoja hayapo. Kwa sababu inapotokezea kesi hata kama imeripotiwa unakuta mashirikiano baina ya familia mbili upande wa baba na mama yanakosekana. Hali hii hufanya kesi hizi ziweze kuendelea siku hadi siku kwa sababu kuna wengine wanaficha, wengine wanataka kwenda mbele. Mwanamke akitaka kwenda mbele anatishiwa talaka. Kwa hivyo hili nalo linapelekea kesi hizi kuweza kuongezeka siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine ambalo limechangiwa ningependa vile vile kulizungumza ni suala la kuvunjika kwa ndoa kiholela na kukosekana kwa mgawanyo wa mali. Serikali yetu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeanza kupitia Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya mwaka 1985. Sheria hii imeonekana kwamba imeanza kupitwa na wakati na Sheria hii inazungumzia masuala ya ndoa na mgawanyo wa mali.

Kwa hivyo tupo katika mchakato wa kuweza kuitengeneza Sheria hii ili iweze kuja katika Baraza lako tukufu, na tunawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe Sheria hii itakapokuja basi tuweze kuichangia sana ili kama kuna mambo ya kuongeza tuyaongeze ili iendane na wakati wa sasa na ionekane kwamba endapo itatokezea suala la talaka, basi kila mmoja aweze kupata haki yake na mgawanyo wa mali uweze kupatikana baina ya mwanamke na mwanamme, na mwanamke asiwe kaachwa tu peke yake halafu akakosa pa kuanzia kushika maisha yake.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, niombe kuchangia kuhusiana na suala zima la lengo la serikali kujenga nyumba za wazee. Lengo la kujengwa nyumba hizi ni kuwahifadhi wale wazee ambao hawana familia yoyote wala hawana raslimali yoyote. Kwa hivyo lengo hili la serikali linafanyika vizuri. Kutokana na hili hatuoni haja ya kujenga nyumba za wazee katika kila mkoa, kwa sababu nyumba zilizopo zina nafasi kubwa sana na zinatosheleza kukidhi wazee hawa. Lakini endapo tutajenga nyumba katika kila Mkoa, hii itatoa fursa kwa vijana kuweza kuwaacha wazazi na kutokuwashughulikia na huo ni wajibu mkubwa sana wa kila mtoto kumlea mzazi wake, tuwalee wazazi kama ambavyo wao wametulea.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo kutokana na hili ni kwamba serikali bado haijaona haja ya kujenga nyumba za kulelea wazee katika kila Mkoa na nyumba zilizopo basi zitatumika kulea wale wazee ambao hawana familia za kuweza kuwategemea. Tunaomba sana jamii hususan vijana basi tuwalee wazazi wetu na tusiwatupe, kwa sababu wao wametulea sisi wakati tuko wadogo wanapokuwa watu wazima wanajisikia faraja sana kuona kwamba mtoto wake ndiye ambaye anamtunza mpaka mwisho wa uhai wake, endapo mtu unafanya hivyo basi tutambue kwamba ukimtupa mzee wako na wewe vile vile watoto wako watakuja kukutupa.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja ya makadirio haya kwa asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa nitampa nafasi Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Nakuomba utumie muda usiozidi dakika 15 tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia na kuweza angalau kujibu baadhi ya hoja za Wajumbe ambao walitaka ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, nianze basi kwa kumuomba Mwenyezi Mungu anijalie niweze kujibu hoja hizi na Wajumbe waweze kufahamu na kutuelewa ili na wao Mwenyezi Mungu awape moyo wa kuweza kutupitishia bajeti yetu hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nianze na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, suala alilouliza suala alilouliza bajeti ya udhalilishaji ni nyingi na vitendo vya udhalilishaji vinaendelea.

Naomba kumjibu Mhe. Naibu Spika, kwamba ni kweli hata wizara nayo inasikitika kuona vitendo hivyo vinaongezeka. Hata hivyo fedha hizo si za masuala ya udhalilishaji tu bali zimetumika katika harakati mbali mbali ikiwemo kuhamasisha uongozi wa Dini, kuratibu mikutamo ya Mawaziri, kutengeza mpango wa kazi wa kitaifa wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto pamoja na kuzijengea uwezo Kamati za Shehia.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo naomba nimjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mheshimiwa wangu huyu wa Jimbo la Chake Chake, yeye alitaka kujua ndoa zinavunjika kiholela hakuna mgawanyo wa mali.

Naomba nikubaliane naye kwamba wimbi la talaka Zanzibar linachangiwa na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Wizara katika kulifanyia kazi suala hili, inafanyakazi karibu na Mahakama ya Kadhi ili kuhakikisha watoto wanapata matunzo na haki zao. Wizara imeshajihisha mapitio ya Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya mwaka 1985 ambapo inazungumzia masuala ya ndoa, talaka na mgawanyo wa mali katika kuvunjika kwa ndoa.

Mheshimiwa mama yangu pale Mhe. Panya Ali Abdalla alitaka kujua katika utafiti, wizara imegundua nini kuhusiana na masuala ya udhalilishaji wa watoto. Naomba kumjibu kwamba masuala ya udhalilishaji yanasababishwa na mmong'onyoko wa maadili, kuvunjika kwa ndoa utandawazi, uadilifu katika malezi na makuzi ya watoto.

Mhe. Naibu Spika, halafu Mhe. Suleiman Sarahan Said aliendelea kutaka ufafanuzi wa umri kuanzia mtoto wa siku moja mpaka miaka mia. Kwa mujibu wa Sheria ya Mtu Mzima ni miaka 15, 18, 21 na kwa wale watoto wanaofanya makosa. Kuhusu ufafanuzi wa umri kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Namba 6 ya mwaka 2011 imefafanua kwamba mtoto ni mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18 na Sheria ya Baraza la Vijana 2013 na Sera ya Vijana 2015, kijana ni kuanzia umri wa miaka 15 hadi 35.

Sera ya Hifadhi ya Jamii ya 2014, mzee ni kuanzia miaka 60 na kuendelea. Kimataifa kijana ni miaka 15 hadi 24, mtoto miaka 0 hadi 18 na mzee ni miaka 60 na kuendelea.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir yeye alitaka kuhusu sheria zinazorudisha nyuma masuala ya ushahidi kuletwa Barazani. Sheria zinazoshughulikiwa masuala ya ushahidi ni pamoja na Sheria ya Ushahidi Namba 9 ya mwaka 2014 na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Namba 7 ya mwaka 2004 na Sheria ya Jinai ya mwaka 2014.

Sheria ya Ushahidi tayari imeshaletwa Barazani na imeshatiwa saini na Mhe. Rais. Sheria ya mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 2014 na Sheria ya Jinai zinafanyiwa kazi. Ni vyema kuwahimiza wahusika wazilete Barazani. Tunatarajia Sheria hii italetwa Barazani karibuni kujadiliwa. Tunaomba Waheshimiwa Wawakilishi itakapoletwa basi waichangie na kuiboresha.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na Mhe. Panya Ali Abdalla alitaka kujua tangu Mahakama ya Mtoto ya Mahonda ianzishwe kesi ngapi zimefunguliwa. Naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla kwamba tangu Mahakama ya Mahonda ifunguliwe ni kesi mbili za watoto zilizoorodheshwa. Mhe. Tatu Mohammed Ussi alitaka kujua je, kuna nyumba ya kuweka vijana wanaotelekezwa kwa upande wa Pemba. Naomba kumjibu kwamba hakuna nyumba iliyowekwa kuwahifadhi vijana waliotelekezwa kwa upande wa Pemba. Utaratibu ni kwamba wakijitokeza kuleta malalamiko katika Wizara inashughulikiwa suala hilo na ikishindikana linapelekwa katika vyombo vya sheria.

Mhe. Asha Abdalla Mussa alitaka kujua kwa nini Pemba hakuna kesi hata moja ya kubaka. Napenda kumjibu kwamba Wizara inaripoti malalamiko yanayoripotiwa Ofisini tu, inawezekana matukio ni mengi lakini wahusika hawaripoti Ofisini, huwa wanaripoti katika maeneo mengine ikiwemo Polisi na vituo vya mkono kwa mkono.

Aidha wizara imeripoti matukio yaliyoripotiwa Vituo vya Mkono kwa Mkono katika ukurasa wa 22 ya aya ya kwanza. Alitaka kujua tofauti ya takwimu za udhalilishaji. Takwimu zilizoripotiwa ni za utekelezaji wa mwaka 2016/2017 kutoka Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto Unguja na Pemba. Vile vile alitaka kujua watoto wanafanyiwa vitendo vya udhalilishaji wanapewa hukumu gani. Napenda kumjibu kuwa Sheria ya Mtoto Namba 6 ya mwaka 2011 imeainisha huduma ambazo wahanga wanatakiwa kupewa, ikiwemo ushauri nasaha na huduma za matibabu. Kwa mwaka huu Sheria ya Mtoto inatarajiwa kufanyiwa mapitio kuangalia changamoto zilizopo.

Mhe. Ussi Yahya Haji yeye alishauri nyumba za wazee zijengwe kila Mkoa. Hili Mhe. Waziri wa Elimu naona tayari ameshalitolea maelekezo. Mhe.

Abdalla Maulid Diwani matumizi ya mzabuni yamekuwa makubwa. Mzabuni analeta huduma kwa mujibu wa matwaka yetu lakini ifikapo mwezi wa Juni 2017 mfumo wa zabuni utakatishwa.

Halafu Mhe. Abdalla Maulid Diwani aliuliza kwamba idadi wa Wakoma wailioko Welezo ni 33 lakini wameripotiwa 55. Napenda kumjibu kwamba Welezo hakukai wazee walioathirika na Ukoma, bali wanaishi wazee waliokuwa hawajiwezi ambao wanahitaji huduma. Wazee walioripotiwa hapa ni 55, waliathirika na ukoma wanaishi Makundeni Pemba ambao wanalipwa shilingi ishirini na tano elfu kila mmoja kwa kujikimu kwa kila mwezi. Vile vile Mhe. Abdalla Maulid Diwani alitaka kuwepo kwa madaktari na usafiri wa wazee.

Napenda kumjibu kwamba kuna utaratibu wa madaktari wanaopita kila mwezi kuchunguza afya za wazee na kuwapatia matibabu. Aidha kituo cha Afya kinasaidia kutoa huduma. Suala la usafiri ni kweli ni muhimu linaendelea kufanyiwa kazi, tayari suala hili linashughulikiwa lakini misaada kama TV na usafiri kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe kuwachangia wazee wetu tunapokea.

Mhe. Suleiman Makame Ali kuhusu nyumba ya Limbani imewekwa uzio na waya hakuna mlinzi. Napenda nimjibu kwamba ni kweli nyumba ya wazee Limbani imewekewa uzio wa waya, lakini vile vile wapo walinzi wanne na wanalinda kila siku. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kuhusu fedha za wazee zinaliwa. Je, ni kiasi gani cha ubadhirifu uliofanyika na hatua gani zimechukuliwa kwa watendaji ambao si waadilifu.

Mhe. Naibu Spika, ninapenda kumjibu kwamba hakuna fedha ya mzee iliyobainika kuibiwa. Fedha za wazee wanaofariki na wasiochukua zaidi ya miezi mitatu zimekuwa zikirudishwa Mfuko Mkuu wa Hazina. Kuanzia Julai 2016 hadi kufikia mwezi wa April 2017 kiasi cha shilingi milioni mia moja hamsini na tatu, laki nne, kumi na mbili elfu zimerejeshwa na kasoro ndogo ndogo zinajitokeza na bado tunaendelea kuzifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitaka kupata ufafanuzi kuhusiana na vifungu mbali mbali. Naomba kumjibu kuwa fungu HG01030104 bilioni saba milioni mia tisa arubaini na saba laki moja na mbili kati ya fedha hizi shilingi bilioni sita nukta tano ni kwa ajili ya pencheni ya jamii. Fedha zilizobaki ni kwa ajili ya matumizi mengine ya Idara ikiwemo hifadhi ya mtoto, hifadhi ya wazee, hifadhi ya jamii, kuzika maiti zisizokuwa na wenyewe na shughuli za uendeshaji.

Kuhusu fedha za kuazimisha siku wa wanawake duniani. Wizara imepangiwa shilingi milioni kumi na mbili na ishirini elfu na sio milioni mia moja na ishirini. Kuhusu ufafanuzi wa fungu la mishahara Pemba ni shilingi milioni mia sita thamanini laki nne sabini na nane elfu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo na mimi natamka kwamba naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Sasa basi nimpe nafasi Mhe. Waziri aje ajibu hoja.

Mhe. Waziri naomba nikukumbushe tu kwamba una muda wa saa moja kwa ajili ya kutoa hoja, iwapo hutamaliza naomba useme kwamba majibu mengine yaingie kwenye *hansard*.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto napenda kushukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waliochangia hotuba ya Wizara wa moja kwa moja na kwa maandishi. Jumla ya Wajumbe waliochangia kwa maandishi Mhe, Naibu Spika, ni 16 na baadae nitawataja na waliochangia moja kwa moja ni watu 22. (*Makofi*)

Pia napenda kuwashukuru Mheshimiwa Wajumbe wote walioko hapa ambao tuliokuwa tukijibu.

Kwanza napenda kusema kwamba namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutusaidia kwamba tumefika kipindi hichi na hakuna kilichonifurahisha mimi leo, kama nyinyi Wajumbe mlivyochachatika kuchangia wizara inayowahusu moja kwa moja. Hamuwezi kuamini ninawabariki na ninawapenda sana, kwa sababu masuala yote haya yanawahusu sana nyinyi na mimi ni masuala ya jamii, nyinyi kati yenu ni mababa ni mama ni mabibi ni babu. Kwa hivyo masuala haya ya Wizara yangu wanawagusa moja kwa moja na ndio maana mmeweza kuchangamka na damu zinawachemka. Najua hapa mnasubiri Waziri suala fulani atajibu vipi. Nitajibu tu wala msiwe na ghofu kwa sababu ninachojibu ni michango ya uwelekezi wenu na kwa Kamati mahiri ya kudumu ya Wizara yetu ambayo ambayo iko chini ya Mhe. Mwenyekiti wetu Ali Suleiman Ali (Shihata). (*Makofi*)

Kipindi kilichopita Baraza zima lilichangamsha sana Wizara yetu lakini hiyo nasema kwamba nimeshukuru kwa sababu mmetuchangamsha na kufundisha kazi, ndio maana leo hii mnasema kwamba wazee wanawapongeza wanakula vyakula kama mlivyosema siku moja wanakula hiki na hiki, kabla sijamaliza mkasema aah! sivyo ilivyo. Nilikuwa nataka kusema wamepaswa kula nini. Kwa hivyo mambo yamezidi kuwa mazuri. Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kabisa napenda niwapongeze sana na yote yaliyotokea humu naamini yataingia kwenye *hansard.(Makofi).*

Lakini pia nikupongeze wewe Mhe. Naibu Spika, unajua tulipoanza Baraza wanawake tulizubaa lakini tangu walipoanza UWAWAZA moto wa kuotea mbali, na ni jana tu au juzi Mheshimiwa tumepata vyeti rasmi ambavyo tukivionesha popote duniani tutakwenda makongamano ya aina yoyote na tutakaribishwa. Kwa hayo napenda niwashukuru sana na Mungu aendelee kuwabariki. (*Makofi*)

Napenda nichukue nafasi hii Mhe. Naibu Spika, kuwataja waliochangia moja kwa moja.*"Ananitayarishia maji mwanangu siyanywi hayo maji nitajitahidi"*. (*Vicheko/Makofi*)

(Hapa Mhudumu wa Ukumbi alikuwa anamtayarishia maji ya kunywa ni utaratibu wa kawaida)

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe waliochangia moja kwa moja ni pamoja na:-

Mhe. Maryam Thani Juma		
Mhe. Suleiman Sarahan Said		
Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Mchangiaji mashuhuri huyu
Mhe. Abdalla Maulid Diwan	-	Mchangiaji mashuhuri
Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf	-	Mchangiaji mashuhuri
Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wetu
Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mwanasheria huyu anawakilisha viti maalum
Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	(*Diaspora*)
Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Mchangiaji mashuhuri
Mhe. Mussa Fuoum Mussa		
Mhe. Panya Ali Abdalla		
Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Hondari kabisa na makini
Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Mchangiaji wa busara
Mhe. Tatu Mohammed Ussi		

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Anawakilisha watu wanaomuhusu kwa moyo wa dhati sana
Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Msomi wa UWAWAZA huyu
Mhe. Machano Omar Said
Mhe. Shehe Hamad Mattar - Mwenyekiti wetu
Mhe. Said Soud Said (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum)
Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali- Mkereketwa wa Watoto kama ninavyokereketwa mimi
Mhe. Ali Khamis Bakar

Napenda niwapongeze na kuwashukuru sana kwa sababu kwa kuchangia kwenu taifa limesikia mlipokuwa mnachangia kwa sauti. Lakini Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni pamoja na :-

Mhe. Ussi Yahya Haji
Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
Mhe. Nassor Salim Ali
Mhe. Rashid Makame Shamsi
Mhe. Yussuf Hassan Idd
Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Katiba na Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
Mhe. Ame Haji Ali
Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
Mhe. Zaina Abdalla Salum
Mhe. Salma Mussa Bilal
Mhe. Mussa Ali Mussa
Mhe. Saada Ali Mwendwa
Mhe. Waziri wa Habari, Michezo, Utamaduni na Utalii- Jana mlimpigia makofi mengi sana nilidhani na mimi mtanipigia hivyo hivyo, lakini kila mtu na bahati yake
Mhe. Hamida Abdalla Issa
Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Mhe. Naibu Spika, nadhani nimemaliza lakini kama nimekusahau tafadhali niambie na umuombe Mwenyekiti uingie kwenye *hansard*.

Mhe. Naibu Waziri wangu sijakusahau na naomba niwashukuru viongozi Mawaziri na Manaibu Mawaziri walionisaidia kujibu masualsa na naamini

masuala waliyojibu kama nitakosea kuyarudia nikiyarudia nikiyagundua tu nitasema hili limetamkwa na fulani.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali amechangia vizuri sana na amefafanua mambo mengi, kwa sababu Wizara yake anasema wanafunzi, mimi nasema ni watoto wangu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Waziri wangu Bi. Shadya Mohammed Suleiman najua sasa hivi ameanza kuchangamkia tenda na anachangia vizuri, namshukuru sana kwa uchangiaji mahiri na ninaamini mmemuelewa.(*Makofi*|).

Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba nichangie yale ambayo nadhani hayajachangiwa.

Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi ya kusema kwamba kulikuwa na hoja moja ambayo imechangiwa na Wajumbe wengi sana, zaidi ya 27 inayohusiana na kifungu cha udhalilishaji juu ya milioni hamsini na tano. Suala lenu tumelipokea, tutalizingatia na tutakaa na Kamati yetu ya kudumu ya Wizara pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango na Kamati ya Bajeti watakaoweza kutushauri ni vifungu vipi tunaweza kuvitoa na tukavipeleka mahala pengine. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, lakini napenda nielimishe hilo kwanza. Nia na madhumuni iliyosababisha tuweke kwamba kifungu hiki kipate 55 milioni, ilikuwa ni kwa sababu ya uratibu tu, uratibu ni pamoja na kufuatilia kwenda kuangalia kuna shughuli gani. Lakini katika Wizara yangu kuna Kurugenzi nyengine zinazofuatilia masuala ya watoto, masuala ya udhalilishaji ya wanawake ambayo nayo pia yanachangiwa pesa. Ndio maana hata mukiona kwamba kipindi kilichopita tulichanganya pamoja, lakini safari hii ilibidi tuzigawe ili tuweze kuzifanyia kazi kwa karibu zaidi na kuendelea kule. Lakini pia kuna nyengine huwa zinasaidiwa na watu wa nchi za nje ambao kwa bahati mbaya safari hii hawakutuletea mapema, wangetuletea mapema tungeziingiza hapa zingeonekana kwamba ni pesa nyingi. Naomba tu nichukue tu ibaki kwenye *Hansard* kwamba kama itatokezea kuwa hatujafanya vizuri kwa pesa hizi 55, basi mtaelewa ni kwa jinsi gani ambavyo tumefanya, lakini kwa ushauri wenu kwa heshima napenda kuuheshimu na kusema kwamba mawazo yenu ndio yanayojenga nchi yetu. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, naona masuala mengine mengi ambayo nimeshasaidiwa kujibiwa. Lakini pia kuna Mhe. Abdalla Maulid Diwani aliuliza kwamba idadi ya wakoma pale Welezo, nadhani ameshajibiwa na Naibu Waziri Mama

Shadya nashukuru. Pia aliuliza kutokuwepo na madaktari wa usafiri na wazee. Suala hili tumelichukua na tutalifanyia kazi na TV tutahakikisha kwamba wazee wanapata kwa sababu ni kipindi cha kuburudika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nikuambie kwamba kati kati ya wazee wale kuna wengine walikuwa wachezaji wa mipira, kipindi cha mpira wanataka kuona, wengine walikuwa wana muziki wako pale wamestaafu wamekuwa ni watu wazima. Jambo jengine kupata ufafanuzi kuhusiana na vifungu mbali mbali vya Mhe. Jaku Hashim amejibiwa na Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Suleiman Sarahan umeshajibiwa nashukuru.

Mhe. Asha Abdalla Mussa kuhusu idadi halisi ya wazee waliosajiliwa hadi kufikia mwezi Aprili 2017. Mhe. Naibu Spika, idadi halisi ni 27,097. Unguja ni 17,179 na Pemba 9,018. Kati ya hao wazee 25,609 Unguja na Pemba walilipwa pencheni zao. Gharama iliyotumika tangu mwezi Julai, 2016 hadi 2017 ni shilingi bilioni 4,533,180,000. Unguja bilioni 3,169,020,000, na Pemba bilioni 1,364,160,000. Gharama za uendeshaji ni shilingi milioni 161,940,800 Unguja na Pemba ni 56,823,000.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mussa kuhusu je, suala la wazee wasio na vyeti au vyeti vyao havina vigezo linatatuliwa vipi. Napenda kumjibu kwamba Wizara inatumia maafisa wa kwenda kufanya uhakiki kutaka kujua iwapo wanazo stakabadhi nyengine zilizokuwa zikitumika mara baada ya mapinduzi. Pia tunawataka waeleze matukio muhimu katika historia ya Zanzibar, kama mzee ana mtoto mkubwa maafisa huuliza stakabadhi za mtoto ili kujua umri na kuweza kumtathmini mzee huyo. Kwa jinsi hiyo utapata tu taarifa au vyenginevyo wakitokezea watatu au wawili wazee walioko jirani yake wanaomfahamu waliocheza naye ambao wanaweza kuthibitisha kwamba huyu ana miaka hiyo basi anaweza kusajiliwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif aliuliza ni sababu zipi zilizopelekea ajira ya nje kwa nchi za Kiarabu tu na sio nyengine za Ulaya au Marekani. Naomba kumjibu kwamba nchi hizo ndizo zenye fursa nyingi za ajira ambazo hazihitaji sifa kubwa za kielimu. Nchi zilizoendelea hasa za Umoja wa Ulaya, zinapendelea kuajiri watu wasio katika Jumuiya za Ulaya lakini iwapo fursa zitakuwepo basi wananchi wazalendo wanaweza kwenda katika nchi hizo. Lakini mtakumbuka nilisafiri kwenda kuhakikisha kwamba nimekwenda Geneva mwaka jana, katika kuwepo kule niliweza kuwa-*lobby* watu wa *ILO* wakatuwezesha kutaka kuwasomesha, ndio wale watoto walioko Maruhubi ambao walipelekwa watoto 100 wamebakia 60, baada ya wengine 10 kututoroka ambazo hizo ni jitihada za kwenda kuendelea kutafuta sehemu za nje.

Lakini na nyinyi nawaombeni wapendwa wangu, kwenye *WhatsApp* ninawaona sana, mna mashirikiano makubwa sana na nchi za nje, mkipata nafasi basi tuambieni tupate kuwasiliana na mabalozi wanaohusika ili tuweze kuwapeleka watoto wetu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani kuhusu vijana. Ni kwa kiasi gani Shirika la *UNFPA* limewasaidia. Napenda kumjibu suala lake kwamba Shirika la *UNFPA* limesaidia hatua ya ukamilishaji wa sera ya maendeleo ya vijana pamoja na mpango kazi. Mafunzo ya *study* za maisha kwa vijana walionje ya skuli pamoja na kuimarisha Mabaraza ya Vijana.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu hifadhi ya mtoto. Mhe. Suleiman Sarahan Said aliuliza wazazi wanaozaa watoto mapacha zaidi ya wawili, kuna mpango gani. Mhe. Naibu Spika, wengine wanazaa hata hawa watoto wanne. Kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu kawajaalia wanaume wa siku hizi wana rutuba sio za kawaida. Napenda kumjibu kwamba tayari kuna utaratibu wa kuwasaidia fedha za maziwa akinamama wanaojifungu zaidi ya mapacha wawili. Hiyo wizara inatokana na ustawi. Kama unao Mhe. Mjumbe waweke wazi waje wasaidiwe.(*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala lake aliuliza wafanyakazi wa Nyumba ya Watoto hawana mashirikiano. Napenda kumjibu kwamba Wizara haina ushahidi wa kuwa wafanyakazi wa Nyumba ya Watoto hawana mashirikiano. Lakini tunamuahidi kuwa suala hili tutalifanyia kazi na ikibainika hatua zitachukuliwa ili waweze kushirikiana.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kuhusu Mabaraza ya Watoto. Ni kweli yameundwa na yanapatiwa mafunzo ya namna ya kuyaendesha na kufanya kazi zao kwa mujibu wa malengo na maazimio ya kitaifa, kimataifa na utekelezaji wa haki zao.

Mhe. Naibuu Spika, Mabaraza hayo pia yamepewa mafunzo ya namna ya kujikinga na kupambana na vitendo vya ukatili wa udhalilishaji wa watoto, tukishuhudia na picha zinazoonekana sasa hivi watoto saa zote wanajitokeza wakikemea. Pia yamejengewa uwezo wa kuripoti matukio pindi yanapotokea katika maeneo yao. Kuhusu udhalilishaji umepungua au umezidi baada ya kuwepo Mabaraza haya. Hili ni suala ambalo linahitaji utafiti wa kina kwani bila ya kuwa na takwimu sahihi basi huwezi kutambua kama matukio yamepungua au yameongezeka. Lakini ninachofahamu ni kuwa jamii imepata mwamko wa kuripoti matukio hayo, kabla ya hapo watu walikuwa hawaripoti

ingawaje mpaka sasa hivi wengine wanaficha, wanakubaliana wenyewe kwa wenyewe hawaleti taarifa.

Mhe. Panya Ali Abdalla aliuliza kwamba serikali ina mpango gani wa kurikodi maelezo ya mtoto anapotoa ushahidi. Napenda kumjibu kwamba serikali imeandaa Kanuni ya matunzo na hifadhi ya mtoto ambayo zimeeleza utaratibu wa kurikodi maelezo ya mtoto wakati wa kufanyiwa mahojiano katika vituo vya Polisi, kwa kushirikiana na maafisa wa Ustawi ya namna ya kuhifadhiwa taarifa hizo kwa ajili ya ushahidi. Kwa bahati nzuri mnakumbuka Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein ni hivi karibuni tu amepitisha Sheria ya Ushahidi wa Mtoto iliyokuwepo kwa muda wa miaka 100 iliyopita, ambayo imerekebishwa mambo mengi sana ambayo hata mtoto mlemavu leo anaweza kutoa ushahidi na ukaeleweka ukatumika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nadir Abdul-latif aliuliza mgao wa fedha wa Baraza la Vijana. Napenda kumjibu kwamba programu ya maendeleo ya vijana inajumuisha na utekelezaji wa shughuli za Baraza la Vijana shilingi milioni 427,363,000 zinajumuisha shilingi milioni 100 za ruzuku ya Baraza la Vijana. Fedha hizo zitatumika katika kuratibu uendeshaji wa Mabaraza ya Shehia, Wilaya na Kitaifa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said Mhe. Viwe Khamis Abdalla walipenda kujua kuhusu kufanya marekebisho ya Kanuni ya kuanzisha Baraza la Vijana inayohusiana na uchaguzi. Kanuni hatuwezi kuifanyia karekebisho kwa sasa, kwani ni miaka miwili tu tangu ianzishwe. Lakini tunaahidi kuzifanyia kazi changamoto zote zilizojitokeza wakati wa uchaguzi.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani aliuliza kwa nini Wizara imeunda Mabaraza ya Shehia 384, lakini imeripoti Mabaraza 52. Napenda kumjibu kwamba idadi hiyo ya Mabaraza 52 iliyoripotiwa ni Mabaraza yaliyoundwa mwaka ambao yanakamilisha Mabaraza 384 ya Shehia.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kuhusu hoja ya Baraza la Vijana haijaanza kufanyakazi zake vizuri. Baraza la Vijana linaendelea kufanyakazi zake kama kawaida ikiwemo mafunzo, kushiriki katika shughuli mbali mbali za kiuchumi na kitaifa. Napenda nichukue nafasi hii ni juzi tu ukiwepo fedha umeweza kuzindua Baraza la Vijana na Watoto ambalo liko katika hatua hizo tunakupongeza sana na ninaamini litaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hassan Khamis Hafidh amemwambia Mhe. Waziri ahakikishe awalee Baraza la Vijana ili walete tija kwa taifa. Ushauri wako nimeupokea na kuufanyia kazi na wewe ukiwa kama ni kijana basi uwe karibu, usiningoje Barazani njoo ofisini kwangu tupange pamoja, naamini una mchango wa kutosha. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, sasa Kamisheni ya Kazi. Mhe. Ussi Yahya Haji anaomba kupata ufafanuzi kuhusu watoto waliotolewa katika ajira hatarishi ambao Pemba 449 na Unguja 966. Wanawake wangapi na wanaume wangapi kwa kila mkoa na je, Mikoa mengine kulikuwa hakuna watoto kama hao. Kaskazini Pemba wanawake walikuwa ni 111 na wanaume 238, Kusini Unguja wanawake ni 428 na wanaume 538. Tunaendelea kufuatilia na kwa ushirikiano wenu mkituambia wako wapi wanaohangaika itatusaidia zaidi, kwa sababu sehemu nyengine inakuwa ni ngumu kujua kama watoto wanahangaika.

Mhe. Naibu Spika, ajira ya watoto naomba kumjibu kwamba suala la kuwaondosha katika ajira lilikuwa ni mradi kwa maeneo maalum. Hivyo kufikia maeneo yote haikuwezekana Mheshimiwa. Lakini mkazo utawekwa kwa maeneo ambayo hatujayafikia hatua kwa hatua kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mikopo. Mhe. Hassan Khamis Hafidh kuhusu watu waliofaidika na mikopo. Napenda kumjibu kwamba watu waliofaidika na mikopo kwa mwaka 2016/2017 ni wananchi 3,486 wanawake 1944 na wanaume 1,542 kama inavyoonesha kwenye kiambatanisho nambari 3 *page 46*. Kwa mwaka ujao tumepanga kutoa shilingi milioni 600 ili ziwafaidishe wananchi 4,000 wote walionufaika wameondokana na umaskini kwa viwango tofauti.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi alitaka kujua kuhusu ufuatiliaji wa mfuko wa AK na JK. Mfuko wa AK na JK haupo na wadaiwa wa mifuko hiyo wamekabidhiwa Mfuko wa Uwezeshaji. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 34,400,000 kwa Unguja na Pemba zimerejeshwa. Wizara kwa kupitia Mfuko wa Uwezeshaji inawafuatilia wateja wa Mfuko wa AK na JK na kuchukua hatua zinazofaa kwa wasiolipa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ninapenda niwakumbushe tu Waheshimiwa kwamba utaratibu waliokuwa wanakopesha huu ulikuwa kidogo una matatizo, ndio maana utaona Wizara yetu inahakikisha kwamba kunakuwa kuna wadhamini katika vikundi mbali mbali. Utaratibu wa utoaji mikopo hauko wazi. Mhe. Mjumbe anauliza kuhusu utaratibu wa utoaji mikopo umeelezwa wazi kwa

kupitia muongozo wa utoaji wa mikopo ambao unasema kwamba kuanzisha kikundi, kuwa na biashara, kuleta ombi la mkopo, mfuko kutathmini maombi, kutoa mikopo na kufuatilia marejesho.

Mhe. Naibu Spika, napenda kusisitiza kuwa hakuna upendeleo wa aina yoyote katika utoaji wa mikopo hii, wale ambao wanalalamika mara nyengine ni wale ambao wana rekodi mbaya za ulipaji na wengine ni wadaiwa sugu wa Mfuko wa AK na JK.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Suleiman Makame Ali alisema mwaka jana zimetengwa shilingi milioni 600 na gharama za uendeshaji shilingi milioni 41, lakini gharama ni shilingi milioni 232,436,000. Kwa nini iwe hivyo wakati kiwango cha mikopo ni kile kile shilingi milioni 600. Kuhusu mapendekezo ya wanaouza vifaa jumla wasipatiwe mikopo na badala yake wapewe wenye biashara ndogo ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nijibu kama ifuatavyo. Napenda kumjibu kwamba shilingi milioni 41 ya mwaka ni matumizi mengineyo *OC* za Unguja peke yake. Lakini hizi shilingi milioni 232 ni matumizi mengineyo *OC* ya Unguja na Pemba, tunasikitika na pendekezo lako lakini Mfuko unafanyakazi zake kwa mujibu wa muongozo ambao unaeleza aina gani ya biashara ambazo Mfuko unatakiwa utoe mikopo. Hivyo Mfuko hupelekea zaidi ya kutoa mikopo modogo midogo mingi kuliko mikubwa.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar alitaka kujua ni vikundi vingapi vya vijana vimepatiwa mikopo. Napenda kumjibu kwamba vijana 142 walipatiwa mikopo kwa mwaka 2016/2017 sawa na asilimia 65 ya fedha zote zimekwenda kwa vijana. Tafadhali angalia ukurasa namba 5.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis alisema asilimia 7 ya makundi maalum ni makundi yepi. Walemavu wanalalamika kuwa wanapokuja kuomba mikopo wanaambiwa waende Idara ya Watu Wenye Ulemavu, anadai huko ni kuwanyanyapaa. Vile vile apatiwe majina ya vikundi vya walemavu vilivyopatiwa mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu kwamba makundi maalum ya watu wenye ulemavu na watu walioathirika na maradhi ya Ukimwi kwa kupitia Jumuiya ya *ZAPHA+* na vikundi vya watu wenye ulemavu vilivyopatiwa mikopo ni kutoka Tumbatu, Matele, ZANABU Wilaya ya Micheweni Pemba. Wizara yetu haiwafanyii watu wenye ulemavu unyanyapaa wala haitathubutu bali inafanyakazi zake bega kwa bega. Mfano Mjumbe mmoja wa Bodi ya Mfuko

ametoka katika kundi hilo. Lakini katika Kamati ya kuyaadhinisha mkopo mmoja wa wajumbe, ametokea Idara ya Walemavu pia. Kwa hivyo unyanyapaa hautawezekana na tunalaani vitendo vya unyanyapaa kwa sababu mtu akiwa hivyo hakupenda wala hakuomba awe hivyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Panya Ali Abdalla kuhusu fedha wanazopewa wajasiriamali zinakidhi haja na ufuatiliaji wa mikopo ukoje. Napenda kumjibu kwamba fedha wanazopewa zinakidhi haja kwani wanapewa kwa mujibu wa mahitaji yao, pia ufuatiliaji wa mkopo hufanywa mara kwa mara, mkopo wa mtu mmoja mmoja ndio inafanya vizuri zaidi kuliko vikundi.

Mhe. Naibu Sika, kuhusu masuala ya uwezeshaji liligusiwa na Mhe. Zulfa Mmaka Omar, Mhe. Suleiman, Mhe. Asha Abdalla Mussa na kuhusu safari ya maonesho ya wajasiriamali. Napenda kujibu kuwa safari hizi zinaratibiwa na Wizara kwa mashirikiano makubwa na Jumuiya ya Wajasiriamali wenyewe, uteuzi hufanywa na Jumuiya ya Wajasiriamali kwa kufuata vigezo vilivyowekwa na Afrika ya Mashariki, kama uwezo upo wajasiriamali hawa huandaliwa nauli kama haupo huelezwa hali halisi. Wajasiriamali waliopelekwa Uganda wamesaidiwa nauli ya kurudi pamoja na mizigo yao.

Pia napenda kumuelewesha kuwa lengo la kueapeleka wajasiriamali katika maonyesho ni kujifunza na kutafuta masoko ya bidhaa zao. Wajasiriamali wa Zanzibar wamepata usaidizi kupitia taasisi mbali mbali hapa Zanzibar na wapo wanaopata usaidizi kutoka Taasisi za Tanzania Bara, pia wapo wajasiriamali waliojilipia wanyewe. Mhe. Naibu Spika, ninapenda nieleze tu kwamba walipokwenda safari hii Uganda, wamekuwa ni wajasiriamali namba moja katika suala zima la masuala ya viungo na namba mbili katika masuala ya asali. Kwa hivyo wameanza kupata masoko kwa kuambiwa wapeleke bidhaa hizo mahali zinakohitajiwa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa nakuja kuhusu ushirika. Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema vikundi vinasumbuka katika kufungua akaunti benki. Naomba kumjibu kwamba Vyama vya Ushirika havipati usumbufu kufungua akaunti benki. Wizara inavisaidia kukamilisha taratibu zote za kibenki zikiwemo na kuwapa barua rasmi za kuwatambulisha, kuidhinisha kumbukumbu zao na vikao vinavyohitajika. Mhe. Naibu Spika, kuambatanisha hati ya usajili ya majina ya watia saini, baada ya kukamilisha taratibu hizo kikundi kinafunguliwa akaunti ni tofauti na pale mtu anapokwenda mwenyewe kwenda kufugua.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abdalla Maulid Diwani alizungumzia vikundi vya Jimbo la Jang'ombe havijapewa huduma za uwezeshaji wa mikopo. Naomba

kumjibu kwamba Wizara inavipa huduma vikundi vyote baada ya kukamilisha taratibu za kisheria. Hata hivyo kwa Jimbo la Jang'ombe Wizara imewaunganisha na uwezeshaji *SACCOs* na kuwapa huduma za mafunzo ya mikopo kwa vikundi 6 vyenye wanachama 138 na kukopeshwa jumla ya Shilingi milioni 50,900,000/=, kati ya hizo zilizorejeshwa ni milioni 36. Vikundi vilivyofaidika ni pamoja na, "Nia Njema, sijui kama viko kwako Mheshimiwa, Hapakazi, Mshikamano, Wemahauozi, Nguvukazi na Wastara". Naomba kumjibu kwamba Wilaya ya Kaskazini (A) imefanya marejesho mazuri ya mikopo kwa kiwango cha asilimia 80.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ussi Yahya Haji alisema sababu zipi ambazo zimefanya fedha za mkopo zilizobaki kuwa nyingi katika Wilaya ya Kaskazini (A). Sababu zilizotolewa baadhi ya fedha hazijarejeshwa ni baadhi ya mikopo mipya na haijafikia muda wa marejesho. Kwa mfano mtu akiambiwa akichukua mkopo wa kuku, huwezi kumwambia alipe siku ya pili, lazima akae muda atakaokwenda kuuza, akipata mapato akiweza kupata nafasi ya pili anaweza kuanza kulipa. Lakini pia walimaji wa mboga mboga huwezi ukamwambia kapanda inawezekana mvua zisiwepo au maji yasipatikane, kwa hivyo anapoanza kuvuna na maendeleo yakaonekana ndio anapoanza kulipa. Mikopo hurejeshwa kwa mujibu wa jadweli na marejesho ya mkopo.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Panya Ali Abdalla alizungumzia tatizo la masoko kwa bidhaa zinazowasilishwa katika Vyama vya Ushirika. Ni kweli kuna changamoto katika suala la masoko lakini Wizara inashirikiana na Wizara ya Biashara kwa kuwaunganisha kwenye maonyesho na wajasiriamali na soko la Jumapili. Aidha Wizara imejipanga kufanya utafiti wa masoko kwa Vyama vya Ushirika sehemu nyengine mbali mbali.

Mhe. Makame Ali Ussi amezungumzia vikundi vingi vya ushirika vina mitaji midogo. Wizara ina utaratibu wa kuvipatia na kuvihakiki vikundi vya ushirika ili kutambua mahitaji yao. Pia inaendelea kuimarisha *SACCOs* ili kupata mikopo zaidi, wao wanavyoomba ndio tunavyowapa na tunawapowatathmini kazi wanazopewa wanazokuja kuombea ndio tunavyowapa.

Mhe. Nabu Spika, malalamiko ya wanawake kiambatanisho namba 9 kinaeleza malalamiko ya wanawake yaliyoripotiwa kwenye ukurasa wa 21 hadi 22 wa kitabu cha bajeti kimeeleza matukio yaliyoripotiwa katika Vituo vya Mkono kwa Mkono Unguja.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy alisema fedha za utawala zipunguzwe ili ziongezwe kwenye udhalilishaji. Napenda kumjibu fungu la

utawala linaonekana kuwa kubwa kwa vile limebeba mishahara na stahiki mbali mbali za wafanyakazi wa utumishi wakiwemo viongozi wakuu wa Wizara. Jumla ya milioni 1,006,085,551/= sawa na asilimia 62 mshahara na 1,040,166,000/=. Matumizi mengine ya *OC* ni Shs. 645,385,000/=.

Pia napenda kutoa maelezo kwamba fungu la mipango linaonekana kubwa kutokana na kuwa milioni 227,838,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Shs.2,000,000/= zilizobaki ni kwa ajili ya kufanya utafiti, kuandaa sera za mafunzo kazi kwa wanagenzi, kuandaa mpango mkakati wa Wizara, kumalizia sera za uwezeshaji wa sera ya mtoto, kuandaa Sheria ya Hifadhi ya Jamii na kufanya ufuatiliaji wa tathmini wa shughuli za Wizara.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Wanu Hafidh Ameir alizungumzia malipo ya malimbikizo posho za likizo. Wizara imefanikiwa kulipa malimbikizo ya posho la likizo. Utaratbu uliotumika ni kupunguza wafanyakazi 20 kila inapoingizwa fedha na matumizi mengineyo. Kwa sasa Wizara haina limbikizo la posho hilo.(*Makofi*).

Mhe. Panya Ali Abdalla kwa nini kitabu cha bajeti hakielezi malengo. Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu kwamba mfumo wa sasa wa uandaaji wa bajeti kwa kutumia programu unaeleza malengo, kupitia programu hii ya programu ndogo ndiyo hivyo kila programu imeeleza malengo yanayotarajiwa kufikiwa.

Mhe. Rashid Makame Shamsi kuhusu usalama na afya kazini na uchunguzi wa matukio ya ajali. Matukio ya ajali yanachunguzwa na baadae sababu za ajali hizo hutumiwa kwa mafunzo na kuweka mbinu za kukabiliana na sababu hizo kwa sehemu zote za kazi. Matukio ya moto yanashughulikiwa. Hivi karbuni matukio ya wafanyakazi kuungua kwa vipasha moto vya *buffet* vimekuwa vingi. Idara imelifanyia kazi suala hili na marekebisho makubwa yamefanyika baada ya kufahamu kiini cha tatizo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hassan Hamis Khafidh amesema wafanyakazi wa kampuni ya ujenzi wa *ESTIM* Mtoni kwa Bakharesa aliyefariki akiwa kazini. Suala hili limeshafanyiwa kazi na familia yake imeshalipwa fidia kulingana na Sheria ya Fidia. Utaratibu wa kuwawekea Bima wafanyakazi utawekwa vizuri kwenye marekebisho ya Sheria Fidia na Usalama Kazini. Kwa taarifa ya ziada tu ni kwamba huyu amepata zaidi ya mara tatu, amepata *ZSSF*, amepata kiinua mgongo, amesimamiwa kuhakikisha kwamba amepata haki zake zote.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, napaneda kukushukuru na kukupongeza kwa mara nyengine tena pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kwa michango waliyotupa.

Baada ya maelezo haya Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba sasa kutoa hoja na Mungu awabariki sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Umemaliza Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, nimeshamaliza na kwa mara nyengine naomba kutoa hoja, ahsante. Mbarikiwe sana Wajumbe muongeze mshikamano. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika. Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja, sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokata, waliokuali wameshinda.(*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto sasa naomba baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku haiwezekani utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haya nitasubiri mpaka tukae.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tukae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kuhusu utaratbu kuhusiana na Kanuni ya 63.

Nilikuwa nataka muongozo wa kiti chako. Hapo tulipokuwa tunapitisha zamani programu kuu tunasimama Wajumbe watatu, lakini ukiangalia hichi kitabu hii biashara itakwisha muda mfupi na Wajumbe tuko wengi.

Sasa nataka msaada wa kiti chako na muongozo wa kiti chako. Programu zenyewe ndogo ndogo ziko karibu nne tu mpaka tano, biashara itakuwa imekwisha. Sijui umenifahamu au nizungumze kidogo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekufahamu lakini kwenye programu ndogo Mheshimiwa mnaruhusiwa pia watu watatu, kila programu na programu kuu inatajwa lakini zile ndogo pia mnaruhusiwa kupiga buti watu watatu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimekufahamu sana lakini kutokana na hii hali ilivyo, na hii biashara yenyewe ilivyo, itakwisha muda mfupi tu. Mhe. Mwenyekiti, kila Mheshimiwa mmoja atakuwa na hoja mbili au tatu na hii ni bajeti tunayojadili ni ya wananchi. Sasa nilikuwa nataka msaada wa kiti chako na muongozo wa kiti chako.

Mhe. Mwnyekiti: Mhe. Jaku tulikubaliana na ni utaratibu ambao Mhe. Spika ameuleta. Sasa tukubaliane hapa kwamba mfumo utakuwa tu kwenye programu kuu, lakini haina maana kwamba mtu au watu watatu watashindwa kupiga buti kwenye programu ndogo.(*Makofi*).

Tunaendelea.

FUNGU Q 01 - WIZARA YA KAZI UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO.

Kifungu Q01 Wizara ya Kazi Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Jumla Kuu **891,078,000**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU Q 01- WIZARA YA KAZI UWEZESHAJI WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu Q01 Wizara ya Kazi Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto 14,456,640,000

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hapa huwezi kupiga buti bado kupiga buti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili fungu kubwa hili kuna maelezo naomba niyatoe kabisa tukubaliane mwendo tutakaokwenda na naomba unilinde sana, mimi nimeambiwa mzee wa busara basi busara itumike na Kanuni itumike.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema huko tunakokwenda kunako vifungu vikubwa na vidogo vidogo, lile fungu la utawala liko mwisho na maelezo aliyotupa Waziri alisema, Kamati ya Bajeti itakaa na tunajadili pesa katika matumizi, itakaa na Wizara ya fedha baadae waone pahala wa kuhaulisha fedha ili kuliongeza fungu lile ambalo sisi tumelipitia la milioni 55 hakuna fungu jengine linalokwenda ku-*support* zile programu.

Kamati ya Bajeti tuliyonayo ni Kamati ya Ushauri tu kwa Wizara ya Fedha haina *mandate* au hakuna *Act*, tutakapomaliza kupitisha mafungu haya wakenda wakakaa na pesa ihaulishwe kwenda kunako fungu jengine.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tukubaliane tukitoka hapa kupitisha hili fungu kuu, twende kwenye utawala kwanza kabla ya kujadili yale mafungu mengine ili tuone ile busara ya kupunguza mafungu ibaki kabisa kama dhana ya Wajumbe ilivyo, sio kuondoka hapa kwa sababu *Act* inarudia tena, Kamati ya Bajeti hawana *Act* ya kuweza sisi tukitoka hapa wakenda wakaa na Wizara ya Fedha wakaweza kubadilisha, wabadilishaji wa fungu ndio sisi kwa mujibu wa Kanuni. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, na fungu lile la milioni 55 halina sehemu hata moja ambayo nyengine inakwenda ku-*support.* Maelezo yangu ndio hayo nazuia hapa ili nipate ufafanuzi na *Act* kwa Serikali twende mbele vizuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa hili ni Fungu Kuu, hili huwezi kulifanyia marekebisho. Hivyo hili sisi hatuna uwezo wa kuliongeza hili, kinachotakiwa kufanyiwa ni *reallocation*, kama zitapunguzwa fedha kutoka fungu moja kwenda fungu jengine, hilo tunaweza kufanya. Lakini kuliondoa hili Fungu Kuu tukalibadilisha. Hilo halitowezekana hatuna mamlaka hayo.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina dhamira ya hapa. Dhamira yetu Kauli ya Serikali kwanza wafute, kwa sababu watatupiga changa, wafute kwa sababu walisema tukimaliza kupitisha mafungu, tutakwenda kukaa na Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha kuona eneo gani wahamishe fedha. Hilo changa la macho. Maana tukimaliza hapa hakuna *Act* inayowapa *mandate* wao ya kutoa fedha pahala.

Mhe. Mwenyekiti, ninamaanisha tukimaliza kuhoji hapa, twende kwenye utawala tuzuie lile fungu watwambie wenzetu hapa na hapa tunapunguza tunakwenda ku-*support* ile programu ambayo ndio dhamira yetu basi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango tusaidie kwenye hilo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, nimeisikiliza vizuri hoja ya Mhe. Mwakilishi lakini vile vile na hoja zilizotolewa na Wajumbe mbali mbali wakati wa kuchangia kwamba hili fungu limewekewa fedha kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana nao kwamba hizi fedha ni kidogo lakini Waziri alizungumza sababu zilizopelekea fedha hizi kuwa kidogo na miongoni mwa sababu hizo alisema kwamba hizi zinahusika na uratibu tu na ukilinganisha na zile za mwaka jana Mhe. Mwenyekiti kwamba ziliwekwa kimakosa, kwamba zile fedha zilikuwa pia zina fedha za kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kuwa zilikaa kimakosa, lakini fungu hili la Udhalilishaji wa Watoto na Wanawake kuna vifungu vingi vimewekwa katika bajeti lakini pia kuna fedha nyingi za Miradi za Wafadhili ziko katika suala hili.

Lakini pamoja na hayo alisema kwamba yuko tayari akae na Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha tuangalie ile hoja iliyotolewa na Waheshimiwa lakini kuna suala zima la Utaratibu na Kanuni yetu Mhe. Mwenyekiti, kwamba Bajeti hii imepitiwa na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi. Kamati ya Kudumu ilisharidhia na badala ya hapo, ikaja kwenye Kamati ya Bajeti ambayo Kamati ya Bajeti nayo kabla ya kuja hapa iliridhi. Sasa hoja za waweshimiwa wajumbe tutizame pia kwenye Kanuni, ukiangalia kwenye Kanuni ya 98, Kanuni yetu Mheshimiwa Mjumbe ana haki ya kutoa shilingi au kupunguza fungu lakini hata kuwa na haki ya kuongeza mahala pengine na hapo anapopunguza ili awe anasimamia hoja yake ya kwamba haikujibiwa vizuri.

Lakini sio kuongeza fungu yengine, sasa kama tunapitisha, tunapitisha vile vifungu viwe pungufu na baadae sasa Kamati ya Bajeti ije ikaje kufikiria hizo fedha tutazipeleka kwenye eneo hili. Lakini Mheshimiwa Mjumbe hapa kuzuia

hili fungu kubwa haiwezekani kwa mujibu wa Kanuni zetu, twende kwenye programu kama ana hoja na pale kwenye hoja haikujibiwa vizuri hapo aseme na akizuia shilingi au akizuia fedha fulani katika fungu lile Baraza litaamua Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Naam Mhe. Miraji

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mimi nilikuwa nataka maelezo ya Serikali, Serikali kabla ya majibu ya waziri wote wawili nimewasikiliza wa mwanzo kumsikiliza waziri husika, walitoa kauli ya kuwa watakaa na Wizara ya Fedha na Kamati ya Bajeti kuona ndo nikusema mstakbali wa hili, tukubaliane kabisa kwa sababu hii Kamati inayokwenda baada ya kupitisha sie hakuna *mandent* tena ya kwenda kupunguza hilo fungu. Sasa kauli hii anayosema sasa basi tutasubiriana na utaratibu huo wakufanya ili twende hivyo wanavyosema, lakini pale mwanzo nilikuwa nasimamia kuwa wanatupiga changa, wanatuona sisi huku juu tuliko hatukuja humu kwa kuwawakilisha watu wamekuja wao tu kuwakilisha. Sasa hiyo ndo dhamira yangu sasa wakati kauli ya pili ishasafisha kauli ya mwanzo twende tutakwenda kwenye fungu lakini utaratibu naomba Mheshimiwa kiwe kiti chako twende fungu la utawala tuliliwekea dhamira ili kuengeza fungu lile la uzalilishaji.

Na Mawaziri hawa wote walilitupa kauli moja ili twende vizuri kauli yako ilisema kuna maeneo mengine yana *support* programu hii, ukitizama kitabu kizima kimoja baada ya nyengine hakuna eneo linalo *support* programu, kwa hivyo wasitupe majawabu wakatushughulisha watuweke wazi. Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa nataka hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea na mwisho mmekubaliana vizuri.

PQ0101 Programu Kuu ya Uwezeshaji
Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kuchangia niliomba ufafanuzi kwanza nilimtaka Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelezee kwamba fungu hili la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika kitabu chao cha Hotuba walisema kwamba kupitia mfuko huo wa wawezashaji wananchi kiuchumi kulikuwa na pesa milioni mia 600 na wametowa mikopo

milioni mia 600, lakini ukiangalia fedha ulizoomba mwaka jana 2016/2017 ni shilingi milioni mia 527 nilitaka kujua idadi ya halisi ya fedha walizoomba na idadi ya fedha zilizotolewa na zimetumika vipi, kwa sababu utafauti ambao ulioko kwenye kitabu cha bajeti na kitabu cha hotuba.

Lakini pia nisema toka kuanzishwa kwa Bodi, imeanzishwa Bodi ya Mfuko huu wa Uwezeshaji Mhe. Rais kaanzisha Bodi ni vikao vingapi wamekaa toka kuanzishwa kwa Bodi hii. Ahsante sana Mhe.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. kwanza napenda niseme nasikitika inawezekana sijaweza kusoma lakini nilikuwa nishalijibu kwa maandishi nishakuwa nalo hapa baada ya kusaidiwa na wenzangu nimeliruka.

La kwanza ni kusema kwamba hivyo vifungu vinapatikana kwenye programu ndogo, ufafanuzi uko kwenye programu ndogo za huduma mbali mbali ambazo kama tukiendelea zinaonekana wazi.

Nasema hivi hilo fungu analosema Mheshimiwa linaonekana kwenye programu ndogo za huduma, ukiendelea humo utazikuta hizo za maelezo yote anayotaka kuzungumza kwa masuala ya uwezeshaji, lakini lile suala la kusema tumekaa vikao vingapi Mwenyekiti wetu bahati mbaya amekuwa na dharura nyingi sana na nyengine amekuwa akijiuguza kiasi kusema kwamba hatujaweza kupata lakini bado tunaendelea kuwajulisha tunakaa ili tuweze kufanya hili. Kwa sababu sisi tunataka tukusanye pesa nyingi ili kuwahitaji watu wengi hasa katika kipindi hichi ambacho mabaraza ya vijana yameanzishwa tunataka tupate fedha za kutosha. Tutakaa wakati wowote ambao Mwenyekiti wetu atakuwa yuko tayari na nafasi na afya yake iko salama Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha Abdalla Mussa lakini nawaomba niwataje Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa ruhusa hii lakini pamoja na majibu yake Mhe. Waziri bado zijaridhika na kwa sababu katika ukurasa wa 5 katika hotuba yake hii bado tena wamesema imetoa mikopo 341 lakini kati ya mikopo hiyo ni yenye jumla ya shilingi milioni 600 bado naendelea kusimia hoja yangu. Katika kitabu kikubwa cha bajeti kuna fungu hapa wanasema waliomba pesa milioni mia 527 katika fungu hili lao la mwaka 2016/2017 na sio milioni 600 nataka ufafanuzi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. kwa heshima na taadhima napenda nimwambie ndugu yangu na ninapenda kwamba ni mtu anayejali masuala ya hesabu ni changamoto nzuri na nimefurahi sana kwamba anafuatilia atatusaidia sana.

Lakini nataka nimkumbushe tunachozungumzia ni masuala ya uwezeshaji na mikopo, fedha za kutolewa mikopo haziombi bali hutokana na marejesho ya wale waliokopa, wakirejesha nyingi watapewa watu wengi na tunataka sana kwa wale kila waliomba arejeshe mapema iwezekanavyo na ziwe nyingi ili ziweze kuwafikia vikundi vyengine kwa pamoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. tatizo unajua nafikiri Mhe. Waziri tatizo ni *figure* zaidi ndio zinazo majibu yapo. Mhe. Asha kwanza nimsikilize naomba nimpe nafasi Mheshimiwa aliyetowa hoja halafu nitakupa wewe. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti nimeisikiliza hoja nzuri ya Mhe. Asha Abdalla Mussa ukisoma katika programu ya kwanza ambayo ali cot Mhe. Asha ni 527 ambapo programu hii ilikuwa ni uwezeshaji wananchi kiuchumi mwaka jana ambapo mwaka huu tulipanga bilioni moja 1.2 lakini katika sekta ameuliza Mhe. Mwakilishi ya Uratibu wa Uendelezaji ya programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi akitazama iko ile ile mia 600, kwa hiyo hoja yake ambacho tume *target* ndo kile kile kimeweza ku *refless* katika kitabu cha bajeti hakuna tofauti yoyote hukusema vizuri.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kweli mpaka sasa pamoja na majibu ya Mhe. Waziri Nchi (OR) lakini naendelea tena kusema bado zijaridhika lakini nitake kusema kwamba fungu hili kwa upande wangu bado nalizuia. *(Makofi)*

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti wakati nachangia mchango wangu hapa asubuhi.,

Mhe. Mwenyekiti: Naomba tusikilizane.

Mhe. Simai Mohammed Said: Utaratibu Muongozo wako umesimama mtu mara tatu

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Fedha kwanza tumpe nafasi Mhe. Waziri wa Fedha alikuwa na…

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusiana na Kanuni ya 65 (1) inasema mjadala kwenye Baraza utakuwa ni mjadala wa jumla na mjadala wa Kamati ya Matumizi utahusu vifungu makhsusi sasa sijui Mhe. Asha yeye anazungumzia suala la jumla au anazungumzia *specificity* kwenye kifungu hichi cha PQ0101.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti labda mimi sikusoma labda sijui, lakini nnachosema kwamba katika ukurasa 5 wamezungumzia masuala haya ya uwezeshaji lakini katika kitabu chao kikubwa, katika hii programu hii ya uratibu pamoja na uwendeshaji wa programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka jana katika hizo hizo pesa milioni 527 kuna pesa milioni 460 alizosema Mhe. Waziri wa Nchi hapo, lakini kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 hizo milioni mia 600 na. Kwa sasa nataka kujua hivi, hizi pesa waliosema wao katika hichi kitabu cha hotuba yaani uleutafauti, uleutafauti labda sijafahamika au sijui sijafahamu mimi kwa hiyo nilikuwa nataka maelezo kwa kina.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee. *(Makofi)*

PQ0101 Programu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikishangia nilisema kwamba wizara hii 2016/2017 ilisema kwamba inatowa mikopo mia 600 yenye thamani ya shilingi mia 600, na wakatuomba kwamba tuwaidhinishie milioni 41,230 lakini mara hii hii, watoa mikopo hii hii mia 600 yenye thamani ya shillini milioni 600 lakini wataka tuwaidhinishie 232,486 Mwenyekiti samahani, kwa hivyo mimi naomba hapa nikitaka kujua kuna lipi kubwa la kwenda kufanya mara hii hata wakataka hizi milioni 232,486.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti naomba kwa ruhusa nilijibu swali la Mhe. Suleiman Makame kwamba mfuko huu ni *revolving fund* pesa hii inatolewa mikopo inarejeshwa, inaengezwa kwa hizi pesa zimeombwa kuengezea mfuko ambao pesa nyingi zimo mikononi ili ziweke kuengeza wananchi waweze kufaidika na waweze kutumia hii huduma. Na ndio maana hizi pesa zilizoombwa 232,486 kwa ajili ya kukuza mfuko, lakini pesa nyingi zimo mikononi ni *revolving fund* ambazo zinatumika zinarudi unaweza ukakuta hata mwakani pesa ambayo inaweza kurudi ikawa ni

nyingi zaidi ya hii ambayo ipo hapa. Kwa sababu pesa nyingi ziko mikononi wananchi wetu wanarejesha taratibu naomba kuwasilisha Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nashukuru Mhe. Salama kwa kuweza kumsaidia Mhe. Waziri, Uwezeshaji lakini mbona hapa sioni kwamba inasema pesa hii itakwenda hivi hivi, walituandikia tu wanaomba milioni hizi ili kufanya kama yaliyopita yale pale sasa kama ingelikuwa wameeleza kama watafanya hivi maelezo aliyosema Mhe. Salama isingekuwa tatizo, lakini hapo hakueleza hilo kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti hapa naomba tena ufafanuzi sijapata kufahamu uzuri, kwa sababu kama wangeeleza kama alivyoeleza Mhe. Salama kwenye hichi kitabu kwamba kuna moja, mbili, tatu twajua kwamba "kukopa ni harusi kulipa ni matanga" twajua hilo, lakini sasa wangeeleza tu kwamba hizi tukishapata tutafanya hivi tutafanya hivi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Mwenyekiti ahsante wakati nachangia Mhe. Mwenyekiti nilizungumzia suala la mikopo kwa vijana, hapa tunaona kwamba kuna pesa ambazo zinaingizwa lakini kwamba vijana, wanamanunguliko kwamba hii vijana hawapatiwi na wanasumbuliwa sana na katika kitabu nimeona kwamba kuna watu kama 100 na kidogo ambao wamepatiwa mikopo je. Mhe. Waziri nakuomba ulielezee tena kwa sababu sikuridhika kwa sababu wale watu ni kidogo na pesa hizo nazipatia usumbufu kwa hiyo nakuomba Mheshimiwa unipe uhakika wa vijana wangu kupata mikopo nafuu katika fungu hili la pesa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti hapa nimepata funzo moja ambao nalihitaji kwa msaada wako, nipate kupewa nafasi ya kuwapa wawakilishi wangu wajumbe semina, kuhusiana na maswala ya mikopo ili waweze kufaidika vizuri katika maelezo yao. Hivyo wakati watakapokuwa wanaongea tupate lugha moja kwa sababu maswali mengine wanayoengea hapa ni maswala yapo kwenye mipango ya utekelezaji ambayo ya vijana wateendelea kupewa na waliopewa wame hawapewi watu ovyo, huwezi ukampa tu kwa kuwa ni kijana aje aombe pesa umpe hana shughuli anayofanya pasipo tathmini, pasipo ufatiliaji, pasipo utaratibu haiwezekani.

Ndo maana mikopo mingi imepotea huko nyuma sasa hivi lazima wame na vikundi ambavyo vinawasaidia waweze kudhaminiana kwa hiyo Mheshimiwa naomba nipewe nafasi tukimaliza tu tutuwe semina ya kutosha ili na wao waweze kufaidika vizuri, lakini hapa naomba wapitishe hivi vifungu ili tuweze

kufanya kazi na watushauri zaidi tuendelee katika shughuli za kuwasaidia vijana hasa Mabaraza yanaanza sasa hivi ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. uwelewa kweli hatuna sikatai lakini sasa lakini hata yeye mwenyewe katika jibu lake aliniambia kwamba kasaidia vijana mmoja mmoja, na tunajua tatizo la kumsaidia mtu mmoja mmoja, kwa hiyo sasa wakati wa kujibu alikuwa anipe uwelewa wa kutosha kwa sababu yeye hakusaidia vikundi kauli mbiu yake inasema "ushiriki ni nguvu pamoja katika na kuleta maendeleo" lakini sasa hii kauli mbiu alipiga na chini akenda kumsaidia kijana mmoja mmoja, ndo nikataka kumwambia kwamba alieleze vizuri kwamba vijana wangu hawa wa vikundi watapata vipi na mmoja mmoja, wananufaidika vipi na mikopo hii nafuu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. naomba: Mhe. Mwenyekiti naomba nimfafanulie kwamba Mhe. wapenzi wote wawakilishi hili suala linawahusu tunaposema kikundi kimoja kimoja hicho kikundi kinakuwa *registered* kina watu kama watano kama kumi kama iishirini ndani ya kikundi kile mmoja na kuwa na jambo lake analotaka kufanya kuna mwengine anafunga kuku mwengine anataka kuuza mwengine anafungua uwakala mmoja mmoja kwa *interest* zake lakini zinadhaminiwa na kikundi ndio mana tunasema wamoja wamoja mmoja mmoja kutokana na kile kitu anachotaka, naomba tusaidiane tuelimishane vizuri tupige hatua kwa kuwasaidia tusiwachanganye watoto huku nje wakatusikia wakaona kwamba tunafanya mambo sio, nia ni nzuri na tumesimama na tunataka kuhakikisha watoto wanapata ajira za kujitegemea na mchezo wa kuranda nje wishe ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti niliwahi kuwa waziri katika wizara hii na nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jibu lake hilo ni sahihi na naomba nimsaidie kidogo Mhe. Mwakilishi swali lake, hakuna utaratibu wa kumkopesha mtu mmoja mmoja, tunasisitiza tuwakopeshe kwa makundi na wajiunge katika Vyama vya Ushirika au katika kikundi cha ushirika chochote kuanzia kumi na kuendelea, hatuwezi hata mara moja kumpa mtu mmoja mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tunapopeleka kwenye kikundi na yeye yule kijana na yeye yumo kwenye kundi lile, kwa hivyo na yeye anafaidika. Lakini tukisema umpe mmoja mmoja hatuwezi kumaliza kazi hiyo. (*Makofi*).

Kwa hivyo hivi sasa kinachofanyika ni utaratibu mzuri sana kama tunnaambiwa tujikusanye kwenye vikundi ili tuweze kuwasaidia.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mheshimiwa kauli inaweza kumfunga mtu lakini naomba tuendelee.

Jumla ya Programu Kuu ya Uwezeshaji	
Wananchi Kiuchumi	1,212,671,000

Kifungu PQ0102

Mhe. Mwenyekiti: Tunaanza na Mhe. Wanu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii lakini kabla sijaingia kwenye hoja yangu naomba niseme maneno machache.

Mhe. Mwenyekiti, kila siku tunasema kwamba nyeupe itabaki kuwa nyeupe na nyeusi itabaki kuwa nyeusi. Naomba ni ninukuu Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasema:-

"Kuyaendeleza makundi mbali mbali moja ya kazi ya SMZ katika Ilani ya Chama". na inasema "Watoto kama taifa la kesho wanayo haki ya kulindwa kwani ndio chanzo cha raslimali watu na mrithi wa taifa la kesho, watoto wanayo haki, kutoa mawazo, kupata lishe bora, malezi na ulinzi ..."

Hii ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ilani ya ASP sijui inasemaje.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba nimesikia majibu mazuri ya Mhe. Waziri na nampongeza sana kwa kujibu kisiasa. Naomba na hili nalo awapatie mafunzo na wengine na wao wajifunze taaluma hiyo wanaihitaji.

Hoja yangu ni kwamba Mhe. Waziri amejibu kwamba katika fungu hili la Mapambano Dhidi ya Udhalilishaji wa Watoto, hizi fedha zilizotengwa hapa ni kwa ajili ya uratibu tu. Kuna mafungu mengine ambayo pia yana fedha yatashughulikia shughuli hii ya Mapambano Dhidi ya Udhalilishaji wa Watoto. Suala ambalo Mjumbe mwenzangu amesema ameangalia kitabu kizima hajaona na mimi nime- *peruse* sijaona. Labda Mhe. Waziri atu- *direct* ni vifungu gani ambavyo pia vinakwenda kusaidia hili fungu. Hilo ni moja.

Lakini la pili katika hoja hiyo hiyo ni kwamba mwaka jana wamesema hii pesa inakwenda kuratibu hii ya mwaka huu. Najiuliza mwaka jana kulikuwa kunaratibiwa kitu gani cha milioni 451, hata mwaka huu kuwe kuna milioni 55 za kuratibu. (*Makofi*).

Lakini jengine nitahoji mpaka nitakapofika Fungu la Utawala naomba Mhe. Waziri anipe majibu katika hayo niliyoyasema.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kuna *other programs* ambazo zinasaidiwa na mashirika mbali mbali. Lakini nadhani sijui tunafanya programu kuu na ndogo sijui tunafanyaje, hapo Mheshimiwa na mimi naona kama nitahitaji maelezo zaidi. Maana na mimi naona wananichanganya sasa tumeshamaliza kule juu tunafika mahala...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto unatakiwa utoe majibu ya Mhe. Mjumbe, usichanganikiwe kabisa.

Naomba utoe tu majibu kama umelifahamu, kama hukulifahamu tutamwambie arudie lakini naomba utoe majibu.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mheshimiwa naomba arudie sijamfahamu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Wanu naomba urudie.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nadhani ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Wanu Hafidh bila ya maelezo mengi naomba uingie kwenye kifungu moja kwa moja.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: *I am coming* Mwenyekiti. Mhe. Waziri nadhani masuala yangu ameyasikia lakini kinachomchanganya ni kwamba amesema programu kuu na programu ndogo. Sasa kinachomchanganya ni kwamba nyinyi mmepitisha uamuzi wa kupitisha fungu kubwa kwa pamoja.

Kwa hivyo hilo fungu kubwa linalopitishwa sasa hivi, hoja yangu ipo kwenye hili fungu dogo la hilo fungu kubwa.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sasa hivi, fedha hizo zipo kwenye bilioni nane, laki

tano kumi na nne, mia tisa tisini na saba (8,514,997,) ambazo zinatoka kwenye kuimarisha huduma za Ustawi.

Mhe. Mwenyekiti: Programu ndogo iko kwenye ukurasa wa 25.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ndiyo ilipo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, naomba usaidie.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba labda kidogo nitoe ufafanuzi.

Hii Programu ya Udhalilishaji ndani ya Wizara hii kuna Programu nyingi ambazo mara nyingi zinasaidia katika kushajihisha. Mfano *UNFPA* wana programu ndani ya Wizara katika suala zima la udhalilishaji ambalo kikawaida pesa za *donors* haziingii katika kitabu, lakini najua kuna programu ya *UNICEF* wanasaidia udhalilishaji, kuna programu ya *UN Women* inasaidia ndani ya ya Wizara kundi la udhalilishaji.

Kwa hivyo ninafikiri katika hali hiyo pesa hii imewekwa kwa sababu kuna *other donors* ambao wanaisaidia programu hii kwa asilimia kubwa na ni fungu pesa ni nyingi ambazo hazionekani hapa kwa sababu siyo pesa ya serikali. Kwa hivyo nilikuwa naomba tu kidogo nisaidie Wajumbe ili tuweze kupata ufafanuzi kwa sababu hivi vitu tunafanya kazi kwa pamoja na lengo letu ni kufanikisha katika kulinda maslahi ya watoto wetu.

Kwa sababu hakuna mtu hata mmoja anayetaka udhalilishaji uendelee. Sote nia yetu kama serikali kuhakikisha tunapiga vita kwa mashirikiano ya pamoja. Nilikuwa naomba nitoe ufafanuzi huo kwamba *other donors* wana-*support full* katika hii *program* ambayo ndiyo tunakwenda nayo. Ahsante.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, sisi wana siasa tuna ule msemo kwamba wananchi wetu wanasahau sana. Lakini pia leo nime-*note* kumbe pia nayo serikali inasahau sana.

Kwa sababu wanajua kwamba shida tunazopata kupitia wafadhili hasa tunapomaliza chaguzi zetu. Na wanajua tatizo la udhalilishaji ukubwa wake ukoje, hivyo unapangaje kujenga jengo, unaacha *core issue* ambayo nchi ina *face*, yaani ile sijui niseme nini. Yaani lile tatizo lenyewe ukubwa wake na

sensitivity yake unaweka milioni 55 unakaa kitako unasubiri *donors* wakutilie pesa ili uka *solve* lile tatizo.

Lakini pia majibu yao, majibu ya Mhe. Waziri wa Fedha yako tofauti, majibu ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira yapo tofauti na Majibu ya Mhe. Waziri Wanawake na Watoto ambaye ndiye muhusika Mkuu Waziri wa Kisekta yapo tofauti.

Kwa sababu yeye aliposimama kama Waziri wa Kisekta akasema kwamba pesa nyengine zinazo-*support* hii *program* zipo katika bilioni 8. Bilioni nane aliyoitaja yeye hakuna sehemu hata mmoja ambayo kumetajwa programu ya udhalilishaji wa watoto.

Programu ya bilioni 8 aliyoitaja kuna

- Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii,
- Kulipia fidia kwa watu,
- Kuratibu shughuli za malezi ya mtoto,
- Kutoa misaada ya jamii,

Hamna hata sehemu moja ambayo inakwenda kwenye udhalilishaji. Mimi niseme siwezi kuli-*hold* fungu hili kwa sababu siwezi kumega pesa katika fungu hili. Ninachotaka mimi fedha zitoke kwenye *source* nyengine lije kwenye fungu hili. Mimi maneno yangu niliyosema ndiyo hayo lazima serikali iwe na *seriousness* kwenye hili suala la udhalilishaji. Msije hapa na majibu tofauti mkatuvunga vunga, mkafikiri sisi sote *foolish*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Wanu Hafidh lugha unayotumia siyo sahihi naomba ufute kauli yako, naomba ufute kauli yako.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nafuta kauli lakini itakuwa wameshanielewa.

Mhe. Mwenyekiti: Hujafuta bado Mheshimiwa. Futa kauli sema nimefuta kauli yangu, futa kauli.

Mhe. Wanu Hafidh: Mwenyekiti, utakuwa unanilishia maneno lakini nafuta kauli.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, Naibu Waziri alinijibu lakini nilikuwa nataka ufafanuzi tu. Hichi kitabu mimi narudia tena elimu yangu ni ndogo, hichi kitabu HQ 010201106 imeandikwa mia moja kumi na mbili milioni lakini Naibu Waziri alipokuja akasema, kasema milioni 12. Hebu nielimisheni hichi kitabu, siyo maneno yangu. Unajua kusema huwezi kuja kukamatwa lakini maandishi yana uzito wake unaweza hata kufungwa, lakini nielimishwe.

Mhe. Mwenyekiti, hapa hapa pana pesa tunaweza tukazipunguza tukazileta hapa. Tuangalie hizi milioni 55 na milioni 50 za mbio za mwenge. Mbio za mwenge majimboni kwetu tunachangishwa. Tuangalieni lipi lenye uzito, kudhalilishwa watoto au mbio za mwenge ndiyo zenye uzito. Hoja zangu ni mbili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nimeshakusikia Mheshimiwa kaa upate majibu. Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alisema lakini nafikiri Waheshimiwa Wajumbe hawakumfahamu sawa sawa.

Lakini zipo fedha zilizotengwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ninaweza kutoa mfano mdogo kwamba kuna programu ya Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii ambayo ina karibu *four hundred millions*.

Lakini pia ukitizama kuna programu nyengine ya *Child Protection* ya *UNICEF* ukiangalia kwenye *page* ya 30 kuna karibu milioni 300 kwenye zile programu katika ukurasa wa 30. Sasa hoja ni kwamba fedha hizi zipo, lakini zimo na zimekuwa *distributed* katika miradi au *program* mbali mbali na katika shughuli nyengine.

Lakini wakati niliposaidia kujibu suala la mwanzo Mhe. Mwenyekiti, nilisema hivi:-

"Kwamba pamoja na yote hayo, fedha hizi zimo lakini hoja ya Waheshimiwa Wajumbe kwamba zile milioni 55 ni kidogo nilikubali kwamba kweli ni kidogo, lakini zipo njia mbili:

Njia ya kwanza ni kukaa na Kamati na Wizara inayohusika baada ya kusikiliza hizi hoja na kupitia vifungu vyote na programu zote tukajua kama inawezekana ndani ya Kamati kukafanyika *reallocation*.

Njia ya pili baada ya kupitisha bajeti hii, bado upo utaratibu wa kisheria wa kwamba Waziri mwenyewe anao uwezo wa kutizama vifungu vyake na kufanya *reallocation* kwenda kwenye lile eneo la msingi, uwezekano huo wote upo".

Mhe. Mwenyekiti, ningewaombe tu Waheshimiwa Wajumbe wakakubali tukapitisha vifungu hivi bado *concern* yao tumeisikia imepokelewa na itazingatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kusema hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa naomba mukae.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango nimekuelewa vizuri sana na nafikiri wanachokitaka Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba ifanyike *reallocation* fungu hili liongezewe fedha na wanachokitaka ni kwamba kwenda katika mfumo wa kuwa kuna Kamati ya Bajeti ambayo pamoja na Wizara ya Fedha wakae pamoja ili waone watatoa katika mafungu gani na kuyaongezea kwenye fungu ambalo linahusiana na suala la udhalilishaji. (*Makofi*).

Nafikiri hilo ndilo Waheshimiwa wanalolitaka. Kwa hivyo *option* ya kwanza mimi nafikiri ulilolisema ni sahihi kabisa.

Na hilo tunaweza sisi kama Baraza kufanya maamuzi hapa kuliweka kando kuendelea kuliacha lile ili Kamati ya Bajeti ilisimamie hilo.

Kwa hivyo Mheshimiwa ulivyosema ni sahihi kabisa, *option* ya mwanzo ni sahihi kabisa. Naam nimekuruhusu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, nimekufahamu vizuri na kama Waheshimiwa Wajumbe watakubaliana na hoja yangu.

Hoja yao ni ya msingi lakini badala ya kuzuia hapa kupunguza fungu sasa hivi, kwa sababu hatuwezi kuongeza sasa hivi kwenye fungu jengine kwa sababu Kanuni hairuhusu hivyo. Kinachowezekana ni kwa Waheshimiwa Wajumbe kuzuia kutoa shilingi katika fungu hili ambalo mimi nahisi tusifike huko.

La msingi ni kwamba sisi tutakaa kwa sababu bado kuna vifungu vingi ambavyo vina fedha zitakazokwenda kwenye masuala ya udhalilishaji wa wanawake na watotot zimo humu. Ni suala la kwenda kukaa na kufikiria jinsi

gani tuta vi-*harmonies* hivyo vifungu ili lile suala la kuhakikisha kwamba udhalilishaji wa wanawake na watoto unapata fedha za kutosha hilo tutalifanya.

Lakini bado kuna *provision* baada ya kupitisha bajeti hii Mhe. Waziri mwenyewe anayo nafasi hiyo ya kufanya uhaulishaji. Nisingependa tukazuia fungu lolote kwa sababu uhaulishaji upo na Waziri ataufanya, tusiufanye ndani ya Baraza ndiyo kitu ambacho nakizungumza mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa hilo hatuwezi kulifanya hapa kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha ni sahihi kabisa, itabidi Kamati ya Bajeti ndiyo ikae pamoja na Wizara kwa ajili hili sasa hivi tunaweza kuendelea na vifungu vyengine, lakini kauli hii jamani ni kauli ya Kamati hii tuliyokaa.

Kwa hivyo haiwezi serikali kwenda kinyume na kauli hii na ni kwa mujibu wa Kanuni zetu. Mheshimiwa. Mhe. Machano, aah! mwenye hoja Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, ...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa umakini wako na kuniona.

Mhe. Mwenyekiti, hichi chombo kinaongozwa na Kanuni. Kanuni ya 98 naomba uniruhusu niisome.

Mhe. Mwenyekiti: Isome.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu cha 98, "Masharti ya Hoja ya Kupunguza Fungu".

"Hoja ya kupunguza fungu lolote kwa mujibu wa fasili ya (7) (c) - (g) ya Kanuni hizi haitokubaliwa isipokuwa kama:-"

Nakuja Kifungu (6) "Mjumbe yeyote anaweza kutoa hoja ya mabadiko juu ya fungu lolote la makadirio ya Matumizi, isipokuwa hakuna Hoja itakayotolewa kwa ajili ya kuongeza katika fungu lolote".

Kwa hivyo tunaweza kupunguza fungu.

Hoja yangu mimi nauliza umuhimu wa mwenge milioni 50, leo tunaacha kadhia hii ya milioni 50 kwa wanawake na watoto.

Lakini vile vile Mhe. Waziri kanipa darasa nzuri, ndiyo niliposema mimi *simultaneous equation* ina njia mbili ya ku-*solve, substitution method* na *elimination method*. (*Makofi*).

Hapa Mhe. Waziri katika fungu hilo hilo 300 mwisho, Mhe. Waziri aliandika kuna fungu la huduma kuna *seven billions* chini hizo hakuna mtiririko wake kuna milioni tatu na laki moja, halafu kuna pesa ya maendeleo.

Mimi jina langu Jaku. Mheshimiwa mwengine akaja akanita Haji. Maana yake kichwa kimoja lakini unabadilisha kofia hicho hicho. Bado tuna hoja. Sijui umenifahamu Mheshimiwa. Hapa hapa pameandikwa *seven billions*.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa naomba umalize hoja yako tuweze kuendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tupunguze fungu la mwenge. Majimboni kwetu tunachangia mwenge.

Mhe. Mwenyekiti: Yameshatolewa maamuzi hapa Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aah! tunachangia majimbo mwetu.

Mhe. Mwenyekiti: Haya kaa kitako Mheshimiwa, naomba ukae.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri nimo katika Kamati ya Uongozi wa Baraza na kwenye kikao cha Kamati ya Uongozi tulijadiliana sana umuhimu wa kuanza bajeti za Wizara kabla ya Bajeti Kuu za Serikali.

Na sisi ambao tulipendekeza kwamba tufuate Kanuni kwa kusoma Bajeti za Wizara, tulikuwa tuna hoja kwamba kunaweza kukawa na mabadiliko ambayo yakafanyiwa mabadiliko baada ya Kamati yetu ya bajeti kukutana na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa utaratibu na naomba wenzangu waelewe kwamba tunatakiwa tupitishe vifungu kama vilivyo, baadaye baada ya Kamati ya Bajeti na Serikali kukubaliana, Serikali itakuja na *schedule amendment,* kwamba tunafanyia marekebisho ili bajeti yetu ikae sawa. (*Makofi*).

Vyenginevyo vyovyote itakuwa tunakwenda kinyume na utaratibu wa kibajeti. Hatuwezi kupitisha bajeti nusu ya Wizara, kwamba fungu hili lilale, fungu hili lipitishwe na pia hatuna mamlaka ya kuongeza fungu. Kwa hivyo tuiwachie

Kamati yetu iamini na nafikiri tuna siku nne ya Kamati yetu kujadiliana na Serikali, *otherwise* zile siku nne zitakuwa hazina maana.(*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pana makosa hapa kidogo. Hii Wizara imefanya.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 25 naomba tupaangalie, kuna *seven billions*, kuratibu uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto yatima.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku tunajadili fungu hili hili tunajadili kitu chengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimo katika kuleta mawazo ndio fungu hili hili.

Mhe. Mwenyekiti: Fungu hili hili au tunajadili kitu chengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimo katika kuleta mawazo, ndio fungu hili hili uliangalie hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Maelekezo Mhe. Jaku ameyatoa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, ameyatoa Mhe. Machano Othman Said, mimi nimeyazungumza maelekezo ni kwamba sisi uwezo wa kuongeza hapa hatuna kwa mujibu wa Kanuni hatuna. Kinachotakiwa tufanye sasa hivi, tuwape maelekezo Serikali wende wakafanye marekebisho ya kuongeza hili fungu, kitu hicho tumekubaliana na *Hansard* zitazungumza.

Sasa Serikali italeta *Schedule of Amendment* hapa na sisi tutaridhia hilo. Sasa kuna tatizo gani hapa Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kuchangia mawazo ungenisikiliza kwanza halafu kama liko sawa, sawa, Haliko sawa tunasubiria hayo mengine, huo ni mchango tu.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea Mhe. Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Uratibu wa Uendeshaji wa Vituo vya Kulea Watoto, hili fungu limewekwa sehemu tatu na nakupa ushahidi wake sasa.

Kuratibu Uendeshaji wa Kulelea Watoto HQ010301104 bilioni saba, laki tisa (7,000,900,000). Huku alisema Mhe. Waziri wa Fedha kuna *child protection* milioni mia tatu hamsini (3,050,000) ndio hii hii, hapatoshi hapo kuna milioni tatu vile vile...

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mheshimiwa mawazo yako hayo mengine yapeleke kwenye Kamati ya Bajeti, yafikishe kwenye Kamati ya Bajeti ili Kamati ya Bajeti waweze kulifanya hilo.

Mhe. Nadir

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nina suala langu jengine katika nilipochangia.

Mhe. Mwenyekiti: Halihusiani na hili

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Inahusiana na Kukuza Usawa wa Kijinsi, kifungu hichi hichi

Mhe. Mwenyekiti: Hili tumeshamaliza Mhe. Nadir, tumemaliza umechelewa. Mhe. Wanu

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Serikali walivyosema kwamba Kamati iende na utaratibu waliosema ni mzuri tu, lakini kwa sababu katika fungu hili hatuwezi kuongeza fungu na sisi ni kazi yetu kupunguza. Sasa fungu hili tusiachie Kamati hivi hivi tulipitishe lakini na marekebisho ili huku mbele tuangalie tunapunguza wapi na Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha itakwenda kukaa kuangalia ni sehemu gani pakuongeza kwenye lile fungu ambalo tunalisimamia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Wanu hilo jambo ambalo unalitaka wewe sio kazi yetu hapa sisi. Hapa sio kazi yetu. Kanuni hazisemi hivyo. Kamati ya Bajeti ndiyo maana yake, tuna Kamati ya Bajeti itafanya shughuli hiyo Mheshimiwa. Naomba unikubalie hilo.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Mhe. Mwenyekiti, imebidi nisimame kuwasaidia Wajumbe wangu na ninaomba sana waiamini Kamati ya Bajeti. Kwa sababu Kamati ya Bajeti iko *straight* haimpendelei mtu, wala haitorubuniwa na mtu, itakwenda kwa mujibu wa Kanuni tunavyokwenda, tutaleta mapendekezo yetu kadri tutakavyoona tumekaa na Serikali na tukikwazana tutawambia hapa tumekwazana, waamuzi watakuwa ndiyo wao. Kwa hivyo naomba watuamini tuendelee Mheshimiwa. *(Makofi)*

***Mhe.* Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti tunaendelea

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Mawaziri tumeyapata, lakini na ninukuu yale ya kwako zaidi ile *Schedule of Amendment* ambayo inaletwa mtatuletea kabla ya Bajeti Kuu ya Serikali au mtatuletea lini, tupate kauli hiyo ya Serikali ili tuone tutakapokuja mwisho huko hawa wenzetu wamezingatia tuliyoyapanga au wametupiga changa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Wakati wa Kamati ya Bajeti itakapowasilisha ripoti yake. Kwa hivyo Kamati ya Bajeti ndio itatoa maelezo ya mabadiliko hayo *Schedule of Amendment* itakuja kabla ya Bajeti Kuu ya Serikali, tunaendelea.(*Makofi*).

Kifungu PQ0102	Programu Kuu ya Kukuza Usawa wa Kijisia na Uendelezaji wa Wanawake	302,702,000
Kifungu PQ0103	Programu...	

Mhe. Mwenyekiti: Tunaanza na Mhe. Nadir baadae kuna Mhe. Viwe halafu anafuata Mhe. Abdalla Diwani.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri Castico kwa uvumilivu wake, nampenda sana dada yangu. *(Makofi)*

Naenda kwenye suala niliochangia kwanza kwenye udhalilishaji, nilizungumza hawa wanawake wenye jinsia moja nchi hii wamezagaa wengi.

a) Wizara itachukuwa hatua gani haijaja kunijibu ya kufuatilia haya mambo kusitisha kama alivyokuwa anafanya Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi.

b) Nilizingumza suala la watoto wanaobakwa na kudhalilishwa. Je, wizara yake imefanya utaratibu gani au inafanya vigezo gani vya kuweze kuhakikisha na Wizara husika inasitisha haya mambo kwa nguvu zote.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri. Waheshimiwa tunapojenga hoja zetu twende kwenye mafungu. Hapa tunazungumzia bajeti zaidi kuliko utendaji, twendeni kwenye mafungu ili tuweze kupitisha hii bajeti lakini tukianza kuuliza masuala lakini endelea Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nasema masuala haya mengine kama ulivyozungumza kwamba

kuna mambo hayapimiki, kuna mambo huwezi ukathibitisha, sheria za nchi zinakataza mambo yote yasiyofaa na ni masuala ambayo mengine hata kuyaeleza yanakuwa ni magumu. Lakini kwa kuwa ni utaratibu unaofanyika na nyinyi ni mashahidi wengine, kama kweli kuna watu unawajua wa namna hiyo si kuna utaratibu, wengine ni tabia inapaswa kuendelea kuwafundisha, kuwashauri, kuwaombea, kuwasaidia na kuwaepusha. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mheshimiwa hata sijui niwambie nini, maana munapozungumza munanigusa ndani ya nafsi ambayo inaumiza sana. Naomba tuendelee kushirikiana ili tuweze kujenga nchi yetu na kila mmoja anayehusika ahusike, kama unamjua mtu anashughulika mtafute umshauri, inawezekana kwanza mambo yenyewe hakuanza mwenyewe kwa hiari, alianziwa na mtu halafu akaachiwa kwenye mataa, kabaki anaendelea hana jinsi ya kujisaidia.(*Makofi*).

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafahamu labda kakusudia niwataje. Sasa mimi nitaomba tuendelee lakini nitaomba hilo suala wanawake wenzake awahimize yeye anaowajua.

Mhe. Mwenyekiti: Jamani jitahidini muweke nidhamu ya Baraza, msijisemee tu maneno ambayo yanaleta taswira mbaya ya Baraza hili nakuombeni sana. Nyinyi mnafahamu wewe ukisema neno linafsiriwa, unaposema neno wengine wanatafrisi wanajua maana umekusudia nini Mheshimiwa. Kwa hivyo naomba sana wakati tunapozungumza hapa tuwe tuna nidhamu ya Baraza.

TAARIFA

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti. taarifa. Kwani Mhe. Mwenyekiti, unataka kuniambia Zanzibar hakuna wanawake *lesbian*, maana yake mimi nimezungumza udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti: Aah! kaa kitako, mimi sijakuruhusu kaa kitako

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Tuendelee

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimtaka Mhe. Waziri aje anieleze kuhusiana na ruzuku ambayo kuwa wapatiwa Baraza la Vijana Taifa. Ninashukuru Mhe. Waziri katika maelezo yake alinieleza kuwa kuna milioni mia moja (100,000,000) ambazo huwa zimeandaliwa kwa ajili ya Baraza hili la Vijana kama ni ruzuku, lakini kwenye kitabu hichi ambacho walituwasilishia sijaiona hiyo milioni mia moja

(100,000,000) na kwenye buku kubwa pia sikuiona hiyo milioni mia moja (100,000,000).

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aniambie kwenye kitabu hichi pesa hiyo imeainishwa wapi ili na mimi niweze kiunga mkono bajeti yake hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukijibu kila wakati, lakini naomba niseme tena kwa mara nyengine kwamba kuna mambo mengine hayaoneshwi humu. Ruzuku, miradi ya wafadhili wengine ambayo inaahidiwa italetwa na kama ruzuku iko kwenye *queue.* Kwa hivyo naomba tuendelea kuvumiliana na kuaminiana Waheshimiwa kwamba hizi milioni mia moja (100,000,000) zimewekwa kwa nia nzuri ya kuwasaidia ipo kwenye *queue* .

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tizama ukurusa wa 26 huduma ya mwisho kabisa

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: 10302 ukurusa wa 26 Maendeleo ya Vijana.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Mhe. Viwe

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, naomba anionyeshe kifungu gani sisi tuko hapa kwa ajili ya wananchi wetu na Baraza la Vijana ni chombo ambacho kuwa aliahidi mwenyewe Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Viwe angalia kifungu cha HQ01030207 Uratibu wa Uendeshaji wa Mabaraza ya Vijana wametengewa milioni mia moja (100,000,000).

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Tuendelee

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa nachangia nilizumza juu ya suala zima la kadhia pale pale Baraza la Vijana. Niliona shilingi milioni mia nne na ishirini na sasa (427,000,000).

Sasa nikamwambia anipe mchakato lakini alinipa mchakato wa *one hundred million* (100,000,000) hii hapa iko chini. Hivi ni kweli tuna Mabaraza ya Wilaya 11, tukigawa hii nafikiri tutapate *eight point three millions* kwa kila

Wilaya. *Is this serious* katika kuyafaidisha haya Mabaraza kuona lile lengo lililokusudiwa la Mabaraza kujiendeleza katika masuala mbali mbali ya elimu na ufanisi wao, *is this serious* kweli kwa milioni nane laki tatu (8,300,000) kwa kila Baraza la Wilaya bado hujagawa kwenye Shehia. Kwa mfano Shehia zangu Wilaya ya Mjini nia Shehia 55 tugawe kwa milioni nane na laki tatu (8,300,000), nini tutafanya katika hicho.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri majibu

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, hesabu anayosema ya kugawa, sijui anataka tugawe kwa kutafuta vigezo vipi. Kwa sababu kuna Shehia nyengine ni ndogo, nyengine ni kubwa. Halafu hii pesa ni kwa ajili ya vijana, Uratibu wa Uendeshaji wa Vijana Mabaraza ya Vijana, sasa sijui ni ipi unayoitaka.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie.

Katika maelezo yako uliyozungumza, naomba ninukuu kitabu cha kwako hiki, wala si maneno yangu mimi, kupitia programu, eeh! umeniruhusu katika ukurasa wa 27.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba uende kwenye vifungu sio mjadala, jenga hoja yako katika kile kifungu. Endelea

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sio mjadala. Sasa yeye mwenyewe anasema haujui. Humu kwenye kitabu kayaandika, sasa nataka kumsomea aliyoandika humu.

Yeye kaandika kuhusu Baraza la Vijana kupitia Programu ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka wa fedha 2017/2018 itajenga uwezo Mabaraza, Katiba za sekretarieti, kuwapatia vifaa kwa ajili ya kuendesha shughuli zake. Sasa katika hapa ndiyo mimi nikakamata nikasema imetengewa milioni mia moja (100,000,000) kutoka katika hili fungu la milioni mia nne na ishirini na saba (427,000,000), tuko sawa sawa hapo.

Mhe. Mwenyekiti, nikamuuliza tukisema tugawe kwenye Wilaya, tuna Wilaya 11, Mabaraza ya Shehia 11, tukigawa milioni mia (100,000,000) itakwenda kwenye milioni nane na laki tatu (8,300,000). Je, hiyo *sensibility* ambayo iliyozungumzwa kwamba itajenga uwezo wa Baraza la Vijana, kweli hizi pesa zitakwenda bado hajaangalia katika Shehia, tulisema katika Wilaya tu na kila

Wilaya kama nilivyosema inatofautiana ukubwa wake sijui namna gani, atajua yeye mwenyewe kutokana na wingi wa Shehia zake.

Je, *it is serious*, jamani tuka *serious* katika suala hili kama kweli tumeanzisha Sheria ya 2016 Sheria Nam. 13 ya Mabaraza ya Vijana.

Kwa hivyo tenga pesa kama hizi, hatuoni kama bado kama tunafanya masihara tunataka kufa lakini kuzimia hatuwezi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Abdalla Maulid Diwani ya kwamba kuna shilingi milioni mia moja (100,000,000) na akazigawa kwa Mabaraza yote tisa (9), kwa sababu hii hapa inazungumzia suala la Uratibu na Uendeshaji wa Mabaraza.

Lakini ukitizama kwenye fungu hilo hilo, mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana ambao kuna karibu milioni mbili na nane zinawalenga hao hao. Lakini ukifungua ukurasa wa 28 kuna suala la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kuna karibu milioni mia nne (4,000,000), ni makundi hayo hayo, vijana wanaingia. Kwa hivyo huku kuna masuala ya uendeshaji wa Mabaraza ya Vijana wenyewe lakini pia katika suala zima la uwezeshaji na mafunzo ya stadi zinawalenga makundi hayo hayo.(*Makofi*).

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, si sahihi kusema kwamba milioni mia moja (100,000,000) na unagawa kwa idadi ya Mabaraza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Diwani naomba tuendelee, muda nafikiri ameeleza uzuri Mhe. Waziri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa lakini nafikiri ni haki yangu kuhoji, naomba unipe ruhusa hiyo niendelee. Najua dokta kanielewesha kidokta, sawa lakini mimi bado akili yangu sijafahamu, juu ya dokta kasema lakini nasimamia mimi ninachokiamini siku zote.

Mhe. Mwenyekiti, katika hii milioni mia moja (100,000,000) iliyowekwa hapa na kwenye kitabu chake narudia tena mambo yale yale japo kanisomea nimeangalia humu sijapaona pale niliposoma angalau pakanijenga uwezo lakini madhali dokta kasema wacha tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea

Kifungu PQ0103 Programu Kuu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi 8,940,360,000

Kifungu PQ0...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hata kifungu hakijasomwa bado, endelea Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwanza nimsifu sana Mhe. Waziri kwa *improvement* kule kwa wazee Sebleni na kule Welezo kwangu. Lakini nilipokuwa nachangia Mheshimiwa nilionesha nia niliomba vitu viwili. Niliomba mkataba wa mzabuni anao-*supply* chakula Sebleni kwa sababu alikuwa anafanya dhulma.

Pia Mhe. Mwenyekiti, niliomba kopi ya malipo ya miezi mitatu iliyopita, kwa sababu chakula walichokuwa wanalishwa na Serikali ilichokuwa inalipa ilikuwa haifanani, yote niliyaomba haya. Lakini halikadhalika Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Wazee na nilisema nitakamata mshahara wa Waziri.

Mfuko wa Wazee Mheshimiwa ulikuwa unapigwa changa, sasa pia nikajua wizara yenyewe ilituambiwa kuna ripoti inaandikwa kutoka kwa *CAG* dhidi ya kufanya utafiti ya mfuko wa wazee. Je, ile Ripoti ya kwa *CAG* pia niliuliza imefikia wapi, yote sikujibiwa. kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, naomba majibu na ninaomba na kopi zangu ili niruhusu kifungu hiki kwa sababu nina uhakika chakula walichokuwa wanalishwa hakiendani na Serikali kilichokuwa kinalipwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hiki siyo nafikiri kifungu sicho, hiki kinahusiana na Uendeshaji wa Uratibu wa Wizara.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kwa mimi Uendeshaji wa Uratibu wa Wizara ambayo ndio inafanya mambo yote hapa, ukiangalia huku kifungu hiki hiki ndio kina mpaka Utawala na Uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti: Sipo hapa Mheshimiwa, sipo hapahusiani na hoja yako hapo, sio hii haihusiani na hoja yako Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, hapa ndipo panapo Utawala, hapa ndipo panapo mshahara wa Waziri na nilitangaza nia ya kuuzuia mshahara wa Waziri. Kwa uwono wangu mdogo hapa ndipo kifungu hiki kina Utawala na Uendeshaji.

Kama Mhe. Mwenyekiti, hapa sipo najua wewe mwenzangu ni mzoefu naomba unioneshe kwa heshima na taadhima palipokuwa ndipo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nasema kuanzia hizi kopi zipo hapa sasa nimekuwekea mahususi, lakini nampeleka Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Keshapata Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Majibu keshapata na mshahara wangu usizuiwe, maana yake utaniweka pabaya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. Mimi nataka ufafanuzi kidogo naomba Waziri anisikilize kwa makini kabisa. Tuko katika maendeleo ya vijana karibu shilingi 427 milioni, lakini mashaka yangu...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba ukae.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa bado tunaendelea na Kamati ya Matumizi na muda umeshafika wa kumaliza, hivyo ningemuomba sana Mhe Mwanasheria Mkuu atengue Kanuni ya Muda kwa ajili ya kuweza kuendelea kumaliza na bajeti ii ya leo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu karibu.

KUWEKA KANDO KANUNI YA 23 (4) YA MUDA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe leo wamechangamka sana basi naomba tuwaongezee muda ili wapate kuchangamka zaidi. Kwa mantiki hiyo naomba tutenge kando kanuni ya 23(4) ili tuongeze muda mpaka hapo tutapomaliza kupitisha bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokata, wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Hoja yangu naomba Waziri na mimi anisaidie anielimishe, nataka niangalie hiki kifungu chenyewe SQ010302 Maendeleo ya Vijana imetengewa shilingi 427 milioni.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hata kuanza hatujaanza subiri kwanza kaa kitako. Mhe. Hassan Khamis Hafidh ulikuwa unasemaje.

UTARATIBU

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana mikataba imekuja lakini pia niliuliza kuhusu ripoti ya kwa *CAG* dhidi ya Mfuko wa shilingi 20,000 ambayo inaandikwa imefikia wapi? Jibu sikupata.

Mhe. Mwenyekiti: Ripoti ya *CAG* hatuijadili sasa hivi Waheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Sijauliza kuhusu kujadili, hoja yangu niliyouliza najua inaandaliwa imefikia wapi ripoti ya *CAG* kuhusu Mfuko wa Shilingi 20,000 sio kujadili.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh mimi nimeielewa na bahati nzuri huyo *CAG* yuko chini ya wizara yetu na *CAG* anafanya kazi kwa mujibu wa maelekezo anayopewa.

Sasa hili suala lina utaratibu wake kama tulivyowasilisha zile ripoti za *CAG* za matumizi ya Mashirika ya Serikali pamoja na Wizara, tumewasilisha kwa hatua ya mwanzo na tungojee na hiyo hatua ya pili itakapofika tukijaaliwa kwa utaratibu ule ule itakuja hakuna wasi wasi, hakuna cha kuficha.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaanza na Mhe. Jaku Hashim baadae atakuja Mhe. Wanu Hafidh Ameir tutamaliza na Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi. Mimi nilikuwa nataka kupewa elimu kidogo kufahamishwa. Narudia yale yale kuwa elimu yangu ni ndogo.

Kifungu cha SQ010302, Maendeleo ya Vijana imetengewa shilingi 427 milioni nafikiri Mhe. Mwenyekiti umeiona.

Mhe. Mwenyekiti: Mbona tumemaliza huko Mhe. Jaku Hashim, tumeshakipitisha hiki kifungu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ndio tulipofikia.

Mhe. Mwenyekiti: Hatuwezi kujadili kifungu ambacho tumeshakipitisha, nakuomba ukae tuendelee na wengine. Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi lakini wakati nachangia katika mchango wangu fungu hili hasa ndio nilisema kwamba nalizuwia kwa sababu sikuwa na imani nalo na sikupata maelezo mazuri kutoka kwa Waziri.

Lakini fungu hili hili ndilo ambalo nilishauri Kamati ya Bajeti kwamba wanapokwenda kuangalia na wakikaa pamoja na Wizara ya Fedha, basi waliangalie fungu hili kwani kuna mambo mengi ambayo yamejificha katika fungu hili.

Nadhani Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ananisikia. Lakini pia tulijibiwa hapa kwamba hata kukipelekwa shilingi bilioni moja basi zinakwenda kutafunwa na udhalilishaji utabaki pale pale, lakini mimi simlaumu mjibuji kwa sababu hapo ndipo upeo wake wa fikra unapofikia. Mimi naamni tukipeleka pesa na zikifanyiwa kazi ipasavyo basi haya mambo yatapungua katika jamii yetu.

Sasa hili mimi naomba tuendelee lakini namtanabahisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwamba katika fungu moja ambalo la kuangalia ni hili. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa nili-*announce* kwamba nazuwia hili fungu, sasa hivi nalirejesha rasmi na naiachia Kamati ya Bajeti ikafanyie kazi lakini niikumbushe tu serikali kwamba *sometime they have to swallow their pride and suppressed their eagle.*

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mimi sina azma ya kuzuwia kifungu chochote isipokuwa nataka ufafanuzi tu. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kuhusu suala la wazee kule Pemba kupatiwa ulinzi. Mhe. Mwenyekiti, niko kwenye Kifungu SQ010403, Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kusema chochote kwanza niende kwenye Hotuba ya Mhe. Rais aliyoieleza humu ndani ya Baraza kwamba wazee ni hazina na chemchem ya busara, hekma katika jamii kutokana na udhaifu waliyonao katika maisha na serikali inaheshimu mchango wa wazee katika kuwapatia maendeleo pamoja na malezi na maadili mema wanayotupatia wazee wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikitaka kujua tu kwamba wale walinzi kule Limbani walionao ni watu wa kawaida ama ni vikosi kutoka serikalini. Nataka kujua hapo tu.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba Mheshimiwa anaendelea kufuatilia masuala hayo ya Pemba na yeye kama ni mtu ambaye yuko Pemba anaweza kuwa anatupa *feedback* nzuri zaidi.

Suala ni kwamba hawa walioko sasa hivi ni wa kawaida lakini tutafanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba wanapatikana vikosi na hasa baada ya kwamba tumejenga uzio na utakuwa na geti inakuwa ni rahisi zaidi kufuatilia ulinzi.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana mimi sitakuwa na mengi isipokuwa namuomba Mhe. Waziri kwamba lifanyike hili kwa sababu mlinzi unapomuweka pale hata kama bakora humpi likitokea tatizo yeye mwenyewe huenda akaenda mbio. Kwa hivyo naomba alichukue hili alifanyie bidii kwamba vikosi vipatikane waweze kukaa pale.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea. Aah, sitaki kufundishwa kazi nasema tunaendelea, nimesema tunaendelea. *(Makofi)*

Kifungu PQ 0104 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wiara ya Kazi, UwezeshajiWazee, Vijana, Wanawake na Watoto 2,943,297,000

Kifungu PQ0105

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kuhoji vifungu ni sawa lakini mimi nakwenda kwenye suala ambalo nililizungumza na ni suala muhimu katika nchi yetu Unguja na Pemba.

Nilizungumza wana utaratibu gani kwenye vijana wetu wengi waliokuwa hawana kazi katika taasisi za *private sectors*. Kuna watu nchi za wenzetu mfano watu wa Unguja, Wazanzibari lazima kwenye sehemu yoyote basi asilimia 50 isishuke wawe wameajiriwa. Wazanzibari hawana kazi wanadhulumiwa wanawekwa watu ambao hawana maana. Wazanzibari wanaweza kazi Mhe. Waziri hajanijibu, wanafanya utafiti gani au wana sera gani kuhusu Wazanzibari halisi kwenye kupewa ajira mahotelini, kwenye viwanda na sehemu nyenginezo wanapata Wakenya na watu wengine wasiohusika. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima ni kwamba muajiri yeyote anapotaka kuajiri anaajiri mtu anayemuhitaji na mwenye sifa husika. Tumejitahidi na tunaendelea kujitahidi sana kuwashajihisha vijana wetu kwanza kuwafundisha namna gani wanaweza kuhojiana na waajiri na pia tunawahamasisha sana *certificate* zao zinapopelekwa kwenye sehemu za ajira, wengi wanataka wanaokwenda kuajiriwa wakiwa na "C" tatu ukiwa hasa na somo la Kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu wengi wanaishia kuwa na "D" na mara nyengine hata "C" moja hawana. Lakini hilo pia halijatuvunja moyo, tunaendelea kuwafundisha, wanaendelea kufundishwa angalau Kiingereza waliofanikiwa katika Kiingereza kwenye *interview* za ana kwa ana licha ya kukosa sifa wanaajiriwa na sheria ipo ya kuajiri watu wa nchi inayohusika ambapo kama hawapo ndipo wanapoajiri wageni. Kwa hivyo nawaomba Waheshimiwa washiriki na wazazi wote wanaonisikiliza tuwashajihishe watoto waweze kuandaliwa ili waweze kuajirika na waweze kuwekwa katika maeneo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la kuchekesha ni pamoja na sisi kwamba jitihada tunazofanya ni juzi tu tumewapeleka watoto Maruhubi Chuo cha Utalii, katika vitendo vya mazoezi tumewapeleka mia moja sasa hivi wamebakia sitini na

tano nadhani. Katika mazoezi ya jambo dogo tu katika yale masuala ya kutafuta namna gani ya kubeba sahani wamekwenda pwani kwa kuwa ni karibu na pwani wanatia pale kana kwamba ni zoezi la kubeba sahani na chakula ndani yake. Mheshimiwa alipoingia mtoto pale kaingia kasema mimi siwezi mchezo huu wanamngoja aje aripoti kwenye darasa ameshaacha skuli.

Sasa tunasema tunaendelea kujitahidi kuwabembeleza watoto wetu na kuwafundisha na kuwashajihisha na wengine wote wamesema hatuwezi mambo haya ya kutumwa kutumwa lakini pia wanakuwa na dharura nyingi. Tuwasaidie watoto wetu wanapokwenda kuajiriwa hata maofisini ukiangalia wanaoajiriwa na serikali wana bahati, kwa sababu hata zile dharura wakiwanazo wanakwenda, lakini kwenye *private sectors* huwezi kuwa na dharura ukaacha kazi. Kwa hivyo naomba tuendelee kuwashajihisha na kuwasaidia ili waweze kuajirika, *otherwise* sheria inafuatiliwa na mimi ni mmoja wapo mkereketwa kuhakikisha kwamba vijana wanapata ajira ndio maana nakesha kutafuta wapi vijana wetu waajiriwe. Ahsante.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri mimi hajanifahamu Mhe. Waziri.

Kwanza nataka kueleza kidogo tu Wazanzibari wako *fit* na wanaweza kazi. Haya maneno yanayosema kwamba Wazanzibari hawawezi kazi wanaweza Tanzania Bara na Wakenya, hili suala mimi sikubaliani nalo, Wazanzibari wanaweza kazi na wako vizuri na wamesoma na katika nchi yetu Kiingereza sio kipaumbele, sisi Waswahili, Kiswahili mwanzo Kiingereza ni *part two.* Ajira wanaweza kufanya kazi ijapokuwa kwenye hoteli, mimi kwenye *Hotel Industry* niko mwaka wa 12 kuna sehemu za ajira hazitaki Kizungu. Mimi nimeuliza sera yao nini kwa Wazanzibari kwenye masuala ya *private sectors* wameweka vipi masharti *between ministry* na *private sectors,* sera yao nini kuhusu masuala ya kazi ili waweze kusaidiwa Wazanzibari hawapewi kazi kwenye *private sectors*.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri amelijibu lakini amelitolea na mifano mengine, amejibu kwamba sera ipo kwamba kwanza wachukuliwe na hata Katiba yetu inasema na mara nyingi tunasikia kwenye redio wanapotangaza wanatangaza kazi ingawa za serikali, lakini nyengine pia Mzanzibari kwanza, si ndio. Lakini amelijibu ametoa na mifano kwamba vijana wetu wakati mwengine wanakuwa hawaajiriki kutokana na sifa. Mheshimiwa kubali tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, basi mara ya mwisho kabla sijakubali kuendelea mfano mdogo Hoteli ya Melia ina wafanyakazi 360 miaka ya nyuma, wafanyakazi ambao *housekeeping cleaner* na wengine si chini ya 220 ambao watafanyakazi ambazo hazihitaji elimu kubwa. Lakini ninachotaka mimi anambie sera yao katika *private sectors* wameweka asilimia 50 lazima Wazanzibari wawemo au asilimia ngapi.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria usaidie, aah! Mhe. Rashid.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana napenda kumjibu Mhe. Nadir Abdul-latif kwamba sera yetu hususan katika Sekta ya Utalii na kuajiri ndani ya sekta za utalii ni lazima kama alivyosema Mhe. Waziri na nampa pongezi sana kwa alivyolifafanua wazi wazi.

Sera yetu inakutaka kwanza umuajiri Mzanzibari kwa nafasi zote ambazo kuanzia chini za bustani, kutandika vitanda, kufagia zote mpaka unafika kwenye meneja. Endapo hoteli itakosa Mzanzibari ambaye hana sifa ya kuajiriwa pale atakapokosekana ndio ataajiriwa mgeni.

Sasa kipi kinachotokea kwenye hoteli za kina Melia, *Park Hyatt* na hoteli za Lagema na nyenginezo, lazima tukubali hizi ni hoteli za *five star*, wana vigezo vyao vya kufikia kuwaajiri watu. Wazanzibari wetu wanashindwa na vigezo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni juzi tu Hospitali ya *Global* wametakiwa watu kwenda kuajiriwa ma-*nurses* wetu wana *diploma* lakini wanashindwa hata kuzungumza neno la kuulizwa hali na yule daktari ambaye anatakiwa amsaidie ili aweze kumpa majina ya mgonjwa na *terminology* zile za udaktari. Kwa hivyo kutokana na ukosefu kama huo kwa Wazanzibari wetu najua ni hodari, wavuvi wazuri, wakulima wazuri lakini wanapofika kwenye ujuzi mwengine wa kazi ndugu zetu wanashindwa na wakati mwengine wanapopewa kazi za mfululizo wana tatizo Mhe. Mwenyekiti, anaweza akapewa kazi kwa mujibu wa masaa yalivyo, watu wetu hawakuzowea kufanya kazi kwa mujibu wa kazi zinavyotakiwa kufanywa, ukimpa kazi ya masaa sita yeye umemuumiza kesho kaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, zipo sera na sera zinawalinda watu wetu, *research* tumezifanya juu ya mambo haya na watu wetu tunawapeleka, lakini bado kuna

tatizo kidogo tuendelee kuwaelimisha wananchi wetu, tuendelee kuwapa elimu ndugu zetu, nafasi zipo na zipo katika njia zote za sekta ya *private*.

Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri wakati mwengine tunapojibu tunakuwa tunajiingiza kwenye serikali.

Kwa sababu unaposema watu hawawezi basi sehemu ambazo zinasomesha nyingi ni za serikali. Mimi ninachotaka kuzungumza kwa sababu kwenye masuala ya hoteli mimi nina mwaka wa 12 na nimeshafanya kazi kwenye hoteli karibu tano kubwa, sawa kwenye *Park Hyatt* lakini wapo Wazanzibari ambao pia wamesoma wanaweza kufanya kazi *Park Hyatt*, wapo ambao wanaweza kufanya Melia, sera haifuatwi Wazanzibari hawajaajiriwa kwenye mahoteli. Mimi natembea kila siku mahotelini na mimi nataka anihakikishie Mheshimiwa kwamba sera hii haifuatwi kwa sababu Wazanzibari kazi hawapewi kwenye mahoteli sio kigezo cha *five stars*.

Mhe. Mwenyekiti, tukitizama kwenye nchi za wenzetu kuna wakalimani hata kama kuna *nurse* hajui Kizungu...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri maelezo yanatosha, hayo mambo mengine.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mheshimiwa tuendelee lakini sera haifuatwi.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa tunaendelea. Tumemaliza watu watatu tayari.

Kifungu PQ 0105	Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote	1,055,610,000
	Jumla Kuu	**14,456,640,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha

Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa ni pamoja na mabadiliko.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Au pamoja na mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali Makadirio hayo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Soma tena mabadiliko.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba nisome tena. Ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo.(*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo wa Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ameshatoa hoja, wanaokubaliana na hoja hiyo wanyoeshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba tusikilizane. Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na timu yake yote na Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote, lakini tungewaomba sana yale ambayo yamejitokeza leo hapa yafanyiwe kazi. Kwa sababu ni ahadi na yatarudi tena hapa ndani ya Baraza na yatatupa changamoto kubwa kama hayakutekelezwa. Kwa hivyo tunaomba sana yale ambayo serikali imeahidi hasa katika marekebisho ya mafungu ambayo serikali imeahidi kwamba yatafanyiwa kazi yafanyiwe kazi. Naomba sana serikali yote iko hapa.(*Makofi*).

Lakini jengine niwapongeze sana Waheshimiwa Wawakilishi *backbenchers***.** Nawapongeza kwa changamoto ambazo wamezitoa kwa serikali. Lengo sote tunajenga nyumba moja. Kwa hivyo nia na lengo la kuingia katika vifungu na kujenga hoja ni kuhakikisha kwamba bajeti inayopita itaweza kutekelezeka

vizuri. Kwa hivyo ningeomba sana kwamba hapa tuliyoyazungumza hakuna kumlaumu mtu, huyu kafanya hivi, huyu kafanya hivi hapana, sote tulikuwa na nia moja ya kutengeneza.(*Makofi*).

Baada ya kusema hayo machache niseme tena kwamba pongezi kwetu sote kwamba bajeti hii imeweza kupita vizuri.

Sasa basi, nichukuwe nafasi hii kuahirisha Baraza hadi kesho saa 3: 00 asubuhi.

(Saa 2:00 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 24/05/2017 saa 3:00 asubuhi)